# MADA: "ULINGANISHI WA MOFOFONOLOJIA YA KISWAHILI NA KIDAWIDA."

NA: HANAH CHAGA MWALIWA

"Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya "Master of Art", Chuo Kikuu cha Nairobi."

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY

0271283 4

August 2000.

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya Digrii katika chuo kingine chochote.

**NA: HANAH CHAGA MWALIWA**
**(Mtahiniwa)**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii Chuo Kikuu.

**DKT. KITHAKA WA MBERIA**

**MARGARET W. NJUGUNA**
**(Wasimamizi).**

## TABARUKU

Kwa wazazi wangu Boniface Mwaliwa na Josephine Chao kwa kunielimisha na kunipa shime katika masomo.

Pia kwa ndugu zangu Joseph Mwanjala, Fredrick Mwamghunda, Cromwel Mwadeghu na Moses Mwaliwa, ambao wamenipa moyo katika harakati za masomo haya.

Vilevile kwa mume wangu James Akanga ambaye amekuwa mstari wa mbele kunihimiza katia bidii katika masomo pamoja na kunisaidia kila inapohitajika.

Mwisho ni kwa Chuo Kikuu cha Nairobi kwa kugharamia masomo yangu ya M.A.

## SHUKRANI

Napenda kutoa shukrani zangu kwa wote waliochangia hapa na pale katika ufanisi wa utafiti huu.

Kwanza nawashukuru wazazi wangu ambao wamejitoa mhanga kunielimisha.

Pili nawashukuru wasimamizi wangu Dkt. Kithaka wa Mberia na Bi, Margaret Njuguna ambao wamenipa mwongozo na mawaidha mengi yaliyofanikisha kazi hii.

Aidha nawashukuru walimu wangu Prof. Abdulaziz, James Michiris,
Dkt. Kineene wa Mutiso, Tom Mboya Olali ambao pia wamenisaidia na mawaidha hapa na pale.

Hali kadhalika nawashukuru wenzangu Bernard Orina, Mark Kandagar, Emmanuel Satia, Baongoli na Mwalimu Akida tuliopitia mkondo mmoja wa masomo. Wao pia wamemsaidia si haba kwa mawaidha yao hapa na pale.


Vilvile nawashukuru mabwana Willis Mwatumia, Renson Mbogho na wengine pale maktabani ambao hawakuchoka kunisaidia kila ninapowaendea, kwa huduma za maktabani pamoja na maelezo mengi yanayohusu utafiti huu.

Pia napenda kushukuru msaidizi wangu katika utafiti huu Bw. Willis Mwatumia ambaye hakuchoka kunipa maelezo na data zilizohitajika kwenye utafiti huu.

Mwisho nawashukuru wapiga chapa wa kazi hii Rehema, Eliud, Alinda, na wengineo.

Shukrani, na Mungu awabariki.

Map No. 2




Prepared by DRSRS

## DHAHANIA

Utafiti huu una lengo la kulinganisha fonolojia ya Kiswahili na Kidawida. Katika sura ya kwanza tuna malengo ya utafiti ,pamoja na maelezo ya umuhimu wa utafiti huu. Kwa jumla sura ya kwanza ni muhtasari wa jinsi utafiti huu utakavyoendeshwa.

Sura ya pili ina mambo mawili. Kwanza kuna orodha ya mfumo mzima wa fonimu za Kidawida zikiwa ni za irabu na konsonanti. Pili, kuna orodha ya ngeli-nomino za Kidawida.

Sura ya tatu inaonyesha mifanyiko sita ya kifonolojia inayotokea katika Kidawida.

Katika sura ya nne tutalinganisha Kiswahili na Kidawida kwa kuzingatia vigezo viwili. Kwanza, tutalinganisha mifumo ya fonimu za Kiswahili na Kidawida ili kuona vile zinavyotofautiana na kufanana.Pili, tutalinganisha mifumo ya fonimu za Kiswahili na Kidawida kwa kuzipima na zile fonimu za Bantu-mzazi,ili tuone vile zinavyotofautiana na kufanana na Bantu-mzazi.

Sura ya tano pia ni ulinganishi wa Kiswahili na Kidawida kwa kutumia vigezo viwili. Kwanza, tutalinganisha motisha ya mabadiliko ya kifonolojia yanayotokea katika Kiswahili na Kidawida. Pili tutalinganisha upeo wa sheria za kifonolojia katika Kidawida na Kiswahili tuone ni kwa vipi zinalingana au kutofautiana.

Sura ya sita tutaona hitimisho ya utafiti huu. Tutaeleza matokeo ya utafiti huu kwa muhtasari. Pili tutatoa maoni au mapendekezo kuhusiana na utafiti huu. Mwisho tutatoa maoni ya kijumla kuhusu Kiswahili na Kidawida.

# YALIYOMO

## SURA YA KWANZA

UKURASA

1.0 Utangulizi - 1
1.1 Kiswahili - 3
1.2 Tatizo - 3
1.3 Malengo ya utafiti - 4
1.4 Umuhimu wa somo hili - 5
1.5 Mapitio ya vitabu - 5
1.6 Upeo na mpaka - 9
1.7 Msingi wa nadharia - 10
1.8 Nadhari tele - 11
1.9 Methodolojia - 11

## SURA YA PILI

2.0 Utangulizi - 12
2.1 Dhana ya fonimu na jozi – mlingano finyu - 13
2.2 Fonimu za Kidawida – irabu - 16
2.3 Fonimu za Kidawida – konsonanti - 18
2.4 Fonimu za Kidawida – nusu irabu - 26
2.5 Fonimu za Kidawida – Hitimisho - 27
2.6 Ngeli – nomino za Kidawida – Utangulizi - 28
2.7 Ngeli – nomino za Kidawida - 29
2.8 Hitimisho Tambishi - 37

## SURA YA TATU


| | | | |
|---|---|---|---|
| 3.0 | Utangulizi | - | 40 |
| 3.1 | Kudondoshwa kwa irabu | - | 41 |
| 3.2 | Kuundwa kwa nusu – irabu | - | 48 |
| 3.3 | Ukaakashaji | - | 52 |
| 3.4 | Mkubaliano wa irabu | - | 53 |
| 3.5 | Kuathiriwa kwa nasali na kitamkwa kinachofuata | - | 57 |
| 3.6 | Kuimarika kwa sauti | - | 59 |
| 3.7 | Hitimisho | - | 61 |
| | **Tanbihi** | - | 63 |


## SURA YA NNE


| | | | |
|---|---|---|---|
| 4.0 | Utangulizi | - | 64 |
| 4.1 | Ulinganishi wa fonimu za Kiswahili na Kidawida kutoka kwa Bantu-mzazi | - | 65 |
| 4.2 | Ulinganishi wa fonimu za Kiswahili na Kidawida | - | 65 |
| 4.3 | Hitimisho | - | 70 |
| 4.4 | Ulinganishi wa fonimu za Kiswahili na Kidawida kutoka kwa Bantu – mzazi – Utangulizi | - | 71 |
| 4.5 | Fonimu za Bantu – mzazi dhidi ya fonimu za Kidawida na Kiswahili | - | 71 |
| 4.6 | Hitimisho | - | 77 |
| | Tanbihi | - | 78 |

**SURA YA TANO**


| | | | |
|---|---|---|---|
| 5.0 | Utangulizi | - | 79 |
| 5.1 | Ulinganishi wa motisha katika Kiswahili na Kidawida | - | 81 |
| 5.2 | Kudondoshwa kwa irabu | - | 81 |
| 5.3 | Kuundwa kwa irabu | - | 84 |
| 5.4 | Ukaakashaji | - | 86 |
| 5.5 | Mkubaliano wa irabu | - | 87 |
| 5.6 | Mkubaliano wa nasali na kitamkwa kinachofuata | - | 91 |
| 5.7 | Kuimarika kwa sauti | - | 91 |
| 5.8 | Hitimisho | - | 92 |
| 5.9 | Ulinganishi wa upeo wa sheria katika Kiswahili na kidawida | - | 94 |
| 5.10 | Kudondoshwa kwa irabu | - | 94 |
| 5.11 | Kuundwa kwa nusu – irabu | - | 95 |
| 5.12 | Ukaakaishaji | - | 96 |
| 5.13 | Mkubaliano wa irabu | - | 97 |
| 5.14 | Mkubaliano wa nasali na kitamkwa kinachofuata | - | 101 |
| 5 15 | Kuimarika kwa sauti | - | 102 |
| 5.16 | Hitimisho | - | 104 |
| | **Tanbihi** | - | **105** |


**SURA YA SITA**


| | | | |
|---|---|---|---|
| 6.0 | Utangulizi | - | 106 |
| 6.1 | Muhtasari wa matokeo | - | 106 |
| 6.2 | Mapendekezo | - | 111 |
| 6.3 | Hitimisho | - | 112 |
| | **MAREJELEO** | - | 113 |

# SURA YA KWANZA.

## 1.0 UTANGULIZI

Utafiti wetu una lengo la kulinganisha za Kiswahili sanifu na Kidawida kwa kurejelea mifumo yao ya kiisimu. Lugha hizi mbili zinatumiwa humu nchini Kenya

Kimbololo ni moja ya lahaja anuawai za lugha ya Kidawida inayotumiwa na wazungumzaji – wazaliwa wa eneo la Taita – Taveta. Lahaja za kidawida zimeenea kemaeneo katika wilaya hii, Lahaja ya Kimbololo inatumiwa na wazungumzaji – wazaliwa wa Mbololo, lahaja ya Kimghange inatumiwa na wazungumzaji – wazaliwa wa Mghange, Werugha, na Wundanyi, lahaja ya Kimwanda inatumiwa na wazungumzaji – wazaliwa wa Mwanda, nao Wabura hutumia lahaja ya Kibura, Wakishamba hutumia lahaja ya Kishamba na Warong'e hutumia lahaja ya Kirong'e kwa kuwa hatuwezi kushughulikia hizi zote, inatubidi kuchagua moja kwa ajili ya utafiti wetu. Tutashughulikia lahaja ya Kimbololo.

Kulingana na utafiti wetu, lahaja ya Kimbololo inaonekana kuwa imejitenga na lahaja zingine za Kidawida kwa kiasi kikubwa. Tunapata kwamba kimaeneo, Mbololo ipo katika nyanda za chini ya Wilaya ya Taita – Taveta, ikilinganishwa na sehemu zingine kama vile Wundanyi, Werugha, Mghange, Bura, Kishamba na Rong'e. Pili hali ya ukame hutawala wakati mwingi katika sehemu ya Mbololo hivi kwamba ukosefu wa mvua na uhaba wa chakula huikumba eneo hili karibu kila mwaka. Kijiografia eneo la Mbololo limepakana na sehemu mbalimbali za nchi ya Kenya. Tukiangalia ramani tunaona kwamba Mbololo imepakana na Kajiado, Kitui, Tana – River, Kilifi na Makueni kwa upande wa nje, huku ikiwa imepakana na maneno mengine ya Taita – Taveta kwa ndani. Mbololo inatambuliwa kiutawala kama kata, ikiwa na kata ndogo kadha zikiwemo Tausa, Ndome, Mraru, Ghazi na Wongonyi miongoni mwa zingine. Pamoja na hayo kata ya Mbololo ni sehemu ya mbuga ya Wanyama wa Pori la Tsavo. Wakazi wa hapa zaidi ni wakulima wa mimea kama vile mahindi, mihogo, mbaazi na kunde. Vilevile wao ni wafugaji wa ng'ombe, kondoo na mbuzi

Kiisimu pia tunaona tofauti kati ya lahaja ya Kimbololo na zile zingine, kwa mfano lahaja ya Kimbololo hutumia fonimu ya konsonanti ya mtuo [j] mahali ambapo lahaja zingine za Kidawida zinatumia [dz]

| 1. Kimbololo | lahaja zingine za Kidawida | Maana |
|---|---|---|
| [ j ɔ s ɛ ] | [ d z ɔ s ɛ ] | lote |
| [ m j i s ɛ] | [ m d z i s ɛ ] | mlishe |
| [ m ji j ɛ ] | [ m d zi ɣ ɛ ] | msichana mdogo |
| [ik a ji ] | [ ik a d z i] | kiazi |

Aidha lahaja ya Kimbololo hutumia [d ] mahali ambapo lahaja zingine zinatumia [ t ],

| 2. Kimbololo | lahaja zingine za Kidawida | Maana |
|---|---|---|
| [idamwa] | [itana] | sasa |
| [idakoni] | [itakoni] | sasa |

Vilevile Kimbololo hutofautiana na lahaja zingine katika matumzi yake ya [g] badala ya [ ɣ ] katika baadhi ya maneno kama vile,

| 3. **Kimbololo** | **lahaja zingine za Kidawida** | **Maana** |
|---|---|---|
| [igi] | [iɣi] | yai |
| [gua] | [ ɣua] | nunua |
| [iguɔ] | [ iɣuɔ] | jana |

Hizo ni baadhi tu ya mifano inayoonyesha tofauti za kiisimu baina ya lahaja ya Kimbololo na lahaja zingine za Kidawida.

## 1.1 KISWAHILI SANIFU

Kiswahili ni lugha ambayo imewahi kufanyiwa utafiti na wataalamu wa isimu hasa wale waliotoka nje ya bara Afrika kama vile Edgar C. Polome, W.H Whiteley, Edward Steere, Jam Knappert, Dr Krapf, Carl Meinhof na wenginco. Utafiti wa lugha ya Kiswahili uliendelezwa sana na wasomi wa Uropa ambao waliweka msingi wa somo la Kiswahili.

Baada ya Wageni kurudi kwao, Waafrika walichukua jukumu la kuendeleza usomi wa lugha ya Kiswahili, hasa baada ya kusanifishwa kwa lahaja ya kivinguja. Hivi leo Kiswahili sanifu kimeenea katika eneo kubwa la bara Afrika. Ingawa Bakari Mohammed (1982) anashukulia kuwa lugha ya Kiswahili huzungumza na wakazi wa mwambao wa Afrika Mashariki kutoka Somalia hadi visiwa vya Komoro, ieleweke kwamba hivi sasa Kiswahili kimeenea hadi sehemu za bara kama vile Tanzania bara, Kenya, Uganda, Rwanda, Congo Kinshasa na Jamhuri ya Demokrasia ya Congo. Vile inavyoonekana, Kiswahili inaelekea kuwa lugha mawasiliano barani Afrika.

Si ajabu basi utafiti unaendelea kutekelezwa kwa lugha ya Kiswahili hususan Kiswahili sanifu. Juhudi hizo zitasaidia kukiimarisha zaidi kwa minajili ya majukumu yake nyeti barani Afrika.

## 1.2 TATIZO

Kumefanywa tafiti nyingi kuhusiana na mofofonolojia linganisha kati ya Kiswahili na lugha zingine za Kibantu, Mifano tuliyonayo ni kama vile D.M Mukuriah (1987) aliyelinganisha mofolojia ya Kiswahili sanifu na Kikikuyu cha Kiambu. Profesa Mohammed Bakari (1982) naye alizilinganisha lahaja anuwai za Kiswahili zikiwemo Kiamu, Kimvita, na Kivumba miongoni mwa zingine katika kiwango cha mofofonolojia. C. Maghanga (1990) naye amelinganisha mofofonolojia ya Kiswahili sanifu na lahaja zingine za Kiswahili hasa Kitumbatu, Kimakunduchi na Kipemba. Vilevile Maringah (1987) amelinganisha Kiswahili

sanifu na lugha ya Kimbeere katika kiwango cha mofofonemiki iliyohusu zaidi unyambuaji wa vitenzi.

Mbali na kazi hizo zinazohusiana na Kiswahili, tafiti nyingine zimefanywa kulinganisha lugha mbili au zaidi za Kibantu katika kiwango cha mofofonolojia. Kwa mfano Kithaka wa Mberia (1981) amelinganisha mofofonolojia ya lugha za Kibantu zinazotumiwa sehemu ya kati ya Kenya ikiwa ni pamoja na Kitharaka, Kiambu, Kimbeere, Kikuyu na Kikamba. Aidha Margaret W. Njuguna (1992) amelinganisha mofofonolojia ya Kiswahili sanifu, Kikuyu cha Kabete na Kikikuyu sanifu. Kazi hizi zote zimechangia mno katika mtalaa wa isimu-linganishi hasa kwa upande wa lugha za Kibantu.

Katika kudurusu na kupitia kazi mbalimbali za kifofonolojia, tumepata kwamba hakuna mengi yaliyotafitiwa na kuandikwa kuhusu lugha ya Kidawida, hasa inapolinganishwa na lugha zingine za Kibantu hususa Kiswahili. Kazi tulizoziona kuhusiana na lugha ya Kidawida zimetaja machache kuhusu masuala ya kiisumu kama vile fonolojia. Kazi ya G. Righa (1978) ambayo ni ya kimofolojia, ilishughulikia lugha ya Kidawida japo kwa ufupi sana. Kutokana na pengo hili tumeona kuwa ipo haja ya kushughulikia kwa undani na upana zaidi mofofonolojia ya lugha ya Kidawida kwa kuilinganisha na Kiswahili sanifu. Kama lugha yoyote ile ya Kibantu, Kidawida pia inapaswa kushughulikiwa kiulinganishi na Kiswahili sanifu kwani huenda tukapata mambo mapya ambayo hapo awali hatukuyajua.

## 1.3 MALENGO YA UTAFITI

1. Katika utafiti wetu tunanuia kuibuka na idadi kamili ya fonimu za lugha ya Kidawida na sarufi yake.

2. Pia tunatarajia kuonyesha mabadiliko ya kifonolojia katika lugha ya Kidawida.

3. Aidha tunaazimia kuonyesha upeo wa mabadiliko ya Kifonolojia yanayotokea katika Kiswahili sanifu.
4. Mwisho tunanuia kufananisha na kutofautisha mofofonolojia ya Kiswahili na Kidawida kwa kutumia vigezo vifuatavyo:-
   (a) Mfumo wa fonimu zao.
   (b) Mabadiliko ya kifonolojia
   (c) Motisha ya mabadiliko hayo.
   (d) Upeo wa mabadiliko hayo.

## 1.4 UMUHIMU WA SOMO HILI

1. Utafiti wetu una umuhimu mkubwa kwa ambavyo unahusu mtalaa wa ulinganishi wa lugha za Kibantu. Kwa hivyo utafiti huu mwishowe utakuwa wa mchango usio haba katika somo la Isimu – linganishi na Isimu ya lugha za Kibantu.
2. Pili, utafiti huu ndio wa kwanza kufanywa kwenye kiwango cha kifonolojia kuhusiana na lugha ya Kidawida na Kiswahili. Utakuwa umefungua mlango mpya wa utafiti katika lugha hii ambayo pia ni ya Kibantu.
3. Hali kadhalika utafiti huu utaishia katika kuchangia zaidi utafiti wa Kiswahili sanifu kadiri tunavyoendelea kuilinganisha na lugha zingine za Kibantu.

## 1.5 MAPITIO YA VITABU

Mengi yameandikwa kuhusu mtalaa wa fonolojia kwa ujumla na fonolojia ya Kiswahili, Hata hivyo sio mengi yameandikwa kuhusiana na fonolojia ya Kidawida. Robert Harms (1968) katika Introduction to Phonological Theory anatupatia dhana muhimu na za kimsingi za kifonolojia hasa zile zinazotumika katika fonolojia zalishi. Harms anatukaribisha kwenye ulimwengu wa fonolojia zalishi kwa kutueleza malengo yake. Lengo la kwanza ni kuzieleza kwa ukamilifu masuala ya kjumla ya kifonolojia ya lugha. Lengo la pili ni kutambua vipashio vyote vya kifonetiki katika lugha. Kwa ujumla Harms ametusaidia kwa msingi mzuri wa kuelewa dhana ya fonolojia zalishi pamoja na kutodokezea aina mbalimbali za sifa bainishi tutakazohitaji katika utafiti wetu.

Geoffrey Horrocks (1987) katika Generative Grammar anatupatia ufahamu zaidi wa fonolojia zalishi kwa kutueleza na kutufafanulia dhana za umilisi na utendaji wa msemaji wa lugha. Vilevile Horrocks anabainisha uhususiano uliopo kati ya dhana hizi mbili akisema kwamba utendaji unatengemea umilisi. Hii ina maana kuwa msemaji wa lugha anapoongea huwa anazungumza kuambatana na ujuzi wake wa lugha hiyo iliyo kwenye bongo lake.Dhana hizi ziliasisiwa mwanzo na mwanaisimu aitwaye Noam Chomsky (1965) katika Aspects of the theory of syntax. Chomsky anasema kwamba sarufi ya lugha hunuia kutoa maelezo ya ujuzi wa mnenaji ulio bongoni mwake. Anaongeza kusema kuwa ni vizuri zaidi kwa watafiti wa lugha kujikita katika utendaji badala ya umilisi ili kuweza kuelewa kwa nini wanazungumza vile. Horrocks pia anamnukuu Popper ambaye anasema kuwa utafiti wa aina hii ni wa kisayansi mbao nadharia zake zinakusudiwa kukosolewa sio kuthibitishwa.

Sanford A. Schane (1973) katika Linguistic change and Generative Phonology hususan sura ya saba anashughulikia sheria asilia za kifonolojia. Kwenye mjadala wake alifafanua maana ya sheria asilia, pamoja na kuzianisha katika makundi matatu makuu. Makundi hayo ni pamoja na kanuni za usilimisho, kanuni za muundo mwafaka wa silabi, na kanuni za kutofautiana kisifa kadiri iwezekanavyo. Sheria asilia ndizo zile sheria za kifonetiki ambazo kwa mujibu wa Schane, hupatikana katika takriban lugha zote za ulimwengu. Sheria hizi ndizo zinazotumika kuonyesha ile mifanyiko ya kifonolojia inayotokea katika lugha.

Larry M. Hyman (1975) katika Phonology Theory and Analysis ameshugulikia kwa mapana na marefu mtalaa wa fonolojia kwa ujumla. Zaidi amejikita katika fonolojia zalishi na kujadili kwa kina dhana na mifanyiko ya kifonolojia na sheria zake pamoja na kueleza uhusiano uliopo baina ya fonetiki na fonolojia. Hali kadhalika Hyman ameshughulikia sifa bainifu za fonimu ambazo ni muhimu katika uchanganuzi wowote ule wa kifonolojia. Hyman pia ameshughulikia mjadala wa uasilia katika fonolojia ambao unahusu zile kanuni za

kifonetiki za Schane. Pamoja na hayo Hyman ameshughulikia mifanyiko anuwai ya kifonolojia ambayo ni muhimu kwa utafiti huu.

J.D O' Connor (1971) katika Phonetics anatupatia msingi wa kifonetiki kwa kushughulikia mambo kama vile ala za matamshi pamoja na uainishaji wa fonimu mbalimbali.

Naye Roger Lass (1984 ) katika Phonology pia ameshughulikia mtalaa wa fonolojia kwa undani kwa kugusia mambo kama vile mifumo ya kifonolojia, mifanyiko ya kifonolojia,ala za matamshi na sifa bainishi miongoni mwa mengine mengi. Kazi hii pia ina umuhimu kwa utafiti wetu wa kifonolojia.

Aidha Edgar C. Polome (1967) katika Swahili language Handbook ameshughulikia lugha ya Kiswahili katika viwango vya fonolojia, mofolojia na sintaksia. Polome ametusaidia sana kwa mambo yanayohusu fonimu za Kiswahili sanifu na ngeli – nomino zake.

Pia Carl Meinhof (1973) katika Introduction to the Phonology of Bantu languages ameshughulikia fonolojia ya lugha mbalimbali za Kibantu barani Afrika. Zaidi ya hayo Meinhof ametusaidia na mfumo wa fonimu za Bantu – mzazi ambayo tuliihitaji sana kwenye utafiti wetu.

Joan B. Hooper (1976) katika An Introduction to Natural Generative Phonology anatupatia orodha ya nadharia za sarufi zalishi ambazo ndio msingi wa utafiti wetu

Richard S. Mgullu (1999) katika Mtalaa wa Isimu ameshughulikia Kiswahili sanifu kwenye viwango vya fonetiki, fonolojia na mofolojia. Kazi hii pia ni ya msaada kwetu kwa sababu inatupatia mwongozo wa fonolojia ya Kiswahili sanifu.

Naye Malcolm Guthrie (1948) katika The Classification of the Bantu Languages ametusaidia katika kuelewa dhana ya 'Bantu' pamoja na kutodokezea vile lugha za Kibantu zilivyotawanyika kutoka kwa Bantu – mzazi, Vilevile tumeweza kuona vile lugha za Kibantu zinavyolingana na kutofautiana kiisimu.

Bakari Mohamed (1982) katika tasnifu yake, "The Morphophonology of the Kenyan Kiswahili Dialects" analinganisha na kutofautisha baina ya mofofonolojia ya lahaja mbalimbali za Kiswahili .Kazi hii vilevile ni muhimu kwa utafiti wetu ambao pia ni wa mofofonolojia.

Naye Peter M. Maundu (1980) Katika tasnifu yake, "Sound change and The reconstructon of Kikamba" anajaribu kuonyesha vile Kikamba kilivyodondosha sauti za konsonanti katika mengi ya maneno yake.

Kithaka wa Mberia (1981) katika tasnifu yake, "The Consonants of Kitharaka" analinganisha mofofonolojia ya Kitharaka na lugha zingine za Kibantu katika eneo la kati mwa Kenya zikiwemo Kimeru, Kiembu, Kikikuyu, Kikamba na Kimbeere.

Margaret W. Njuguna (1992) katika tasnifu yake, "Mofofonolojia ya Kiswahili sanifu na Kikikuyu sanifu; mathalani Kikikuyu cha Kabete :Ulinganishi" analinganisha mofofonolojia za Kiswahili sanifu na lahaja za Kikikuyu. Kazi hizi zote ni marejeleo muhimu kwa utafiti wetu kwani zinahusiana na utafiti huu kwa masuala ya kifonolojia na ulinganishi.

Vilevile tuliangalia kazi zilzofanywa kuhusiana na lugha ya Kidawida. Kwa kweli ni kazi chache sana zilizoshughulikia lugha hii hasa kwa upande wa Isimu. G. Righa (1978) kwenye makala yake "A Preliminary of some registers in Taita" anasema kuna lahaja tatu kuu za Kidawida zikiwa ni Kidawida, Kituweta na Kisaghalla. Hapa tunapenda kuchukua nafasi hii kuikosoa kauli hii. Ukweli ni kwamba Kidawida ,Kituweta na Kisaghalla ni lugha tatu tofauti zilizo

na wazungumzaji-wazaliwa wake katika eneo la Taita-Taveta.Kila moja ya lugha hizi zina lahaja zake mbalimbali kulingana na maeneo.Kwa mfano lugha ya Kidawida ina lahaja zake anuwai kama vile Kimbololo, Kimghange, Kimwanda na kadhalika.Pamoja na hayo Righa ameonyesha sifa mbalimbali za kiisimu katika lugha ya Kidawida hasa kwa upande wa mofolojia ,kama vile ngeli nomino, maumbo ya nomino, vitenzi, viambishi vya viwakilishi na muundo wa sentensi.

George C. Mkangi (1975) kwenye makala yake, "The Wataita: From community to individuals – An Introductory observation" anaainisha lugha ya Kidawida kama mojawapo ya lugha za Kibantu katika eneo la Mashariki mwa Kenya. Mkangi pia anaonyesha kukaribiana kwa lugha ya Kidawida na lugha zingine za Kibantu hasa Kiswahili, Kimijikenda na Kipokomo. Hata hivyo tunamkosoa Mkangi anaposema kuwa Kidawida kina lahaja mbili kuu ambazo ni Kidawida na Kisaghalla. Kama tulivyosema awali hizi si lahaja bali ni lugha kamili zilizo tofauti.

James Mwakio (1973) kwenye makala yake "Lines of inquiries into the origin and culture of the Wataita" anaongeza kwa kusema kuwa Kikasighau ni lahaja nyingine ndogo mbali na zile lahaja zilzotajwa na Righa na Mkangi.Hata yeye alikosea lakini tunakubaliana naye anaposema kuwa Kikasighau ni lahaja ya Kidawida.

## 1.6 UPEO NA MPAKA

1. Utafit wetu ni wa kiwakati, lakini mara kwa mara inapobidi tutarejelea masuala ya kimapisi.

2. Tutashughulikia fonolojia-vipande pekee.

3. Utafiti huu utachunguza mabadiliko ya kifonolojia yanayohusu konsonanti na irabu.
4. Tutarejelea lahaja za Kiswahili sanifu kwa upande wa Kiswahili, na Kimbololo kwa upande wa Kidawida.

## 1.7 MSINGI WA NADHARIA.

Utafiti wetu umejikita katika nadharia ya sarufi zalishi iliyoasisiwa na Joan B. Hooper (1976). Kabla ya nadharia hii kuasisiwa, hapo awali kulikuwepo na nadharia kadha za kiisimu, zikiwemo nadharia ya sarufi mapokeo, sarufi miundo na ya ugeuzaji-maumbo.Nadharia hizi za awali zilionekana kuwa na dosari hapa na pale ambazo zilipelekea kuibuka kwa nadharia ya sarufi zalishi.

Nadharia ya sarufi zalishi geuza-maumbo, kama inavyoitwa wakati mwingine huhusu viwango vya fonolojia na mofolojia ingawa hata sintaksia na semantiki huhusishwa.Vilevile nadharia hii huhusu maumbo ya ndani na ya nje. Kuna uhusiano wa kimsingi kati ya muundo wa ndani na muundo wa nje ambao huweza kuonyeshwa kwa kutumia sheria za kifonolojia, sheria hizi hurejelea yale mageuzi yanayotokea katika maumbo ya sauti au maneno husika kwenye muundo wa ndani ili kuyapa maumbo mapya kwenye muundo wa nje. Kwa kuwa nadharia hii ni ya Kisayansi, uhusiano uliopo baina ya muundo wa ndani na muundo wa nje unaweza kuthibitishwa kwa kutumia data iliyokusanywa kutoka kwa utendaji wa wanenaji wa lugha.

Nadharia ya fonolojia zalishi asilia, kwa mintarafu ya Joan B. Hooper (1976) inabeba aina nne za kanuni, zikiwemo kanuni za kifonetiki, kanuni za mofofonolojia, kanuni za 'Via', na kanuni za 'Sandhi'. Kanuni za kifonetiki inahusu zile kanuni bia za kifonolojia peke yake. Kanuni hizi hufanya kazi katika mipaka ya silabi na mwisho wa neno peke yake. Kanuni hizi ni bia kwa sababu hupatikana katika lugha nyingi za ulimwengu kutokana na ile hali kwamba huwa zinasababishwa kwa misingi ya ala za matamshi (fonetiki) ambayo hufanana kote

ulimwenguni. Hata hivyo wakati mwingine kanuni hizi huweza kukumbwa na vikwazo, hivyo basi kuzuia kutekelezwa kwa kanuni hizo. Vikwazo hivyo huweza kuwa vya kisemantiki, kisintaksi au kijamii.

Kanuni za kimofofonolojia huhusisha kanuni za kifonolojia katika mazingira ya kimofolojia au ya kisintaksi katika maneno kama vile nomino, vitenzi, wingi na njeo. Kanuni hizi, tofauti na za kifonetiki sio bia bali hutofautiana katika lugha mbalimbali. Hii ni kwa sababu kanuni za kimofofonolojia huhusu zaidi mipaka ya mofimu, ngeli nomino na maneno ya lugha maalumu: Kwa hivyo haitarajiwi kwamba kanuni hizi zitatokea kila mara katika lugha zote za ulimwengu.

Nadharia ya fonolojia zalishi asilia iliasisiwa na Joan B. Hooper (1973) katika tasnifu yake, "Introduction to Natural Generative Phonology" ambayo ilichapishwa mnamo mwaka wa 1976.

## 1.8 NADHARIA TETE

1. Fonimu nyingi zinazopatikana katika Kiswahili na Kidawida zinafanana, na tofauti iliyopo kati yao ni finyu.
2. Fonimu za Kidawida zimesongea na kuwa mbali zaidi na zile za Bantu-mzazi kuliko fonimu za Kiswahili.
3. Kuna tofauti za motisha na upeo wa mabadiliko ya kifonolojia baina ya Kiswahili na Kidawida.

## 1.9 METHODOLOJIA

1. Tutadurusu kazi zilizoko maktabani zinazohusiana na utafiti huu.
2. Pili tutawahoji wasemaji wa Kidawida ili kukusanya data tutakayoitumia katika uchanganuzi wetu.
3. Mwisho tutatumia ujuzi wetu wa lugha zote mbili.

## SURA YA PILI

## 2.0 UTANGULIZI

Katika sura hii tunanuia kutoa orodha ya fonimu zote za Kidawida. Bila ya kuzipambanua fonimu hizo, utafiti huu hauwezi kuendelea kwani fonimu hizo ndizo msingi muhimu katika kueleza mifanyiko ya kifonolojia inayotokea kwenye lugha hii. Larry Hyman (1975;2) anasema,

> "Fonolojia imefasiliwa kuwa ni mtalaa wa mfumo wa sauti, yaani, jinsi sauti hizo zilizoundwa pamoja na uamili wao katika lugha maalum,"[1] (TY)

Kwa mujibu wa Larry Hyman, ni jukumu letu katika utafiti huu kuweza kubainisha zile fonimu zinazopatikana katika lugha tunayoishughulikia kwa kuangalia jinsi zinavyotumika kwenye lugha hiyo.

Aidha tunaazimia kutoa orodha ya ngeli nomino za Kidawida. Ngeli ni suala la kimofolojia ambalo pia ni muhimu kwenye utafiti huu kwa sababu tunashughulikia mofofonolojia. Mofofonolojia kwa mujibu wa Joan Hooper (1976) inahusisha viwango viwili vya kiisimu katika mtalaa wa lugha, vikiwemo kiwango cha fonolojia kwa upande mmoja, na kiwango cha mofolojia kwa upande mwingine. Kwa ambavyo msingi wa nadharia ya utafiti wetu ni fonolojia zalishi asilia ambayo Joan Hooper (1976) pia imeiita nadharia ya mofofonolojia, hatuna budi basi kuangalia masuala kadha ya kimofolojia ikiwa ni pamoja na ngeli nomino za Kidawida.

## 2.1 DHANA YA FONIMU NA JOZI MLINGANUO - FINYU

Kazi chache zilizoshughulikia simu ya lugha ya kidawida zimejaribu tu kutoa orodha ya ngeli nomino za lugha hii kama vile G. Righa (1978) ingawa haikukamilika. Kutokana na ufahamu wetu hadi hivi sasa hakuna kazi yo yote ya kifonolojia iliyoratibu jumla ya fonimu za lugha ya Kidawida. Utafiti huu unanuia kuziba pengo hilo kwa kutoa orodha ya fonimu za lugha ya Kidawida.Tutafanya kazi hii kwa kutumia mbinu ya jozi mlinganuo finyu. Kama asemavyo Larry Hyman(1975:3),

> "Mtalaa wa kifonetiki wa lugha yo yote ile, hivyo basi hutoa orodha na ufafanuzi wa vipashio vyote vya kifonetiki vinavyopatikana kwenye lugha husika."[3](TY)

Kwa mintarafu ya Larry Hyman mtalaa wa kifonolojia kuhusu utoaji wa orodha ya fonimu za lugha fulani. Fonetiki na fonolojia ni viwango viwili vya kiisimu ambavyo hutegemeana sana. Richard S. Mgullu (1999:48) anathibitisha kauli hii kwa kusema kuwa, matawi haya mawili hutegemeana na kukamilishana kwa sababu zote mbili huchunguza kitu kilekile kimoja, yaani sauti za lugha[4]. Utafiti wo wote wa kifonolojia hauwezi kutekelezwa bila kurejelea fonetiki kwa sababu fonetiki ndio msingi wa fonolojia. Hivyo basi utafiti wetu hautaepuka jukumu hilo muhimu kama tutakavyofanya katika sura hii, sehemu ya kwanza.

Kabla ya kupambanua fonimu za lugha ya Kidawida ni vyema kuelewa dhana hii ya fonimu kama tutakavyoangalia kwenye utafiti huu. Larry Hyman (1975:59) anataja fonimu kuwa ni kipashio kidogo kabisa cha sauti kinachoweza kuleta tofauti ya maana katika maneno[5]. Hyman anaendelea kwa kusema kuwa fonimu inaweza kuangaliwa kwa mitazamo mitatu tofauti zikiwa ni:-

a) fonimu kama tukio la kifonetiki
b) fonimu kama tukio la kisaikolojia
c) fonimu kama tukio la kifonolojia

Utafiti wetu utazingatia zaidi mtazamo wa tatu unaoangalia fonimu kama tukio la kifonolojia. Tunachukua mtazamo huu kwa sababu utafiti wetu unahusu zaidi fonolojia. Kwa mujibu wa Richard S. Mgullu (1999:54) mtazamo huu unaangalia fonimu kwa mwelekeo wa uamilifu wake katika mfumo mzima wa fonolojia. Mgullu anasema kuwa mtazamo huu unadai kuwa fonimu ya lugha fulani huwa ni fonimu kutokana na uamilifu wake. Uamilifu unaozungumziwa hapa ni ule wa kubainisha maana za maneno mawili au zaidi.[6]

> "Kama asemavyo Trubetzkoy (1939) katika Richard S. Mgullu (1999:55),
>
> "Fonimu ni kipashio kidogo kabisa (katika lugha) kilicho na uamilifu wa kutofautisha maana katika maneno."[7]

Fonimu za lugha mbalimbali hutofautiana. Kifonetiki lugha mbili au zaidi tofauti huweza kuwa na foni zilizofanana,lakini kifonolojia lugha hizo zikatofautiana kwa jinsi ambavyo foni hizo zinapangwa, au uamilifu wa foni hizo katika lugha mbili au zaidi ukawa ni tofauti. Katika kiwango cha kifonolojia hizo foni huitwa fonimu ambazo ni tofauti katika kila lugha. Hivi ni kusema kwamba lugha huwa ni tofauti na lugha nyingine kwa sababu ya fonimu zake. Ndiposa tuna lugha nyingi ulimwenguni ambazo kila moja ni ya kipekee na tofauti na lugha zingine. Kwa sababu hiyo basi hatuna budi kutoa orodha ya fonimu za Kidawida kwa kuangalia jinsi ambavyo fonimu zimepangwa katika mfumo wa kifonolojia wa lugha hiyo.

Richard S. Mgullu (1999:62) amemtaja Fischer (1975) akitoa fasili ya mlinganuo finyu kuwa ni tofauti ndogo kabisa ya kifonolojia iliyopo baina ya maneno fulani[8]. Aghalabu maneno hayo huwa yana,

(a) Idadi sawa ya fonimu.

(b) Fonimu zinazifanana isipokuwa moja

(c) Mpangilio wa fonimu ulio sawa

Katika Kiswahili tunaweza kutoa mfano wa maneno kama vile,

1. Paa – mnyama, au sehemu ya nyumba.
2. Baa – hasara.
3. Taa – chombo cha kutoa mwangaza
4. Kaa – aina ya mnyama, kaa la moto, au keti.
5. Vaa – kufunika mwili kwa nguo
6. Zaa – kupata mtoto kwa binadamu au mnyama

Mfano huo unaonyesha vile fonimu moja tu ilivyoweza kutofautisha maana ya maneno hayo yote, Tofauti za maana ya maneno hayo imesababishwa na fonimu /P/, /b/,/t/,/k/,/v/ na /z/. Kwa sababu hiyo, tunaweza kusema kwamba hizi ni fonimu za lugha ya Kiswahili.

Richard S. Mgullu (1999:63) anaendelea kwa kusema,

> "Jozi mlinganuo finyu hususan huwa na maneno mawili tu au orodha mbili za maneno ambayo tofauti zao ni finyu."[9]

Hapa Mgullu anafupatia fasili ya jozi mlinganuo finyu akisisitiza kuwa ni maneno mawili tu yanayohusika, kwa mfano 1. Paa
2. baa.

Maneno haya mawili yana idadi sawa ya fonimu, mpangalio wa fonimu zao unalingana, na fonimu zao zote zinafanana isipokuwa moja tu. Tofauti kati yao ni fonimu /p/ na /b/ ambazo zinasababisha tofauti katika maana ya maneno hayo. Kwa maelezo zaidi, Larry Hyman (1975:60) anasema,

> "Iwapo sauti mbili zilizofanana kifonetiki zinapatikana katika mazingira sawa ya kifonetiki, na ikiwa kubadilishwa kwa sauti moja na nyingine hupelekea katika tofauti ya maana, basi sauti hizo zitakuwa ni fonimu zilizo tofauti.[10] (TY)

Hivyo basi mfano wetu umetubainishia kuwa sauti [P] na [b] ni fonimu mbili tofauti za Kiswahili sanifu, yaani /p/ na /b/.

Richard S Mgullu (1999:63) anatudokezea kuwa katika mbinu ya jozi mlinganuo finyu maneno husika lazima yawe ni ya lugha moja tu, na maana za maneno hayo pia lazima yawe tofauti.[11] Kwa kutumia mbinu hii tunaweza kuibuka na jumla ya fonimu za lugha tunayoishughulikia[12] kama anavyodai Roger Lass (1984:18).

## 2.2 FONIMU ZA KIDAWIDA – IRABU

Kiisimu sauti hupangwa katika makundi mawili makuu yaani (a) konsonanti (b) irabu.

Irabu ni sauti ambayo wakati wa kutamkwa mkondo wa hewa huwa hauzuiliwi. Hii ni sauti ambayo aghalabu hubeba kiini cha silabi katika neno lo lote lile. Kwa kutumia jozi mlinganuo finyu tunapata irabu saba tofauti kwenye lugha ya Kidawida. Kwa mfano

| | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 1 | /aɤa/ | ———— | [aɤa] | jenga |
| | /ɔɤa/ | ———— | [ɔɤa] | oga |

Maneno hayo mawili yanabainisha fonimu mbili za irabu /a/ na /ɔ/ katika kidawida. Aidha tuna jozi lingine la maneno yafuatayo,

| | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 2 | /ɔhɔ/ | ———— | [ɔhɔ] | wewe |
| | /ahɔ/ | ———— | [ahɔ] | hapo |

Mifano hii nayo inabainisha fonimu / ɔ / katika lugha ya Kidawida. Kisha tuna maneno kama vile,

| | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 3 | /ŋgera/ | ———— | [ŋgera] | labda |
| | /ŋgira/ | ———— | [ŋgira] | ingiza |

| | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 4 | /ela/ | ———— | [ela] | takata |
| | /ɔla/ | ———— | [ɔla] | angalia |

Mifano hiyo inatupatia fonimu ya irabu /e/. Pia tunapata fonimu /i/ hata kwenye mfano ufuatao.

| | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 5 | /tʃia/ | ———— | [tʃia] | njia |
| | /tʃia/ | ———— | [tʃia] | jaa pomoni |

Aidha tunapata fonimu /u/ kwa mfano,

| | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 6 | /mbua/ | ———— | [mbua] | pua |
| | /mbaa/ | ———— | [mbaa] | kubwa |
| 7 | /kau/ | ———— | [kau] | kiu |
| | /kai/ | ———— | [kai] | ghala |

Pia tuna fonimu / ɛ / katika Kidawida, kwa mfano,

| | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 8 | / ɛ la/ | ———— | [ɛ la] | lakini |
| | /ɔla/ | ———— | [ɔla] | angalia |

Kwa hivyo jumla ya fonimu za irabu za Kidawida ni saba zikiwa ni pamoja na /i/, /e/, /ɛ/, /a/, /ɔ/, /o/ na /u/. Yaani,

9 i, u,

e, o,

ɛ, ɔ,

a,

Matokeo haya yanathibitisha kauli iliyotolewa na Malcolm Guthrie (1948:45). Kwamba lugha nyingi za Kibantu huwa na idadi ya fonimu za irabu zipatazo ama tano au saba[13]. Kidawida ni moja ya zile zenye irabu saba.

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | **Maana** |
| 4 | /ela/ ———— | [ela] | takata |
| | /ɔla/ ———— | [ɔla] | angalia |

Mifano hiyo inatupatia fonimu ya irabu /e/. Pia tunapata fonimu /i/ hata kwenye mfano ufuatao.

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | **Maana** |
| 5 | /tʃia/ ———— | [tʃia] | njia |
| | /tʃia/ ———— | [tʃia] | jaa pomoni |

Aidha tunapata fonimu /u/ kwa mfano,

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | **Maana** |
| 6 | /mbua/ ———— | [mbua] | pua |
| | /mbaa/ ———— | [mbaa] | kubwa |
| 7 | /kau/ ———— | [kau] | kiu |
| | /kai/ ———— | [kai] | ghala |

Pia tuna fonimu / ɛ / katika Kidawida, kwa mfano,

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | **Maana** |
| 8 | / ɛ la/ ———— | [ɛ la] | lakini |
| | /ɔla/ ———— | [ɔla] | angalia |

Kwa hivyo jumla ya fonimu za irabu za Kidawida ni saba zikiwa ni pamoja na /i/, /e/, /ɛ/, /a/, /ɔ/, /o/ na /u/. Yaani,

9 i, u,

e, o,

ɛ, ɔ,

a,

Matokeo haya yanathibitisha kauli iliyotolewa na Malcolm Guthrie (1948:45). Kwamba lugha nyingi za Kibantu huwa na idadi ya fonimu za irabu zipatazo ama tano au saba[13]. Kidawida ni moja ya zile zenye irabu saba.

## 2.3 FONIMU ZA KIDAWIDA – KONSONANTI

Konsonanti ni sauti ambayo kutamkwa kwake huhusu kuzuiliwa kwa mkondo wa hewa. Mkondo wa hewa unaweza kuzuiliwa ama kabisa au kwa kiasi kutegemea ni sauti gani inatamkwa.

Kidawida kina konsonanti mbalimbali ambazo tutazibainisha kutokana na fonimu za maneno yake. Tutaanza na fonimu za konsonanti za mtuo ambazo hutamkwa kwa mkondo wa hewa kubanwa kabisa. Kwa mfano,

| | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 10 | /kia/ | ———— | [kia] | okoka |
| | /bia/ | ———— | [bia] | kuwa kali au mkali |

Pia

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 11 | /bɔra/ | ———— | [bɔra] | imba |
| | /kɔra/ | ———— | [kɔra] | choma |

Mifano ya jozi hizo zinabainisha fonimu za konsonanti za mtuo /b/ na /k/ katika kidawida. Aidha tuna maneno kama vile,

| | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 12 | /puruka/ | ———— | [puruka] | kuruka kama ndege |
| | /turuka/ | ———— | [turuka] | gutuka |

Mifano hiyo inatupatia fonimu /p/ na /t/ zilizoko katika lugha hii ingawa /p/ inaonekana kuwa ni nadra sana. Pamoja na hayo tuna jozi la maneno kama vile

| | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 13 | /sia/ | ———— | [sia] | isha |
| | /dia/ | ———— | [dia] | mwaga |

Pia,

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 14 | /dɛka/ | ———— | [dɛka] | pika |
| | /lɛka/ | ———— | [lɛka] | wacha |

Fonimu ya konsonanti ya mtuo inayobainika kwenye mifano hiyo ni /d/ katika Kidawida.

Pia Kidawida kina fonimu ya konsonanti /g/ inayojitokeza kama ifuatavyo,

| | | | | **Maana** |
|---|---|---|---|---|
| 15 | /guʃa/ | ——— | [guʃa] | angusha |
| | /luʃa/ | ——— | [luʃa] | chafua |

Pia

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 16 | /igi/ | ——— | [igi] | yai |
| | /iβi/ | ——— | [iβi] | mbili |

Kisha tuna fonimu /ɓ/ ambayo ni kipasuo cha ndani[14], kwa mujibu wa TUKI (1990). Kwa mifano tuna majozi ya maneno kama vile,

| | | | | **Maana** |
|---|---|---|---|---|
| 17 | /bɔa/ | ——— | [bɔa] | ogopa |
| | / ɓɔa/ | ——— | [ɓɔa] | pona |

tena

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 18 | /bula/ | ——— | [bula] | piga |
| | /ɓula/ | ——— | [ɓula] | funika |

Pamoja na hayo Kidawida kina kosonanti ya mtuo /j/. Kwa mfano tuna maneno kama vile,

| | | | | **Maana** |
|---|---|---|---|---|
| 19 | /jɔka/ | ——— | [jɔka] | panda/kwea |
| | /βɔka/ | ——— | [βɔka] | anza |

Pia,

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 20 | /musiɣɛ/ | ——— | [musiɣ ɛ] | mwache |
| | /mujiɣɛ/ | ——— | [mujiɣɛ] | msichana mdogo |

Kwa ujumla Kidawida kina fonimu za kosonanti za mtuo zipatazo nane, zikiwemo /p/, /t/, /ɓ/, /d/, /j/ na /g/. Fonimu /p/, /t/, /k/ ni konsonanti za mtuo zisizo na sifa ya ughuna ilhali fonimu / ɓ/ /d/, /b/, /j/ na /g/ zina sifa ya ughuna.

Kidawida vilevile kina konsonanti anuwai za vikwamizwa. Vikwamizwa ni sauti konsonanti ambazo hutamkwa wakati ala za kutamkia zinakaribiana kiasi

kwamba mkondo wa hewa unasababisha mgusano unaosikika,[15] kama isemavyo Kamusi ya TUKI (1990). Hizi ni sauti ambazo zinapotamkwa mkondo wa hewa hauzuiliwi kabisa ingawa ala za kutamka zinakaribiana na kusababisha mkwaruzo fulani.

Katika Kidawida tuna maneno kama vile,

| | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 21 | /gwa/ | ——— | [gwa] | anguka |
| | /fwa/ | ——— | [fwa] | kufa |

Pia,

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 22 | /fada/ | ——— | [fada] | finya |
| | /βada/ | ——— | [βada] | vipi |

Mifano hiyo inaonyesha kwa kuna fonimu ya kikwamizwa /j/ katika Kidawida. Aidha tuna maneno haya

| | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 23 | /vina/ | ——— | [vina] | cheza (ngoma) |
| | /kina/ | ——— | [kina] | shimo |

Vile vile,

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 24 | /βuria/ | ——— | [βuria] | rudia |
| | /vuria/ | ——— | [vuria] | vuria |

Hapo tunapata fonimu za vikwamizwa [β] na [v] kama tunavyoona katika jozi lifuatalo pia,

| | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 25 | /vaa/ | ——— | [vaa] | zaa |
| | /βaa/ | ——— | [βaa] | panda |

Kisha tuna jozi hili la maneno,

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 26 | /mbiʃi/ | ——— | [mbiʃi] | mpya |
| | /mbisi/ | ——— | [mbisi] | fisi |

Pia,

| | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 27 | /sia/ | ——— | [sia] | isha |
| | /dia/ | ——— | [dia] | mwaga |

Majozi haya ya maneno yanabainisha kuwepo kwa fonimu za vikwamizwa /s/ na /ʃ/ katika Kidawida.

Aidha tuna fonimu /z/ kama inavyojitokeza hapa.

| | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 28 | /masa/ | ——— | [masa] | mapacha |
| | /maza/ | ——— | [maza] | mambo |

Pia,

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 29 | /tʃuɣwa/ | ——— | [tʃuɣwa] | chanjwa |
| | /zuɣwa/ | ——— | [zuɣwa] | hisi njaa |

Mifano hiyo vilevile imebaanisha kuwepo kwa fonimu ya kikwamizwa /ɣ/ katika Kidawida. Fonimu hii pia tunaipata kwenye mifano ifuatayo,

| | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 30 | /tʃadu/ | ——— | [tʃadu] | kiatu |
| | /tʃaɣu/ | ——— | [tʃaɣu] | kazi |

Pia,

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 31 | /bɔra/ | ——— | [bɔra] | imba |
| | /ɣɔra/ | ——— | [ɣɔra] | sema |

Hali kadhalika tuna fonimu ya kukwamizwa /h/ katika Kidawida. Kwa mfano,

| | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 32 | /ʃɔa/ | ——— | [ʃɔa] | okota |
| | /hɔa/ | ——— | [hɔa] | pona au poa |

Pia,

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 33 | /aha/ | ——— | [aha] | hapa |
| | /aɣa/ | ——— | [aɣa] | jenga |

Hivyo basi tunapata jumla ya fonimu za vikwamizwa katika Kidawida ni nane zikiwa ni /β/, /f/, /v/, /s/, /z/, /ʃ/, /ɣ/ na /h/.

Kidawida pia kina fonimu za nasali ikiwa ni pamoja na zile konsonanti zilizonasalishwa. Tukianza na nasali, hizi ni sauti ambazo zitamkwapo mkondo

wa hewa hupitia kinywani na puani. Sauti zisizo za nasali hutamkwa kwa mkondo wa hewa kupitia kinywani peke yake. Mifano ya maneno inayotupatia fonimu za nasali katika lugha hii ni kama vile,

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | **Maana** |
| 34 | /mɔdɔ/ | ——— | [mɔdɔ] | moto |
| | /ɲɔdɔ/ | ——— | [ɲɔdɔ] | titi |

Pia,

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 35 | /duka/ | ——— | [duka] | beba |
| | /muka/ | ——— | [muka] | kawia |

na,

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 36 | /lafua/ | ——— | [lafua] | pupa |
| | /ɲafua/ | ——— | [ɲafua] | nyepesi |

Jozi hizo zinatupatia fonimu /m/ na /ɲ/ kama zinavyojitokeza katika Kidawida.

Kisha tuna maneno kama vile,

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | **Maana** |
| 37 | /nɛka/ | ——— | [nɛka] | pa |
| | /dɛka/ | ——— | [dɛka] | pika |

Pia,

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 38 | /nuɤa/ | ——— | [nuɤa] | fuata |
| | /ruɤa/ | ——— | [ruɤa] | funga |

Ni dhahiri kwamba Kidawida kina fonimu ya nasali /n/. Aidha tuna fonimu ya nasali /ŋ/, kwa mfano,

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | **Maana** |
| 39 | /mana/ | ——— | [maɲa] | fahamu |
| | /ŋana/ | ——— | [ŋana] | fulani |

Pia,

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 40 | /tana/ | ——— | [tana] | achana |
| | /ŋaɲa/ | ——— | [ŋaɲa] | kiasi fulani |

Kwa hivyo jumla ya konsonati za nasali za Kidawida ni nne, yaani /m/, /n/, /ɲ/ na /ŋ/

Mbali na fonimu hizo za nasali, pia kuna fonimu ambazo ni konsonati zilizonasalishwa awali hivi kwamba zinatamkwa kama sauti moja. Mohamed Bakari (1982) katika tasnifu yake ameonyesha konsonanti mbalimbali zilizonasalishwa awali

katika lahaja anuwai za Kiswahili kama vile Chi-chifundi, Kivumba, Kimvita, Chijomvu, Kiamu, Kitikuu na Kisiyu.

Kifonetiki, konsonanti zlizonasalishwa awali hutamkwa kwa mkondo wa hewa kupitia kinywani na puani. Kidawida kina fonimu aina hizi kama vile,

| | | | | **Maana** |
|---|---|---|---|---|
| 41 | /ɣamba/ | ——— | [ɣamba] | sema |
| | /ɣada/ | ——— | [ɣada] | kuwa mvivu |
| 42 | /lɔmba/ | ——— | [lɔmba] | omba |
| | /lɔɣa/ | ——— | [lɔɣa] | loga |
| 43 | /lumbɔ/ | ——— | [lumbɔ] | wimbo |
| | /luŋgo/ | ——— | [luŋgo] | uteo |
| na | | | | |
| 44 | /mumbi/ | ——— | [mumbi] | mwili |
| | /muŋgi/ | ——— | [muŋgi] | mwingi |

Mifano hiyo inaonyesha dhahiri Kidawida kina fonimu ya konsonati iliyonasalishwa awali /mb/. Aidha tuna fonimu ya /nd/ kwenye lugha hii tunayoipata katika maneno kama vile.

| | | | | **Maana** |
|---|---|---|---|---|
| 45 | /mundu/ | ——— | [mundu] | mtu |
| | /mufu/ | ——— | [mufu] | unga |
| 46 | /kunda/ | ——— | [kunda] | penda |
| | /kuβa/ | ——— | [kuβa] | kupanda mbegu |
| 47 | /ɣɛnda/ | ——— | [ɣɛnda] | nenda |
| | /ɣɛʃa/ | ——— | [ɣɛʃa] | dhani / fikiri |

na,

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 48 | /ŋganda/ | ——— | [ŋganda] | udongo |
| | /ŋgatʃa/ | ——— | [ŋgatʃa] | ndama |

Vilevile tuna fonimu /nj/ kama tunavyoona kwenye mifano ifuatayo,

| | | | | **Maana** |
|---|---|---|---|---|
| 49 | /ɣɛɲja/ | ——— | [ɣɛɲja] | peleka |
| | /ɣɛnda/ | ——— | [ɣɛnda] | nenda |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 50 | /iɲja/ ——— | [iɲja] | ondoa |
| | /inda/ | [inda] | chawa |

na

| | | | |
|---|---|---|---|
| 51 | /kɔɲja/ ——— | [kɔɲja] | onja |
| | /komba/ ——— | [komba] | lamba |

Hali kadhalika tuna fonimu /ng/ katika lugha hii, kwa mfano.

| | | | **Maana** |
|---|---|---|---|
| 52 | /iraŋgi/ ——— | [iraŋgi] | uhai / uzima |
| | /irasi/ ——— | [irasi] | tambara |
| 53 | /maŋga/ ——— | [maŋga] | muhogo |
| | /maza/ ——— | [maza] | mambo |
| 54 | /ndeŋgo/ ——— | [ndeŋgo] | hatari |
| | /ndembo/ ——— | [ndembo] | mgomba |

Kutokana na mifano hiyo tunapata kwamba Kidawida kina fonimu zilizonasalishwa awali zipatazo nne ambazo ni /mb/, /nd/, /nj/ na /ŋg/. Kama asemavyo Kithaka wa Mberia (1981) katika tasnifu yake ya uzamili fonimu hizi aghalabu ni konsonanti za mtuo zenye na hazipatikani mghuno mwanzoni mwa neno[16]. Mara nyingi fonimu hizi huwa katika mashina ya maneno kama tulivyoshuhudia kwenye mifano yetu. Fonimu aina hizi hupatikana kwa uchache sana.

Aina nyingine ya konsonanti inayopatikana katika lugha hii ni ile ya vizuiwa- kwamizwa. Kwa mujibu wa Richard S. Mguku (1999:29) hizi ni sauti za konsonati ambazo zinapotamkwa hewa husukumwa nje kwa nguvu, huzuiwa halafu nafasi ndogo huachwa ili ipite ikiwa na mkwaruzo. Hizi ni sauti ambazo wakati wa kutamkwa mkondo wa hewa huzuiliwa kwanza kisha kuachiliwa kidogo hivi kwamba mkwaruzo unasababishwa katika hali hiyo. Kidawida kina aina moja tu ya sauti hii ambayo ni /tʃ/ kama tunanvyoona hapa,

| | | | **Maana** |
|---|---|---|---|
| 55 | /bia/ ——— | [bia] | kuwa kali / mkali |
| | /tʃia/ ——— | [tʃia] | njia |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | / tʃuɣu/ | ——— | [tʃuɣu] | mbaazi |
| | /kuɣu/ | ——— | [kuɣu] | mguu |

na,

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 56 | /tʃuɣa/ | ——— | [tjuɣa] | chanja |
| | /luɣa/ | ——— | [luɣa] | kamba |

Vilevile Kidawida kina sauti za vilainisho Richard S. Mugullu (1999:29) ametofautisha aina mbali za vilainisho. Kwanza kuna vitambaza ambavyo ni vilainisho vyenye kutamka kwa hewa kusukumwa nje, kuzuiwa na kisha kuruhusiwa kupita pembeni mwa kizuizi bila mkwaruzo mkubwa sana[18]. Kitambaza kinapotamkwa hewa huzuiliwa na kisha kuachilia kupita sehemu za kando za ulimi. Zipo aina nyingi za sauti hii lakini Kidawida kina aina moja tu ambayo ni /l/ kama tuonayo kwenye mifano ifuatayo,

| | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 57 | /ruɣa/ | ——— | [ruɣa] | funga |
| | /luɣa/ | ——— | [luɣa] | kamba |
| 58 | /laɣa/ | ——— | [laɣa] | kifua |
| | /daɣa/ | ——— | [daɣa] | tupa |

Aina nyingine ya kilainisho ni ile Richard Mgullu (1999) anayoiita Kimadende. Kimadende ni kilainisho ambacho kinapotamkiwa ncha ya ulimi huwa imeugusa ufizi lakini kutokana na nguvu ya hewa inayoipita kati ya ncha hiyo na ufizi,[19] ncha ya ulimi hupigapiga kwa harakaharaka kwenye ufizi. Kidawida kina aina moja tu ya kimadende ambayo ni /r/, kwa mfano,

| | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 59 | /rɛda/ | ——— | [rɛda] | leta |
| | /dɛda/ | ——— | [dɛda] | teta |
| 60 | /βika/ | ——— | [βika] | weka |
| | /rika/ | ——— | [rika] | zika |

na,

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 61 | /raʃa/ | ——— | [raʃa] | gombeza |

| | | | |
|---|---|---|---|
| /faʃa/ | ——— | [faʃa] | kanyaga |

Kwa hivyo, jumla ya idadi ya vilainisho vya Kidawida ni viwili vikiwemo kitambaza kimoja /l/, na kimadende kimoja /r/.

## 2.4 FONIMU ZA KIDAWIDA – NUSU – IRABU

Nusu – irabu ni aina nyingine ya sauti za lugha mbali na konsonanti au irabu. Hizi ni sauti ambazo kwa msingi ya kifonetiki, zipo katikati ya konsonanti na irabu tukirejelea sifa zao. Nusu – irabu ni sauti ambazo mithili ya popo, zina baadhi ya sifa za konsonanti na irabu. Kwa mfano utamkaji wa nusu- irabu hauhusu kuzuiliwa kwa mkondo wa hewa sawa na utamkaji wa irabu. Vilevile sifa ya chemba inahusishwa na nusu – irabu kama vile sifa za korona au anteria ambazo pia hutumka kubainisha aina anuwai za konsonanti. Ndiposa Richard S. Mugullu (1999:28) akasema nusu – irabu huweza vilevile kuitwa nusu- konsonanti[20].

Lugha ya Kidawida haikosi kuwa na sauti aina hii kama tuonavyo kwenye majozi yafuatavyo,

| | | | | **Maana** |
|---|---|---|---|---|
| 62 | /duwa/ | ——— | [duwa] | tua mzigo |
| | /duka/ | ——— | [duka] | beba |
| na, | | | | |
| 63 | /wa/ | ——— | [wa] | wa |
| | /sa/ | ——— | [sa] | kama |

Mifano ya maneno hayo inabainisha kuwa ipo fonimu ya nusu-irabu /w/ katika Kidawida. Hii ni nusu-irabu ambayo hutamkwa kwa kuviringwa kwa midomo pamoja na kutamkwa kwenye kaakaa laini. Mifano mingine ni kama vile,

| | | | | **Maana** |
|---|---|---|---|---|
| 63 | /dasa/ | ——— | [dasa] | kutema mate ya baraka |
| | /daja/ | ——— | [daja] | teka |

na,

64 /βwaja/ ——— [βwaja] haya(za uso)
/βwada/ ——— [βwada] shika

Jozi hizi zinatupatia fonimu nyingine ya nusu-irabu /j/ iliyoko katika Kidawida Fonimu hii, tofauti na /w/ hutamkwa kwenye kaakaa gumu na wala, haihusu kuviringwa kwa midomo. Kwa jumla Kidawida kina nusu-irabu mbili tu, ambazo ni /w/ na /j/.

## 2.5 FONIMU ZA KIDAWIDA – HITIMISHO

Kwa kuhutimisha tunaweza kusema Kidawida kina takriban aina zote za sauti za lugha zikiwemo irabu, konsonati na nusu-irabu. Tumeshuhudia aina anuwai za fonimu hizi kama zinavyojitokeza kwenye lugha hii. Jumla ya fonimu zote za Kidawida ni thelathini na sita (36) ikiwa ni pamoja na irabu saba (7) na konsonanti ishirini na tisa (29). Jadwali lifuatalo linatupatia jumla ya fonimu zote za konsonati.

**JEDWALI LA KONSONANTI**

| Aina ya konsonanti | Midomo | Midomo + Meno | Meno | Meno + Ufuzi | Ufizi | Kaakaa gumu | Kaakaa laini | Glota | Jumlas |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mtuo | P,ɓ,b | | | | t, d | j | k, g | | 8 |
| Vikwamizwa | β | f, v | | ʃ | s, z | | ɣ | h | 8 |
| Kizuiwa – Kwamizwa | | | | | | tʃ | | | 1 |
| Nasali | m | | | | n | ɲ | ŋ | | 4 |
| Konsonanti Za mtuo Zilizonasali - wa awali | $^{m}b$ | | | | $^{n}d$ | $^{ɲ}j$ | $^{ŋ}g$ | | 4 |
| Kitambaza | | | | | l | | | | 1 |
| Kimadende | | | | | r | | | | 1 |
| Viyeyusho | w | | | | | j | | | 2 |
| Konsonanti 29 | | | | | | | | | |

## 2.6 NGELI NOMINO ZA KIDAWADA

### UTANGULIZI

TUKI (1990) wanaeleza ngeli ya nomino kuwa,
"ngeli nomino ni kundi moja la majina yaliyo na upatanisho wa kisarufi unaofanana na viambishi vya umoja na wingi vinavyofanana."

Kulingana na fasili hii, ngeli nomino ni jumla ya majina yanayofanana kwa upatanifu wa kisarufi, na viambishi vyao vya umoja na wingi. Mambo haya wawili yanahusu sintaksia kwa upande mmoja, na mofofonojia kwa upande mwingine. Kwa ambavyo utafiti wetu ni wa kimofofonojia, tutajikita tu na sehemu hiyo ya mofofonojia ambayo inahusu vile viambishi vya umoja na wingi vya majina. Hii ni kwa sababu utafiti huu una misingi yake katika nadharia ya sarufi zalishi asili ambayo pia inashughulikia baadhi ya mabadiliko yanayohusu mazingira ya kimofofonolojia kama vile ya nomino, wingi na njeo. Kutokana na hili, inatubidi basi kufahamu ngeli nomino za lugha tunayoishughulikia, ya Kidawida.

Kazi ya G. Righa (1978) imejaribu kutoa orodha ya ngeli nomino za lugha ya Kidawida. Kazi hii iliweza kuorodhesha ngeli nomino kumi pekee na tunaweza kusema kwamba kazi hiyo haikukamilisha ngeli nomino zote kama tunavyozifahamu. Hivyo basi katika utafiti wetu tutajaribu kurekebisha hali hiyo kwa kutoa orodha nzima ya ngeli nomino zinazopatikana katika Kidawida.

## 2.6 NGELI NOMINO ZA KIDAWADA

### UTANGULIZI

TUKI (1990) wanaeleza ngeli ya nomino kuwa,
"ngeli nomino ni kundi moja la majina yaliyo na upatanisho wa kisarufi unaofanana na viambishi vya umoja na wingi vinavyofanana."

Kulingana na fasili hii, ngeli nomino ni jumla ya majina yanayofanana kwa upatanifu wa kisarufi, na viambishi vyao vya umoja na wingi. Mambo haya wawili yanahusu sintaksia kwa upande mmoja, na mofofonojia kwa upande mwingine. Kwa ambavyo utafiti wetu ni wa kimofofonojia, tutajikita tu na sehemu hiyo ya mofofonojia ambayo inahusu vile viambishi vya umoja na wingi vya majina. Hii ni kwa sababu utafiti huu una misingi yake katika nadharia ya sarufi zalishi asili ambayo pia inashughulikia baadhi ya mabadiliko yanayohusu mazingira ya kimofofonolojia kama vile ya nomino, wingi na njeo. Kutokana na hili, inatubidi basi kufahamu ngeli nomino za lugha tunayoishughulikia, ya Kidawida.

Kazi ya G. Righa (1978) imejaribu kutoa orodha ya ngeli nomino za lugha ya Kidawida. Kazi hii iliweza kuorodhesha ngeli nomino kumi pekee na tunaweza kusema kwamba kazi hiyo haikukamilisha ngeli nomino zote kama tunavyozifahamu. Hivyo basi katika utafiti wetu tutajaribu kurekebisha hali hiyo kwa kutoa orodha nzima ya ngeli nomino zinazopatikana katika Kidawida.

## 2.7 NGELI NOMINO ZA KIDAWIDA


1. Ngeli ya Kwanza

Kiambishi cha ngeli hii ni [mu-] ambayo inaweza kujitokeza kwa sura mbalimbali kutegemea mazingira ya kimofofonolojia, yaani alomofu. Kwa mujibu wa Edgar C. Polome (1967:96), nomino zilizo katika ngeli nomino hii aghalabu ni majina ya wanadamu[22] kama vile,

| | | Maana |
|---|---|---|
| 68 | /mundu/- [mundu] => [m̩ndu] | mtu |
| | /muka/ - [muka ] => [ m̩ka ] | mke |
| | /musaβi/-[musaβi] => [m̩saβi] | mchawi |
| | /muana/- [mwana] | mtoto |
| | /muai/ - [mwai] | msichana |
| | /muaɣi/ - [muaɣi] | mjenzi |
| | /maɔ/ - [maɔ ] | mama |
| | /apa/ - [apa] | baba |

Mfano hiyo inaonyesha kuwa mofu ya ngeli hii {mu-}inaweza kujitokeza kama.

69




2. Ngeli ya pili

Kiambishi cha ngeli hii ni [βa-]. Majina yaliyopo kwenye ngeli hii ni wingi wa majjina ya ngeli ya kwanza Kama vile,

| | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 70 | /βandu/ | - | [βandu] | watu. |
| | /βaka/ | - | [βaka] | wake |
| | /βasabi/ | - | [βasabi] | wachawi |
| | /βa:na/ | - | [βana] | watoto |
| | /βa:i/ | - | [βai] | wasichana |
| | /βa:ɣi/ | - | [βa:ɣi] | wajenzi |
| | /mas/ | - | [mas] | mama |
| | /apa/ | - | [apa] | baba |

83 /N-/ → [ m- / n- / n- / ŋ- / Ø ]

10. <u>Ngeli ya kumi</u>.

Kiambishi cha ngeli nomino hii vilevile ni {N-}. Majina yanayopatikana kwenye ngeli hii ni wingi wa ngeli ya tisa na aghalabu huwa yamefanana kimuundo na majina ya ngeli hiyo ya tisa.

| | | | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 84 | /N + βoɣɔ/ | → | [mboɣɔ] | | | nyati |
| | /N + βuri/ | → | [mburi] | | | mbuzi |
| | /N + βuba/ | → | [mbuba] | | | mashamba |
| | /N + ɣɔmbɛ/ | → | [ŋgɔmbɛ] | → | [ŋɔmbe] | ng'ombe |
| | /N+ ɣɔndi/ | → | [ŋgɔndi] | → | [ŋɔndi] | kondoo |
| | /N + ɣuku/ | → | [ŋguku] | | | kuku |
| | /N + lɛmbɔ/ | → | [ndɛmbɔ] | | | migomba |
| | /N +lɛ:/ | → | [ndɛ:] | | | baba zake |
| | /N + lɔ:/ | → | [ndɔ:] | | | mchanga |
| | /N + lazi/ | → | [ndazi] | | | nzima au nyingi |
| | /N +ɔni/ | → | [ɲɔni] | | | nyuni |
| | /N + uŋgu/ | → | [ɲuŋgu] | | | vyungu [chombo] |
| | /N + jala/ | → | [ɲjala] | | | njaa |
| | /N + jau/ | → | [ɲjau] | | | mafahali |
| | /N + kɔʃi/ | → | [kɔʃi] | | | mbwa |
| | /N + tʃɔvu/ | → | [tʃɔvu] | | | ndovu |
| | /N +ʃimba/ | → | [ʃimba] | | | simba |

Hivyo basi alomofu za mofu ya ngeli hii na sawa na alomofu za mofu ya ngeli ya tisa.

10. <u>Ngeli ya kumi na moja</u>

Kiambishi cha ngeli hii ni {lu -} ingawa tuna kiambishi {βu-} katika baadhi ya majina. Tuna mifano kama vile.,

| | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 85 | /luki/ | - | [luki] | ukuni |
| | /lumbɔ/ | - | [lumbɔ] | wimbo |
| | /luŋgɔ/ | - | [luŋgɔ] | uteo |
| | /lum/ | - | [lumi ] | ulimi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| /lukɔ/ | - | [lukɔ] | mwiko wa kupakua chakula |
| /βuʃu/ | - | [βuʃu] | uso |
| / βuli/ | - | [βuli] | kitanda |
| / βuki/ | - | [βuki] | asali |
| / βulalɔ/ | - | [βulalɔ] | nafasi au kitanda |
| / βula/ | - | [βula] | matumbo |

12. <u>Ngeli ya kumi na mbili</u>

Kiambishi cha ngeli nomino hii nni {tʃu-} na majina yaliyoko kwenye ngeli hii ni wingi wa ngeli ya kumi na moja hasa yale majina yenye kiambishi {lu -} kwa mfano,

| | | | | **Maana** |
|---|---|---|---|---|
| 86 | /tʃuki/ | - | [tʃuki] | kuni |
| | /tʃumbɔ/ | - | [tʃumbɔ] | nyimbo |
| | /tʃuŋgɔ/ | - | [tʃuŋgɔ] | teo |
| | /tʃumi/ | - | [tʃumi] | ndimi |
| | /tʃuko/ | - | [tʃukɔ] | miiko ya kupakulia |

13. <u>Ngeli ya kumi na tatu</u>

Kiambishi cha ngeli nomino hii ni [ka-] zinazopatikana kwenye ngeli hii ni zile zinazosisitiza hali ya udogo wa nomino husika kwa mfano.

| | | | | <u>Maana</u> |
|---|---|---|---|---|
| 87 | /kamundu/ | - | [kamundu] | mtu mdogo |
| | /kamburi/ | - | [kamburi] | mbuzi mdogo |
| | /katʃɔŋgɔ/ | - | [katʃɔŋgɔ] | Ndege mwitu |
| | /kalwau/ | - | [kalwau] | mguu mdogo |
| | /kandɔ/ | - | [kandɔ] | kitu kidogo |
| | /kalukɔmbɛ/ | - | [kalukɔmbɛ] | sehemu ndogo |
| | /kamswara/ | - | [kamswara] | ugali mdogo |

14. <u>Ngeli ya kumi na nne</u>

Kiambishi cha ngeli hii {βu-}. Tofauti na ngeli ya kumi na moja, nomino za ngeli hii aghalabu ni za kidhahania, kama vile,

| | | | | **Maana** |
|---|---|---|---|---|
| 88 | /βukɔŋgɔ/ | - | [βukɔŋgɔ] | Ugonjwa |
| | /βusabi/ | - | [βusabi] | uchawi |
| | /βukɛlu/ | - | [βukɛlu] | upumbavu |
| | /βuɣɔsi/ | - | [βurɔsi] | uzee |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| /βu + ɔβa/ | - | [βuɔβa] | [βɔβa] | woga |
| /βu + ɔmi/ | - | [βuɔmi] | [βɔmi] | uanaume |
| /βu + asi/ | - | [βuasi] | [βwasi] | tabu |
| /βu + ai/ | - | [βuai] | - [βwai] | usichana |

Mofu ya ngeli hii {βu-} inabainika kuwa na alomofu tatu,

89 /βu-/ < [βu- / βɔ- / βw-]

15. Ngeli ya kumi na tano

Kiambishi cha ngeli nomino hii ni {ku-}. Nomino za ngeli hii zimetokana na vitenzi nazo huchukua kiambishi hicho ambacho ni kisoukomo. Kwa mfano.

90

| | | | **Maana** |
|---|---|---|---|
| /kubɔra/ | - | [kubɔra] | kuimba |
| /kuvina/ | - | [kuvina] | kucheza ngoma |
| /kulua/ | - | [kulua] | kuchafuka |
| /kukɛla/ | - | [kukɛla] | kupumbaa |
| /kuɣɛnda/ | - | [kuɣɛnda] | kuenda |
| /kubona/ | - | [kubona] | kuona |
| /kudɛka/ | - | [kudɛka] | kupika |
| /kulaɣaja/ | - | [kulaɣaja] | kuporea |
| /kuɣada/ | - | [kuɣada] | kuwa mvivu |
| /kulɛɣa/ | - | [kulɛɣa] | kukataa |

16. Ngeli ya kumi na sita

Hii ni ngeli nomino inayoashiria mahali karibu. Katika Kidawida neno linalotumika hususan ni [aha] kwa mfano.

91

| | **Maana** |
|---|---|
| [tʃɔ: aha] | njoo hapa |
| [kutʃɛ aha] | uje hapa |
| [rɛda aha] | lete hapa |

17. Ngeli ya kumi na saba

Ni ngeli nomino inayoashiria mahali mbali kidogo. Neno linalotumika kurejelea mahali mbali kidogo ni [aja] kwa mfano,

92

| | **Maana** |
|---|---|
| [ɣɛnda aja] | nenda pale |
| [ziɣanda aja] | angalia pale |

[kwadumwa aja]	umetumwa pale

18. Ngeli ya kumi na nane

Hii ni ngeli nomino inayoashiria mahali palipo ndani ya kitu au mahali fulani. Mara nyingi neno linalotumika kurejelea mahali aina hii ni [aho]. Zaidi ya hayo neno hilo linapotumika huwa pia tunaongeza kiambishi tamati [-ni] kwenye neno linalosimamia mahali husika. Kwa mfano,

| | | **Maana** |
|---|---|---|
| 93 | [ahɔ numbɛni] | nyumbani |
| | [ahɔ mwandɔni] | mkutanoni |
| | [ahɔ muzini] | kijijini |

Kutokana na haya, tunaweza kusema kwamba Kidawida kina jumla ya ngeli nomino kumi na nane (18) zikiwemo:-

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 94. | 1. {Mu-} | 5. {i-} na {Ku-} | 9. {N-} | 13 {ka-} |
| | 2. {βa-} | 6. {Ma-} | 10.{N-} | 14.{βu-} |
| | 3. {Mu-} | 7. {Ki}] | 11. {Lu-} na {βu-} | 15. {Ku-} |
| | 4. {Mi-} | 8. {Vi-} | 12. {tʃu-} | 16. {aha} |
| | | | | 17. {aja} |
| | | | | 18.{ahɔ} |

## 2.6 HITIMISHO

Malengo ya sura hii yalikuwa mawili. Tulikuwa na azima ya kutoa orodha ya fonimu, pamoja na ngeli nomino za Kidawida.

Tumeweza kutimiza malengo hayo kwanza kwa kuibuka na jumla ya fonimu thelathini na sita (36) za Kidawida. Aidha tumefaulu kujitokeza na ngeli nomino za lugha hii ambazo ni kumi na nane (18).

Kwa kupata matokeo hayo, sura hii imefaulu kutoa sarufi ya lugha ya Kidawida, kama alivyosema Larry M. Hyman (1975:2) kuwa kazi aina hii ni sehemu mojawapo muhimu katika, mtalaa wa somo la fonolojia[26].

## TANBIHI


1. Larry Hyman (1975): Phonology: Theory and Analysis. New York: Holt, Runehart and Wilson. 2
2. Joan B. Hooper, (1976): An Introduction to Natural Generative Phonology. New York Academic Press.
3. Larry Hyman, (Opp. Cit.) 3
4. Richard S. Mgullu, (1999): Mtalaa wa Isimu. Longhorn Publishers Kenya Limited. 48
5. Larry Hyman, (Opp. Cit) 59
6. Richard S. mgullu, (Opp. Cit) 54
7. Ibid 55
8. Ibid 62
9. Ibid 63
10. Larry Hyman, (opp. Cit). 60
11. Richard S. Mgullu (opp. Cit) 63
12. Roger Lass, (1984): Phonology: An Introduction to basic concepts. Cambridge University Press, Cambridge, London, New York, New Rochelle, Melbourne, Sydney. 18
13. Malcolm Guthrie (1948): The classification of the Bantu languages. London, International African Institute/ Oxford University Press. 45
14. TUKI (1990): Kamusi sanifu ya isimu na lugha. Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili: TUKI /UNESCO/SIDA. 31.
15. Ibid 27
16. Kithaka wa Mberia (1981) : The consonants of Kitharaka. M.A. Theses. University of Nairobi.
17. Richard S. Mgullu, (opp cit). 29
18. Ibid. 29
19. Ibid 29
20. Ibid 28
21. TUKI (opp. cit). 42

22. Edgar C. Polome (1967): Swahili language handbook. Washington: centre for Applied Linguistic. 96

23. Ibid. 97

24. Ibid. 99

25. Ibid. 100

26. Ibid 100

27. Larry Hyman (opp cit). 2

# SURA YA TATU

## 3.0 UTANGULIZI

Lengo letu kwenye sura hii ni kuratibu mabadiliko ya kifonolojia yanayopatikana katika Kidawida.

Kwa kuwa mabadiliko ya kifonolojia katika Kiswahili tayari yamesharatibiwa na kazi zingine kama vile Margaret Njuguna (1972) na Mohamed Bakari (1982) hatutarudia kuratibu tena mabadiliko hayo kwenye kazi hii.Hata hivyo baadaye kwenye utafiti huu tutaweza kulinganisha mabadiliko ya kifonolojia baina ya Kiswahili na Kidawida.

Vigezo tutakavyotumia katika kuangalia mabadiliko haya kwenye Kidawida ni pamoja na -:

a) Kile kinachobadilikia
b) Matokeo ya mabadiliko hayo
c) Motisha ya mabadiliko hayo
d) Upeo wa mabadiliko hayo.

Kwa ambavyo utafiti wetu umejikita katika nadharia zalishi, tutatumia sheria za kifonolojia ambazo zitaonyesha uhusioano uliopo baina ya muundo wa ndani na muundo wa nje,kama anavyosisitiza Joan B. Hooper (1976:IX) .

Tutazingatia zaidi sheria ailika za Sanford A,Schane (1973:207), Schane anagawanya sheria asilia au za kutarajiwa katika kategoria tatu kuu.Nazo ni sheria za uwiano (usimulisho), sheria za muundo mwafaka wasilabi, na sheria za kutengana kwa sauti mbali iwezekanavyo.

Hata hivyo si sheria zote ambazo ni asilia, kuna baadhi ya sheria ambazo hutegemea mazingira ya kimofofonolojia au leksia, na sheria hizi hutofautiana katika lugha mbalimbali.

Sifa ya sheria ailia ni kwamba, kwanza hizi ni sheria zinazopatikana katika lugha nyingi za ulimwengu ikiwa si zote, Pili sheria asilia huwa na sifa ya urudiaji katika lugha hivi kwamba unapata sheria hiyo ikijitokeza mara kwa mara katika lugha husika. Tatu sheria asilia huhusu zaidi msuala ya kifonetiki,si ajabu basi sheria hizi zina sifa ya ubia.
Haya ni kwa mujibu wa Sanford A. Schane (1973:200).

## 3.1 KUDONDOSHWA KWA IRABU

Sanford A.Schane (1973:209) anasema, mojawapo ya sheria asialia zinazohusu sheria za muundo mwafaka wa silabi ni ile ya kudondoshwa kwa irabu. Inaweza kudondolewa inapotangulia irabu nyingine. Pia tunaongeza kusema kwamba katika kidawida na lugha zingine za kibantu, imeonekana kuwa irabu inaweza kudondolewa inapotangulia konsonanti.

Irabu inaweza kudondoleshwa inapotangulia konsonanti katika mazingira ya kiambishi cha ngeli kinapofua tana na sheria linaanzaa kwa konsonanti. Mifano yetu tunaipata katika ngeli nomino za 1 na 3: -

| | | | | | **Maana** |
|---|---|---|---|---|---|
| Ngeli 1 | /mu+ndu/ → | [m̩+ndu] → | [m̩u+ndu] → | [m̩ndu] | mtu |
| | / mu + ka / → | [m+ka] → | [m̩+ka] → | [m̩ka] | mke |
| | /mu+kundwa/ → | [m+kundwa] → | [m̩+kundwa] → | [m̩kundwa] | mpendwa |
| Ngeli 3 | | | | | |
| | / mu+di/ → | [ m+di] → | [m̩+di] → | [m̩di] | mti |
| | / mu+zi/ → | [m+zi] → | [m̩+zi] → | [m̩zi] | Kijiji |
| | /mu+kɔβa/ → | [m+kɔβa] → | [m̩+ kɔβa] → | [m̩kɔβa] | mkia |
| | /mu+kwatʃu/ → | [m+kwatʃu] → | [m̩+kwatʃu] → | [m̩kwatʃu] | mkwaju |

/mu+sigɔ/ → [m+sigɔ] → [m̩+sigɔ] → [m̩sigɔ]   mzigo

Katika mfanyiko huu, Irabu /u/ inadondoshwa kasha nasali /m/ Inapokezwa sifa ya usilabi au mkazo. Matokeo yake ni neon linaloanzia kwa nasali iliyosilabishwa. Badiliko hili yamkuu ni la kihistoria kwa ambavyo motisha yake si ya kifonologia kama inavyotokea katika mifanyiko mingine. Tuna baadhi ya maneno yaliyoko katika kundi hilihili la maneno lakini haipitikiwi na badiliko hili, kwa mfano

| | **Maana** |
|---|---|
| /mu + fu / - [mufu] | unga |
| /mu + indi/ - [muindi] | mguu |
| /mu + mbi/ - [mumbi] | mwili |

Sanford A. Schane (1973: 202) anasisitiza umuhumu wa kuzingatia ruwaza ya mifanyiko yoyote ile ya kifonolojia hasa ile asilia. Kwa sababu hiyo, ruwaza ya mifanyiko kwenye mifano yetu hapo juu lazima ifuatane kama tulivyopanga. Hivi ni kusema kwamba mfanyiko wa kwanza ni ule wa kudondosha irabu /u/ kabla ya kuipokeza nasali /m/ sifa ya usilabi. Hii ni kwa sababu hapo awali sifa ya mkazo zua usilabi ilikuwa ni ya irabu /u/ lakini baada ya irabu hiyo kuondolewa ilibidi sifa hiyo kupokezwa nasali /m/. Kwa sababu hiyo hatuwezi kupangua ruwaza hiyo kwa kwanza na usilabishaji wa nasali /m/ kasha kufuatwe na kuondelewa kwa irabu /u/. Tukifanya hivi itakuwa ni makosa kwa sababu sheria asilia lazima mtendo huo. Hivyo basi sheria tunayoipata katika mfanyiko huu ni: -

3) $$\begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ +\text{juu} \\ +\text{nyuma} \end{bmatrix} \longrightarrow \emptyset \; / \; \# \begin{bmatrix} +\text{konsonanti} \\ +\text{nasali} \end{bmatrix} \text{———} \; + \; [+\text{kons}]$$

Aidha irabu inaweza kudondoshwa wakati inatangulia irabu nyingine. Kwa mujibu wa sheria ya muundo mwafaka wa silabi, kunapokuwa na mfuatano wa irabu, mara nyingi moja ya irabu hizo ama hudondoshwa au kuyevushwa, au

wakati mwingine konsonanti huingizwa katikati ya irabu hizo ili kuvunja ule mkururo wa irabu. Sheria hii tunaipata kwenye ngeli romino ya 2,5 na 14 za kidawida: -

| | | | **Maana** |
|---|---|---|---|
| Ngeli 2 5 | / βa+ai/ → | [βai] | Wasichana |
| | / βa+ana / → | [βana] | Watoto |
| | / βa+avi/ → | [βavi] | Wazazi |
| | / βa+adamu/ → | [βadamu] | Wanadamu |

Hata hivyo, kama asemavyo Edgar C. Polome (1967:60) mfanyiko huu hauwezi kutokea pale ambapo nomino za ngeli hii zimeundwa kutokana na vitenzi, kama vile,

| | | | **Maana** |
|---|---|---|---|
| 6 | /Ba+aɣi/ → | [ Ba : ɣi] | "Wajenzi" |

Hapa tunaona kwamba irabu haikudondolewa. Vilevile tuangalie vivumishi na vimilikilishi katika ngeli ya 2,

7

| | | | **Maana** |
|---|---|---|---|
| Ngeli 2 | /βa+ɔsɛ/ → | [βɔsɛ] | wote |
| | / βa+apɔ/ → | [βapɔ] | wangu |
| | / βa+akɔ/ → | [βakɔ] | wako |
| | / βa+akɛ/ → | [ βakɛ] | wake |

Sheria inayohusu mfanyiko huu ni

8 [+ silabi, - juu, + nyuma] → Ø / # [+konsonanti] ______ + { [+ silabi, - juu, + nyuma] ; [+ silabi, + juu, + nyuma] }

Aidha tuna kivumishi hiki,

| | | | **Maana** |
|---|---|---|---|
| 9 | /βa+ingi/ → | [ βangi] | wowote |

Sheria yake ni,

10
$$\begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ +\text{juu} \\ -\text{nyuma} \end{bmatrix} \rightarrow \varnothing \; / \; \begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{juu} \\ +\text{nyuma} \end{bmatrix} + \underline{\qquad}$$

Ngeli 14

11

| | | **Maana** |
|---|---|---|
| /βu+ɔβa/ → | [βɔβa] | woga |
| /βu+ɔmi/ → | [βɔmi] | uanaume |

Sheria yake ni

12
$$\begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ +\text{juu} \\ +\text{nyuma} \end{bmatrix} \rightarrow \varnothing \; / \; \# \begin{bmatrix} +\text{konsonanti} \end{bmatrix} \underline{\qquad} + \begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{juu} \\ +\text{nyuma} \end{bmatrix}$$

Vilimikisho vya ngeli ya 5 pia vinaonyesha kudondoshwa kwa irabu,

| | | | Maana |
|---|---|---|---|
| 13 | /ji + apɔ/ → | [japɔ] | langu |
| | /ji + akɛ/ → | [jakɛ] | lake |
| | /ji + aβɔ/ → | [jaβɔ] | lao |
| | /ji + akɔ/ → | [jakɔ] | lako |
| | /ji + ɛdu/ → | [j ɛdu] | letu |
| | /ji + ɛŋu/ → | [jɛnu] | lenu |

Sheria yake ni,

14

$$\begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ +\text{juu} \\ -\text{nyuma} \end{bmatrix} \longrightarrow \emptyset \Big/ \# \begin{bmatrix} +\text{konsonanti} \end{bmatrix} + \left\{ \begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{juu} \\ +\text{nyuma} \\ \\ +\text{silabi} \\ -\text{juu} \\ -\text{nyuma} \end{bmatrix} \right\}$$

Pamoja na hayo, kundondoshwa kwa irabu hutokea katika hali ya kuwepo kwa mvutano wa irabu. Mvutano wa irabu ni sheria inayohusu sauti mbili za irabu kuongana na kupata irabu mpya ya katikati. Mfanyiko huu una sheria nyingi ndani yake ambayo huishia kwa irabu inufutiliwa mbali. Kwa mfano katika Kidawida tuna:-

15

i) Shadda la a + i ⟶ ɛ

| | | | | | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ngeli 2 | /βa + iŋgi/ | ⟶ | [βaɛŋgi] | ⟶ | [βɛɛŋgi] | ⟶ | [βɛŋgi] | wengi |
| Ngeli 2 | / βa + ik ɛ/ | ⟶ | [βaɛkɛ] | ⟶ | [βɛɛkɛ] | ⟶ | [βɛkɛ] | akina |
| Ngeli 2/ | βa + ikɔ/ | ⟶ | [βaɛkɔ | ⟶ | [βɛɛkɔ] | ⟶ | [βɛkɔ] | wako mahali |
| Ngeli 3 | /da +ikɔ/ | ⟶ | [daɛkɔ] | ⟶ | [dɛɛkɔ] | ⟶ | [dɛɛkɔ] | tuko |
| Ngeli 5 | /sa + iji/ | ⟶ | [saɛji] | ⟶ | [sɛɛji] | ⟶ | [saɛji] | jinsi |
| Ngeli 10 | /ra + ikɔ/ | ⟶ | [raɛkɔ] | ⟶ | [rɛɛkɔ] | ⟶ | [rɛkɔ] | ziko |
| Ngeli 6 | /ra + idu/ | ⟶ | [ɣaɛdu] | ⟶ | [ɣɛɛdu] | ⟶ | [ɣɛdu] | zetu |
| Ngeli 2 | /na + isi/ | ⟶ | [naɛsi] | ⟶ | [nɛɛsi] | ⟶ | [nɛsi] | nasi |
| Ngeli 9 | /a + ikɔ/ | ⟶ | [aɛkɔ] | ⟶ | [ɛɛkɔ] | ⟶ | [ɛkɔ] | iko |
| Ngeli 10 | /ra + idu/ | ⟶ | [raɛdu] | ⟶ | [rɛɛdu] | ⟶ | [rɛɛdu] | zetu |

Kuna sheria tatu katika mfanyiko huu. Kwanza irabu ya + juu /i/ inavutwa chini na kuwa ya – juu /ɛ/. Pili irabu ya + nyuma /a/ inavutwa mbele na kuwa ya – nyuma /ɛ/ vilevile. Mwisho moja wapo ya irabu hizo zinadondoshwa. Sheria zake ni:-

16

$$\begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{juu} \\ -\text{nyuma} \end{bmatrix} \longrightarrow \begin{bmatrix} -\text{juu} \end{bmatrix} \Big/ \begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{juu} \\ +\text{nyuma} \end{bmatrix} + \underline{\quad\quad}$$

17 $$\begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{juu} \\ +\text{nyuma} \end{bmatrix} \rightarrow [-\text{nyuma}] \;/\; ___ \begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{juu} \\ -\text{nyuma} \end{bmatrix}$$

18 $$\begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{juu} \\ -\text{nyuma} \end{bmatrix} \rightarrow \varnothing \;/\; ___ \begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{juu} \\ -\text{nyuma} \end{bmatrix} \quad \text{au} \quad \begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{juu} \\ -\text{nyuma} \end{bmatrix} ___$$

19 ii) Shadda la a + e → ε

| | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|
| Ngeli 2 | /βa + εdu/ → | [βεεdu] → | [βεdu] | wetu |
| | /βa + εkεri/ → | [βεεkεri] → | [βεkεri] | peke yao |
| | /βa + εka/ → | [βεεka] → | [βεka] | peke yao |

Mfanyiko huu una sheria mbili. Moja ni ya kubadilisha irabu ya + nyuma /a/ iwe ya – nyuma /ε/. Ya pili ni ya kudondosha moja ya irabuu hizo. Sheria yake ni,

20 $$\begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{juu} \\ +\text{nyuma} \end{bmatrix} \rightarrow [-\text{nyuma}] \;/\; ___ + \begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{juu} \\ -\text{nyuma} \end{bmatrix}$$

21 $$\begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{juu} \\ +\text{nyuma} \end{bmatrix} \rightarrow \varnothing \;/\; ___ \begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{juu} \\ -\text{nyuma} \end{bmatrix} \quad \text{au} \quad \begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{juu} \\ +\text{nyuma} \end{bmatrix} ___$$

Shadda la a + ɔ ⟶ ɔ

| | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|
| Ngali 2 | /βa + ɔsɛ/ ⟶ | [ βɔɔsɛ] ⟶ | [βɔsɛ] | wote |

Katika mfanyiko huu irabu ya – mkazo, /a/ inabadilika na kuwa ya + mkazo /ɔ/, mwishowe moja ya irabu hizo inadondoshwa. Sheria ya mfanyiko huu ni,

$$\begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{juu} \\ +\text{nyuma} \\ +\text{mkazo} \end{bmatrix} \longrightarrow [-\text{mkazo}] \;/\; ___ + \begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{juu} \\ +\text{nyuma} \\ -\text{mkazo} \end{bmatrix}$$

$$\begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{juu} \\ +\text{nyuma} \\ +\text{mkazo} \end{bmatrix} \longrightarrow \varnothing \;/\; ___ \begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{juu} \\ +\text{nyuma} \\ -\text{mkazo} \end{bmatrix} \text{ au } \begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{juu} \\ +\text{nyuma} \\ -\text{mkazo} \end{bmatrix} ___$$

iv Shadda la u + ɔ ⟶ ɔ


Ngeli 14


| | | | Maana |
|---|---|---|---|
| /βu + ɔβa/ ⟶ | [βɔɔβa] ⟶ | [βɔβa] | woga |
| /βu + ɔmi/ ⟶ | [βɔɔri] ⟶ | [βɔmi] | wanaume |
| /βu + ɔri/ ⟶ | [βɔɔri] ⟶ | [βɔri] | wazi |

16 – 18

| | | | |
|---|---|---|---|
| / ku + ɔsɛ/ ⟶ | [kɔɔsɛ] ⟶ | [kɔsɛ] | Kote |

Katika mfanyiko huu irabu ya + juu /u/ inavutwa chini na kuwa ya juu /ɔ/. Pili moja ya irabu hizo inadodolewa. Sheria yake ni,




## 2 KUUNDWA KWA NUSU – IRABU

Sanford A. Schane (1973:209) anasema kuwa kuundwa kwa nusu – irabu vilevile ni mojawapo ya zile mbinu zinazotumika kuleta ule muundo mwafaka wa silabi hasa pale kunapokuwa na mfuatano wa ikrabu katika neno.

Sheria hii tunapata katika ngeli nomino za 1, 3, 4, 11, 13 na 17 kama ifuatavyo:-

geli 1

| | | **Maana** |
|---|---|---|
| /mu + ai/ ⟶ | [mwai] | msichana |
| /mu + ana/ ⟶ | [mwana] | mtoto |
| /mu + aɣi/ ⟶ | [muaɣi] | mjenzi |
| /mu + ɛli] ⟶ | [mwɛli] | msafi au mtakatifu |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 30 | /mu + a + ɛla/ → [mwa ɛla] | | Haya ni majina ya kiume |
| | /mu + a + mbɛla/ → [mwambɛla] | | ya watu yanayotokana |
| | /mu + a + liβa/ → [mwaliβa] | | na vitenzi au majina mengine |
| | /mu + a + jala/ → [mwanjala] | | |
| 31 | /u + a + kɛʃɔ/ → [Wakɛʃɔ] | | Vilevile haya ni majina |
| | /u + a + βuda/ → [Waβuda] | | ya watu wa kile |
| | /u + a + njala/ → [Wanjala] | | yanayotokana na majina |
| | /u + a + kiɔ/ → [Wakiɔ] | | au vitenzi |
| | | | **Maana** |
| 32 | /u + a + ida/ → [waida] | | amepita |
| 33 | /mu + ɛŋgɛrɛ/ → [mwɛŋgɛrɛ] | | mwangaza |
| | /ɣu + ake/ → [ɣw ake] | | wake |
| Vimilikishi | | | |
| | /ɣu+akɔ/ → [ɣwakɔ] | | wako |
| 34 | /ɣu+apɔ/ → [ɣwapɔ] | | wangu |
| | /ɣu+aβɔ/ → [ɣwaβɔ] | | wao |
| 35 | /lu + aka/ → [lwaka] | | sauti |
| | /lu + ala/ → [lwala] | | |
| 36 Vimilikishi Ngeli 11 | /lu + apɔ/ → [lwapɔ] | | wangu |
| | /lu + akɔ/ → [lwakɔ] | | wako |
| | /lu + aβɔ/ → [lwaβɔ] | | wao |
| | /lu + akɛ/ → [lwakɛ] | | wake |
| 37 Ngeli 13 | /tʃu + aka/ → [tʃwaka] | | sauti |
| 38 Ngeli 15 | /ku + a +ɛla] → [kwaɛla] | | kumekucha/umetakata |
| | /ku + a + βɔna] → [ kwaβɔna | | umeona |
| | /ku + a + ida/ → [kwaida] | | umepita |

/ku + a + ʧa/ ⟶ [kwaʧa] umekuja

Vimilikishi vya ngeli 16 –18

| | | |
|---|---|---|
| 39 /ku + akɔ/ | ⟶ [kwakɔ] | kwako |
| /ku + aβɔ/ | ⟶ [kwaβɔ] | kwao |
| /ku + akɛ/ | ⟶ [kwakɛ] | kwake |
| /ku + apɔ/ | ⟶ [kwapɔ] | kwangu |

Mifano hiyo yote inaonyesha kuundwa kwa nusu-irabu [w], katika mazingira mbalimbali. Wakati mwingine kunapokuwa na mfuatano wa irabu, badala ya irabu moja kudondolewa na mfuatano wa irabu /u/ inabadilika na kuwa nusu-irabu [w] inapotangulia irabu nyingine.

40
$$\begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{juu} \\ +\text{nyuma} \end{bmatrix} \longrightarrow [-\text{silabi}] \ / \ \underline{\quad\quad} + \left\{ \begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{juu} \\ +\text{nyuma} \\ \\ +\text{silabi} \\ -\text{juu} \\ -\text{nyuma} \end{bmatrix} \right\}$$

Hali kadhalika nusu – irabu /j/ huundwa katika ngeli nomino 4, 8, na 9 za lugha hii, kwa mfano: -

Vimilikishi vya ngeli ya 4, 9

| | | **Maana** |
|---|---|---|
| 41 / i + apɔ/ | ⟶ [japɔ] | yangu |
| / i + akɔ/ | ⟶ [jakɔ] | yako |
| /i + akɛ/ | ⟶ [jake] | yake |
| /i + ɛdu/ | ⟶ [j ɛdu] | yetu |
| /i + aβɔ/ | ⟶ [jaβɔ] | yao |

Sheria ya badiliko hilo ni:-

42 $$\begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{juu} \\ +\text{nyuma} \end{bmatrix} \longrightarrow [-\text{silabi}] \; / \; \# \; ____ + \left\{ \begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{juu} \\ +\text{nyuma} \\ +\text{silabi} \\ -\text{juu} \\ -\text{nyuma} \end{bmatrix} \right\}$$

Katika sheria huyo irabu /i/ inabadilika na kuwa nusu – irabu [j] inapotangulia irabu nyingine .

Katika ngeli ya 8, nusu-irabu /j/ huundwa ingawa baadaye inadondoshwa:-

Ngeli 8

| | | | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 43 | /vi + adu/ | ⟶ | [vjadu] | ⟶ | [vadu] | viatu |
| | /vi + ɔrɔ/ | ⟶ | [vjɔrɔ] | ⟶ | [vɔrɔ] | vyoo |
| | /vi + aŋgu/ | ⟶ | [vjaŋgu] | ⟶ | [vaŋgu] | viboko /fimbo |
| | /vi + ala/ | ⟶ | [vjala] | ⟶ | [vala] | vidole |

Vimilikishi

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| /vi + apɔ/ | ⟶ | [vjapɔ] | ⟶ | [vapo] | vyangu |
| / vi + akɔ/ | ⟶ | [vjakɔ] | ⟶ | [vakɔ] | vyako |
| /vi + ɛdu/ | ⟶ | [vjɛdu] | ⟶ | [vɛdu] | vyetu |

Katika mfano huo mambo mawili yanafanyika. Kwanza kutokana na mkururo wa irabu mbili, nusu – irabu [j] inaundwa kutoka kwa irabu /i/,pili, hiyo nusu – irabu inadondoshwa:-

44 $$\begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{juu} \\ +\text{nyuma} \end{bmatrix} \longrightarrow [\text{silabi}] \; / \; ____ + \left\{ \begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{juu} \\ +\text{nyuma} \\ \\ +\text{silabi} \\ -\text{mkazo} \\ +\text{nyuma} \\ \\ +\text{silabi} \\ -\text{mkazo} \\ -\text{nyuma} \end{bmatrix} \right\}$$

45

$$\begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{konsonanti} \\ -\text{nyuma} \end{bmatrix} \longrightarrow \varnothing \; / \; \# \begin{bmatrix} +\text{konsonanti} \\ -\text{nyuma} \end{bmatrix} ___ +$$

## 3.3 UKAAKAISHAJI

Ukaakaishaji ni mfanyiko wa kifonojia unaohusu kuathiriwa na kubadilika kwa mahali pa kutamkia kuathiriwa na kubadilika kwa mahali pakutamkia. Ukaakaishaji hutokea pale ambapo sauti iliyokuwa ikitamkwa mahali fulani kwenye kinywa inaathiriwa na sauti nyingine hivi kwamba mahali pake pa kutamkia panabadilika na kuwa aghalabu kwenye kaakaa gumu [6] ,chambilecho Roger lass (1984: 169). Katika kidawida mfanyiko huu kuhusu ngeli nomino ya 7 ambapo sauti ya mtuo /k/ ya kaakaa laini inabadilika na huwa kizuiwa – kwamizwa cha kaakaa gumu [tʃ ] kwa sababu ya kuathiriwa na irabu ya mbele /i/ kwa mfano.

Ngeli 7

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | **Maana** |
| 46 | /ki + ala/ → | [tʃiala] → | [tʃjala] → | [tʃala] | Kidole |
| | /ki + arɔ/ → | [tʃiarɔ] → | [ tʃjarɔ] → | [tʃarɔ] | Kazi |
| | /ki + aŋgu/ → | [tʃiaŋgu] → | [tʃjaŋgu] → | [tʃaŋgu] | fimbo |
| | /ki + ɔŋgɔ/ → | [tʃiɔŋgɔ] → | [tʃjɔŋgɔ] → | [tʃɔŋgɔ] | kichwa |
| | /ki + ɔrɔ/ → | [tʃɔrɔ] → | [tʃjɔrɔ] → | [tʃjɔrɔ] | choo |
| | /ki + adu/ → | [tʃiadu] → | [tʃjadu] → | [tʃadu] | kiatu |

**Vimilikishi**

47

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| /ki + apɔ/ → | [tʃiapɔ] → | [tʃjapɔ] → | [tʃapɔ] | changu |
| /ki + akɔ/ → | [tʃiakɔ] → | [tʃjakɔ] → | [tʃakɔ] | chako |
| /ki + akɛ/ → | [tʃiakɛ] → | [tʃjakɛ] → | [tʃakɛ] | chake |
| /ki + ɛdu/ → | [tʃiɛdu] → | [tʃjɛdu] → | [tʃɛdu] | chetu |
| /ki + ɛnu/ → | [tʃiɛnu] → | [tʃjɛnu] → | [tʃɛnu] | chenu |
| /ki + aβɔ/ → | [tʃiaβɔ] → | [tʃjaβɔ] → | [tʃaβɔ] | chao |

**Kivumishi**

48

/ki + ɔsɛ/ → [tʃiɔsɛ] → [tʃjɔsɛ] → [tʃɔsɛ] chote

**Vitenzi**

49

/ki + a + sia/ → [tʃiasia] → [tʃjasia] → [tʃasia] kimeisha
/ki + a + βɔka/ → [tʃiaβɔka] → [tʃjaβɔka] → [tʃaβɔka] kimependeza
/ki + a + dua/ → [tʃiadua] → [tʃjadua] → [tʃadua] kingali kipo
/ki + a + βurwa/ → [tʃiaβurwa] → [tʃjaβurwa] → [tʃaβurwa] kimeiva

Mfanyiko huu una sheria tatu. Kwanza ni sheria ya ukaakaishaji ambayo inafuata na sheria zingine mbili:-

50
$$\begin{bmatrix} +\text{konsonanti} \\ +\text{nyuma} \end{bmatrix} \rightarrow [-\text{nyuma}] \;/\; \#\;____ \begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ +\text{juu} \\ -\text{nyuma} \end{bmatrix}$$

51
$$\begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ +\text{juu} \\ -\text{nyuma} \end{bmatrix} \rightarrow [-\text{silabi}] \;/\; ____ \; [+\text{silabi}]$$

52
$$\begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ +\text{juu} \\ -\text{nyuma} \end{bmatrix} \rightarrow \varnothing \;/\; \#\;_ \begin{bmatrix} +\text{konsonanti} \\ -\text{nyuma} \end{bmatrix}$$

## 3.4 MKUBALIANO WA IRABU

Irabu hukubaliana katika maneno hasa vitenzi vya kauli mbalimbali. Kwa mintarafu ya Sanford A. Scheme (1973 : 207), irabu huweza kukubaliana kwa hali

ya urefu unyuma au umviringo na irábu nyingine[7] jinsi inavyotokea kwenye mfanyiko wa mkubaliano wa irabu.

Mkubaliano wa irabu ni mojawapo ya sheria na uwiano kwa ambavyo vipashio vinaathiriana kisifa japo kwa mbali. Tuna mifano katika kidawida

Vitenzi vya hali ya kutenda

53

| **Kutenda** | **Maana** | **Kutenda** | **Maana** |
|---|---|---|---|
| [ rama ] | ruka | [ramia ] | rukia |
| [aɣa] | jenga | [aɣia] | jengea |
| [zama] | haribika | [zamia] | chukiza |
| [sɛka] | cheka | [sɛkia] | chekea |
| [rɛda] | leta | [rɛdia] | letea |
| [lɛɣa] | kataa | [lɛɣia] | katalia |
| [sɛla] | tembea | [sɛlia] | tembelea |
| [siɣa] | acha | [siɣia] | achia |
| [siŋga] | kolea utamu | [siŋgia] | kolea utamu |
| [iβa] | iba | [iβia] | ibia |
| [sima] | shinda | [simia] | shindia |
| [lɔmba] | omba | [lɔmbɛa] | ombea |
| [bɔra] | imba | [bɔrɛa] | imbia |
| [ɣɔra] | sema/amba | [ɣɔrɛa] | ambia |
| [kɔra] | choma | [kɔrɛa] | chomea |
| [tʃura] | jaza | [tʃurɛa] | jazia |
| [βuja] | rudi | [βuria] | rudia |
| [duka] | baba | [dukia] | bebea |
| [tʃumba] | pita | [tʃumbia] | pitia |

ii) Vitenzi vya ya kutendesha

54

| **Kutenda** | **Maana** | **Kutendesha** | **Maana** |
|---|---|---|---|
| [rama] | ruka | [ramiʃa] | rukisha |
| [zama] | haribika | [zamiʃa] | haribu |
| [sɛka] | cheka | [sɛkɛʃa] | chekesha |
| [sɛla] | tembea | sɛlɛʃa] | tembeza |
| [siŋga] | kolea utamu | [siŋgiʃa] | koleza utamu |
| [siɣa] | acha | [siɣiʃa] | achisha |
| [lɔmba] | omba | [lɔmbɛʃa] | ombesha |
| [bɔra] | imba | [bɔr ɛʃa] | imbisha |
| [duka] | baba | [dukiʃa] | babesha |
| [tʃumba] | pita | [tʃumbiʃa] | pitisha |

Tukiangalia vitenzi vya kauli ya kutenda tunapata kwamba kuna mkubaliano wa irabu za mizizi yz vitenzi na za viambishi vifuatilizi kwenye vitenzi hivyo. Kwenye mifano yetu, irabu [a], [ɛ ], [i] na [u] za mizizi ya vitenzi zinakubaliana na kiambishi kifuatilizi [i] kwa upamde mmoja, halafu irabu [ɔ ] ya mizizi ya vitenzi vinakubaliana na kiambishi kifuatilizi [ɛ ] kwa upande wa pili.

Katika kiwango cha kifonilojia, muundo wa ndani wa vitenzi hivyo huwa na mofu ya kitendea { - i -} ambyo tunaona ikibadilika katika muundo wa nje kulingana na mazingira ya kifonojia :-

| | **Muundo ndani** | | **Muundo nje** |
|---|---|---|---|
| 55 | /ram + i + a/ | ______ | [ramia ] |
| | /zam + i + a/ | ______ | [zamia] |
| | /sɛk + i + a/ | ______ | [sɛkia] |
| | /sɛl + i + a/ | ______ | [sɛlia] |
| | /siŋg+ i + a/ | ______ | [siŋgia] |
| | /siɣ + i + a/ | ______ | [siɣia] |
| | /duk + i + a/ | ______ | [dukia] |
| | /tʃumb + i + a/ | ______ | [tʃumbia] |
| | /lɔmb + i + a/ | ——→ | [lɔmbɛa] |
| | /bɔr + i + a/ | ——→ | [bɔr ɛa] |

Katika mifano hiyo mifanyiko ya uwiano hutokea kwenye baadhi tu ya vitenzi hivyo hasa zilke zenye irabu ya –mkazo [ɔ ] kwenye mzizi. Vitenzi vilivyo na mizizi yenye irabu [a], [ɛ], [i], na [ u ] hazionyeshi kubadilika kwa mofu ya kutenda { - i - }. Navyo vitenzi vyenye mizizi iliyo na irabu [ɔ ] vinaonyesja kubadilika kwa mofu ya kutenda { - i - } na kuwa { - ɛ - }, sheria hii ni ya uwiani ambapo /i/ inabadilika na kwa [ɛ ] kutokana na athari ya irabu ya mizizi /ɔ/ :-

56 [+ silabi, + juu, -nyuma] ——→ [-juu] / [+ silabi, -juu, +nyuma] ______

Tunapoangalia kauli ya kutendesha tunapata kwamba vitenzi vyenye mizizi hiyo na irabu kaze { a} , { i } na [u] zinakubaliana na kiambishi kifuatilizi { - iʃ- }. Nazo vitenzi vyenye mizizi hiyo na irabu hafifu [ɛ] na [ɔ] zinakubaliana na kiambishi kifuatilizi {- ɛʃ - }.

Katika kiwango cha kifonolojia, muundo wa ndani wa vitenzi hivyo huwa na mofu ya kutendesha {-iʃ-}. Mofu hiyo hubadiliks katika muundo wa nje kutegemea mazingara ya kifonojia, muundo wa nje kutegemea mazingara ya kifonolojia:-

57

| **Muundo ndani** | | **Muundo nje** |
|---|---|---|
| /ram + iʃ+ a / | ——— | [ramiʃa] |
| /zam + iʃ + a/ | ——— | [zamiʃa] |
| /siŋg+ iʃ + a/ | ——— | [siŋgiʃa] |
| /siɣ + iʃ + a/ | ——— | [siɣiʃa] |
| /duk + iʃ + a/ | ——— | [dukiʃa] |
| /tʃumb + iʃ + a/ | ——— | [tʃumbiʃa] |
| /sɛk + iʃ + a/ | ———> | [sɛkɛʃa] |
| /sɛl + iʃ + a/ | ———> | [sɛlɛʃa] |
| /lɔmb + iʃ + a/ | ———> | [lɔmbɛʃa] |
| /bɔr + iʃ + a/ | ———> | [bɔr ɛʃa] |

Mifano hiyo inaonyesha mofu ya kutendesha {- iʃ-} inabadilika nakuwa { - ɛʃ - }katika vitenzi vyenye mizizi iliyo na irabu hafifu [ɛ] na [ɔ], irabu hafifu imeathiri mofu ya kutendesha { - iʃ -} ikawa { - ɛʃ - },

58

$$/\text{iʃ}/ \longrightarrow [\text{ɛʃ}] \;/\; \begin{bmatrix} +\text{ silabi} \\ -\text{ mkazo} \end{bmatrix}$$

Kwa ambavyo mifanyiko hii inahusu unyambuaji, sheria hii tunaweza kusema ni ya kimofofonojia kwa sababu masuala ya mofolojia (unyambuaji) yamehusishwa. Hata hivyo sheria ya kifonolojia pia inaonekana hapa, hususan sheria ya uwiano. Hivi ni kusema kwamba sheria hizi wakati mwingine huingiliana.

## 3.5 MKUBALIANO WA NASALI NA KITAMKWA KINACHOFUATA

Vilevile hii ni sheria ya uwiano chambilecho Sanford A. Schane (1973:207). Sheria hii inapatikana kwenye ngeli ya 9/10 ambapo kiambishi awali chake ni nasali {N}, inaathiriwa mahali pake pa kutamkia kwa sababu ya kipashio kinachofuata pale inapoambishwa na madhiria ya nomino mbalimbali.

Matokeo yake ni kuwa mofu {n-} inabadilika na kuwa na sura nyingine (alomofu) ambazo pia ni nasali kutegemea ni kipashio gani kiliiathiri. Uwiano huu ni ania ya usilimisho kwa ambavyo vipashio vinaathiriana mahali pa kutamkia. Katika kidawida tuna mifano ifuatayo:-

Ngeli 9/10

59

| | | | **Maana** |
|---|---|---|---|
| /N + βaɣɔ/ → | [mbaɣɔ] | | "Nyati" |
| /N + βuri/ → | [mburi] | | "mbuzi" |
| /N + βɔ βa/ → | [mbɔβa] | | "shamba" |
| /N + ɣɔmbɛ/ → | [ŋgɔmbɛ] → | [ŋɔmbɛ] | "ng'ombe" |
| /N + ɣɔndi/ → | [ŋgɔndi] → | [ŋɔndi] | "kondoo" |
| /N + ɣuku/ → | [ŋguku] | | "kuku" |
| /N + lɛmbɔ/ → | [ndɛmbɔ] | | "mgomba" |
| /N + lazi/ → | [ndazi] | | "nzima" |
| /N + lɛi/ → | [ndɛ:] | | "babake/ze" |
| /N + ɔni/ → | [ɲoni] | | " nyuni" |
| /N + uŋgu/ → | [ɲuŋgu] | | "chungu" |
| /N + jala/ → | [ɲjala] | | "njaa" |
| /N + jau/ → | [ɲjau] | | "fahali" |

Katika mfanyiko huu kuna aina mbili za usilimisho. Kuna ule usilimisho mbele ambapo sauti inayofuata inaathiri sauti iliyoitangulia. Wakati neon linatamkwa, mtu huona kutamka sauti ya awali akitarajia na kujitayarisha kutamka sauti inayofuata. Kwa mfano tunapotamka neno 'mbogho' katika muundo wa ndani tunapata kwamba, kwanza tunatamka sauti /n/ halafu ndipo

tutamke sauti /β/. Hata hivyo kabla ya kwanza kutamka /β/ msemaji huwa amejitayarisha kwa sababu tayari anatarajia kuitamka sauti hiyo. Katika hali ya kutarajia huko, matokeo ni kuwa kutamkia obstruenti /β/ hivi kwamba /n/ inabadilika na kuwa [m]. Hapo tunaona vile nasali ya ufizi inaathiriwa na kuwa nasali ya midomo kwa sababu ya abstruanti ya midomo hivi kwamba sauti hizi zinatamkwa kama silabi moja.

Aidha nasali /n/ ya ufizi inabadilika na kuwa ya kaakaa laini [ŋ] kwa sababu ya kuathiriwa mahali pa kutamkia na obstruenti ya kaakaa laini /ɣ/ katika utamkaji wa neno kama vile 'ng'ondi'. Huu pia ni usilimisho mbele. Usilimisho mbele pia tunauona katika utamkaji wa neno kama vile 'njala' ambapo nasali /n/ inabadilika na kuwa ya kaakaa gumu [ɲ ] kwa sababu ya atheri za obstruenti /ɟ/ ya kaakaa gumu.

Mfano mwingine ni katika utamkaji wa neno kama vile 'ndembo' ambapo sauti mbili zinazotamkwa mahali sawia, yaani /n/ na /l/ katika ufizi, mazingara ambayo yanasababisha kubadilika. Sauti ya nasali /n/ haikubadilika kwa sababu sauti ambayo ingerathiri mahali pa kutolewa inatamkwa mahali sawia nayo, yaani katika ufizi.

Kuathiriana huku hutokea kwa mingili ya kupunguza juhudi za kutamka. Ukiangalia muundo wa ndani, inachukua juhudi nyingi zaidi kutamka sauti [n] Kwa-nza halafu sauti inayofuata zikiwa mbalimbali. Ni rahisi zaidi kutamka sauti hizi kama silabi moja jinsi hiyo katika muundo wa nje. Kwa kuziweka sauti hizi kwenye silabi moja, baadhi ya juhudi zilizohitajika hapo awali kutamkia sauti mbili tofauti zimepunguzwa kwa sababu sasa sauti hizi zinatamkwa mahali pamoja. Sheria hii inhusu kiambishi cha ngeli ys 9/10 /N-/, ambacho ndicho kinachobadilika,

$$/\text{N-}/ \longrightarrow \begin{bmatrix} \text{m-} \\ \text{n-} \\ \text{ɲ-} \\ \text{ŋ} \end{bmatrix} \Big/ \;____ \begin{bmatrix} \text{β} \\ \text{l, r} \\ \text{ɣ} \\ \text{j, ɔ, u} \end{bmatrix}$$

## 3.6 SHERIA YA KUIMARIKA KWA SAUTI

Aghalabu sheria hizi huhusu sauti za obstruenti. Sauti za lugha zimepangwa kutoka zile dhaifu hadi zile zenye nguvu. Hivi ni kusema kwamba kuna sauti ambazo huhitaji juhudi nyingi kutamka kuliko zingine [8] kama anavyosema Richard S. Mguku (1999: 82). Kwa kutumia kigezo hicho basi tunaweza kupanga sauti za lugha kama ifuatavyo:-

61

| | |
|---|---|
| 1 | mtuo<br>- ghuna |
| 2 | mtuo<br>ghuna |
| 3 | Kizuiwa - kwamizwa<br>- ghuna |
| 4 | Kikwamizwa<br>- ghuna |
| 5 | Kikwamizwa<br>- ghuna |
| 6 | Nasali<br>- ghuna |
| 7 | Vilainisho<br>- ghuna |
| 8 | Nusu – irabu<br>+ ghuna |
| 9 | Irabu |
| 10 | Ø |

Kulingana na mchoro huo sauti yenye nguvu zaidi ni ile ya 1, na sauti dhaifu zaidi ni ile ya 9. Tunapotamka sauti ya 9. Kwa hivyo ukielekea chini, sauti huwa inadhoofika na unapoelekea juu sauti kuwa inaimarika.

Mifano ya kuimarika kwa sauti katika Kidawida ni katika ngeli nomino ya 9/10 vilevile,

| | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 62 | / N + l ɛ m b ɔ / | ⟶ | [ndɛmbo] | mgomba/migomba |
| | / N + lɛ:/ | ⟶ | [ ndɛ: ] | babake/babaze |
| | / N + lɔ:/ | ⟶ | [ ndɔ:] | mchanga |
| | / N + lazi/ | ⟶ | [ ndazi] | nzima |
| | / N + lɔdɔ/ | ⟶ | [ndɔdɔ] | ndoto |
| | / N + liʃɛni/ | ⟶ | [ ndiʃɛni] | malishoni |

Katika mifano hiyo, kilainisho / l / kinaimarika na kuwa sauti ya mtuo [d]. Tofauti na katika badiliko 3.5, hapa kila kinachobadilika si kiambishi cha ngali bali ni ile sauti inayofuata kiabishi cha ngeli.

63 [+ konsonanti, + mfululizo] ⟶ [- mfululizo] / # [+ nasali]

Mfano mwingine ni:

| | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 64 | / N + rifu / | ⟶ | [ ndifu ] | nono |

ambapo kilainisho /ɣ/ kinaimarika na kuwa sauti ya mtuo [d] katika mazingira yaleyale ya hapo juu. Sheria yake ni

65 [+ konsonanti, + mfululizo] ⟶ [- mfululizo] / # [+ nasali] + —

Tunaweza kujumlisha sheria hizi pamoja,

66 [+ konsonanti, + mfululizo] ⟶ [- mfululizo] / # [+ nasali] ——

Aidha tuna mifano ifuatayo,

| | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 67 | /N + βɔɣa/ | ⟶ | [mbɔɣa] | "mboga" |

| | | |
|---|---|---|
| /N+ βɔɣa/ | [mbande] | kuni |
| /N+ βiʃi/ | [mbiʃɪ] | mpya |
| /N+ βɛŋgɔ/ | [mbeŋgɔ] | pembe |

Mifano hiyo inaonyesha kuimarika kwa kikwamizwa /β/ inayokuwa sauti ya mtuo [b].

68 $$\begin{bmatrix} +\text{konsonanti} \\ +\text{mfululizo} \end{bmatrix} \rightarrow \begin{bmatrix} -\text{mfululizo} \end{bmatrix} \Big/ \ \# \begin{bmatrix} +\text{nasali} \end{bmatrix} + \ ____$$

Hali kadhalika sauti ya kikwamizwa /ɣ/ huimarika na kuwa ya mtuo [g], kwa mfano,

| | | | **Maana** |
|---|---|---|---|
| 69 | /N + ɣuku/ ⟶ | [nguku] | kuku |
| | /N + ɣuβɛ/ ⟶ | [ŋguβɛ] | nguruwe |
| | /N + ɣada/ ⟶ | [ŋgada] | kata |
| | /N + ɣɔlɔ/ ⟶ | [ŋgɔlɔ] | moyo |
| | /N + ɣanda/ ⟶ | [ŋganda] | udongo |

Sheria,

70 $$\begin{bmatrix} +\text{konsonanti} \\ +\text{mfululizo} \end{bmatrix} \rightarrow \begin{bmatrix} -\text{mfululizo} \end{bmatrix} \Big/ \ \# \begin{bmatrix} +\text{nasali} \end{bmatrix} + \ ____$$

Kwa muhtasari tunaweza kutoa sheria moja ya jumla ya kuimarika kwa sauti,

$$\left/\!\!\left/ \begin{matrix} l/r \\ \beta \\ ɣ \end{matrix} \right/\!\!\right/ \longrightarrow \begin{bmatrix} d \\ b \\ g \end{bmatrix} \Big/ \ \# \quad N \ ____$$

Sheria,

$$\begin{bmatrix} +\text{konsonanti} \\ +\text{mfululizo} \end{bmatrix} \rightarrow \begin{bmatrix} -\text{mfululizo} \end{bmatrix} \Big/ \ \# \begin{bmatrix} +\text{nasali} \end{bmatrix} + \ ____$$

## 3.7 HITIMISHO

Tumeratibu mabadiliko ya kifonolojia kama yanavyotokea katika Kidawida. Tunapata kwamba mabadiliko yanayotokea katika lugha hii si haba kwani

kuna badiliko la kudondoshwa kwa irabu, vundaji wa nusu-irabu, ukaakaishaji, mkubaliano wa nasali na kutamkwa kinachofuata, mkubaliano wa irabu, na kumarika kwa sauti.

Tumegundua kwamba nyingi ya mabadiliko hayo ni ya kutarajiwa katika Kidawida.

## TANBIHI

1. J. B. Hooper (1976): An introduction to Natural Generative Phonology. New York Academic Press ix
2. S. A. Schane (1973): "Natural rules in Phonology" katika Robert P. Stockwell na Ronall K. S. Macaulay (wahariri) Linguistic Change and Generative Theory. Bloomington. Indiana University Press. 209.
3. Ibid 202.
4. E. C. Polome (1967): Swahili Language Handbook. Center for Applied Linguistics. 1717 Massachusetts Avenue, N. W, Washington, D. C. 20036.60.
5. S. A. Schane (opp.cit) 209.
6. R. Lass (1984): Phonology: An Introduction to basic concepts. Cambridge University Press, Cambridge. London. New York, New Rochelle. Melbourne. Sydney. 169.
7. S. A. Schane (opp.cit) 207.
8. R. S. Mgullu (1999) : Mtalas wa Isimu. Longhorn Publishers Kenya Limited, Nairobi 82

# SURA YA NNE

## 4.0 UTANGULIZI

Azma yetu kwenye sura hii ni kulinganisha Kiswahili na kidawida kwa kutumia vigezo viwili

Kwanza tutalinganisha mifumo ya fonimu za irabu na konsonauti. Bila shaka lugha hizi zina baadhi ya fonimu ambazo ni sawia. Hata hivyo, pia kila moja ya lugha hizi zina fonimu ambazo hazipatikani kwa lugha hizo zinafanana na ni vipi zinatofautiana kwa kurejelea mifumo yao ya fonimu.

Pili tunataka kulinganisha umbali wa fonimu za lugha hizo mbili kutoka kwa Bantu-mzazi. Kwa mujibu wa Makolm Guthire (1948:20)kile kigezo cha kihistoria kilichotumwa na Carl Meinhof (1932) kuainisha lugha za kibantu, kinaweza kutumiwa kujua lugha zipi zinatoka kwa lugha mama moja[1]. Kutokana na maelezo ya Guthuria tunaweza kusema kwamba lugha zote za Kibantu zina lugha mama moja, yaani Bantu-mzazi. Lugha ya Bantu – mzazi ilipitia mabadiliko baada ya wazungumzaji wake kutawanyika kwa sababu za kijamii.

Carl Meinhof (1932) anasema kwamba sauti zile za Bantu – mzazi zimebadilika katika lugha zilizotokana nayo hivi kwamba sauti fulani katika lugha moja inayotokeza kama sauti nyingine tofauti katika lugha nyingine[2]. Kwa mfano tuangalie lugha mbili za Kidawida na Kisaghalla zinazotumiwa huko Taita – Taveta. Tofauti iliyopo baina ya lugha hizi mbili ni pale ambapo wazungumzaji wa kidawida wanatumia fonimu [ r ] pale ambapo wazungumsaji wa Kisagalla wanatumia fonimu [z] katika baadhi ya maneno, kama vile,


| **Kidawida** | **Kisaghalla** | **Maana** |
|---|---|---|
| [ irikɔ ] | [ izikɔ ] | jiko |
| [ irina ] | [ izina ] | jina |

Kutokana na data hiyo, kifonetiki tunaweza kusema kwamba Kidawida imepitia mabadiliko mengi kuliko Kisaghalla kwa kuzingatia vile viwango vya sauti zenye nguvu zaidi ( mtuo) hadi zile sauit zilizo dhaifu zaidi (irabu), kama tulivyoziorodhesha katika sura ya tatu. Huo ni mfumo kwa Bantu – mzazi.

Katika sura hii, tutajatibu kuonyesha ni kwa kiasi gani lugha za Kiswahili na Kidawida zilivyosongea mbali kutoka kwa Bantu – mzazi tukitumia kigezo cha mifumo yao ya fonimu.

## 4. 1. ULINGANISHI WA FONIMU ZA KISWAHILI NA KIDAWIDA - IRABU.

Katika sura ya pili tuliweza kutoa orodha ya fonimu za Kidawida. Tulipata kwamba lugha hii ina junila ya fonimu za irabu zipatazo saba ambazo ni /a/, /ɛ/ , /e/, /i/, /u/, /o/, na /ɔ/. Tunapozipanga katika jedwali tuna,




Tukitumia sifa banifu, tunaweza kupambanua irabu hizo kama ifuatavyo:-

| i | e | ɛ | a |
|---|---|---|---|
| + silabi | + silabi | + silabi | + silabi |
| + juu | + mkazo | - mkazo | - juu |
| - nyuma | - nyuma | - nyuma | + nyuma |
| - mviringo | - mviringo | - mviringo | - mviringo |

| ɔ | o | u |
|---|---|---|
| + silabi<br>- mkazo<br>+ nyuma<br>+ mviringo | + silabi<br>+ mkazo<br>+ nyuma<br>+ mviringo | + silabi<br>+ juu<br>+ nyuma<br>+ mviringo |

Tunapolinganisha mfumo wa fonimu za Kidawida na za Kiswahili, tunaona kuna kushabihiana na kutofautiana.

Kiswahili na Kidawida zina fonimu za irabu sawia tano ambazo ni /a/, /ɛ/, /i/,/ɔ/ na /u/. Tofauti tunaiona pale ambapo Kidawida kina fonimu zaidi za irabu, yaani /e/ na /o/. Kutokana na data hiyo, Kiswahili kina idadi ndogo ya irabu[3] kikilinganishwa na Kidawida. Kwa hivyo Kiswahili ni moja ya zile Lugha chache za Kibantu zilizo na fonimu tano pekee za irabu chambilecho Malcolm Guthire (1948:45).

## 4.2 ULINGANISHI WA FONIMU ZA KISWAHILI NA KIDAWIDA - KONSONANTI

Kwa upande wa konsonanti, tuligundua katika sura ya pili kuwa Kidawida kina jumla ya fonimu ishirini na tisa za konsonanti.

Tutapambanua fonimu hizo kwa kutumia sifa bainifu. Jumla ya fonimu za mtuo ni 8 zikiwemo,

| P | t | k | b |
|---|---|---|---|
| + konsonanti<br>- mfululizo<br>+ anteria<br>- korono<br>+ ghuna<br>-mkondo hewa nje | + konsonanti<br>- mfululizo<br>+ anteria<br>+ korono<br>+ ghuna | + konsonanti<br>- mfululizo<br>+ anteria<br>+ korono<br>+ ghuna | +konsonanti<br>- mfululizo<br>+ anteria<br>- korono<br>+ ghuna |

| ɓ | d | ɟ | g |
|---|---|---|---|
| + konsonanti | +konsonanti | +konsonanti | + konsonanti |
| - mfululizo | -mfululizo | -mfululizo | - mfululizo |
| + anteria | + anteria | - anteria | - anteria |
| -korono | + korono | + korono | - korono |
| + ghuna | + ghuna | + ghuna | + ghuna |
| - mkondo hewa nje | | | |

Tunapolinganisha konsonanti hizo na za Kidawida, tunapata kuwa Kiswahili kina konsonanti, nazo ni /p/, /t/, /k/, /b/, /d/, /f/ na /g/. Lugha hizi mbili zinatofautiana ka fonimu moja ya kipasuo ndani /ɓ/ ambayo haipo katika Kiswahili, Vikwamizwa vya Kidawida ni 8 Vikiwemo,

| f | s | ʃ | β |
|---|---|---|---|
| + konsonanti | + konsonanti | +konsonanti | + konsonanti |
| + mfululizo | + mfululizo | + mfululizo | + mfululizo |
| + anteria | + anteria | - anteria | + anteria |
| - korono | + korono | + korono | - korono |
| - ghuna | - ghuna | + ghuna | + ghuna |

| v | z | ɣ | h |
|---|---|---|---|
| + konsonanti | + konsonanti | +konsonanti | + konsonanti |
| + mfululizo | + mfululizo | + mfululizo | + mfululizo |
| + anteria | + anteria | + nyuma | + nyuma |
| - korono | + korono | + juu | - juu |
| + ghuna | + ghuna | + ghuna | + ghuna |

Tunapovilinganisha na vikwamizo vya Kiswahili, tunaona kwamba Kiswahili kina idadi kubwa ya vikwamizwa kuliko Kidawida. Lugha hizi mbili zinafanana kwa vikwamizo saba pekee, yaani, /f/, /s/, /ʃ/, /v/, /z/, /ɣ/ na /h/. Tofauti iliyopo baina ya hizi lugha mbili ni pale ambapo Kidawida kina kikwamizwa cha midomo /β/ ambapo hakiko katika Kiswahili. Nacho Kiswahili kina vikwamizwa vitatu /θ/, / / na /x/ ambavyo haviko katika Kidawida. Sababu mojawapo ya kuwepo kwa tofauti hii ni kuwa Kiswaahili ni lugha iliyoathiriwa sana na lugha za kigeni hususan Kiarabu[4]. Tunafahamu kwamba maneno mengi ya Kiswahili yenye konsonanti hizi /θ/, / / na /x/ ni maneno yaliyokopwa kutoka lugha ya Kiarabu, kwa mfano 'thawabu', 'dhahabu' na 'Khasara', chambilecho Edgar C. Polome (1967:37).

Lugha za Kiswahili na Kidawida zina fonimu moja tu ya konsonanti ya kizuiwa – kwamizwa, ambayo ni / tʃ /. Hapa tungependa kumkosoa Richard S.Mgullu (1999:68) anayesema kwamba Kiswahili kina vizuiwa – kwamizwa viwili /tʃ / na /j/[5]. Kama tulivyoshuhudia katika sura ya pili konsonanti /j/ ni ya mtuo wala si ya kizuiwa – kwamizwa. Tukitumia sifa bainifu, lugha hizi mbili zina kizuiwa – kwaminwa kimoja tu,

| tʃ |
|---|
| + konsonanti |
| - mfululizo |
| - anteria |
| + korono |
| - ghuna |

Tukiangalia konsonanti za nasali, Kidawida kina nasali nne sawa na Kiswahili, Nazo ni

| m | n | ɲ | ŋ |
|---|---|---|---|
| + konsonanti | +konsonanti | +konsonanti | + konsonanti |
| - mfululizo | -mfululizo | -mfululizo | - mfululizo |
| + anteria | + anteria | - anteria | - anteria |
| -korono | + korono | + korono | - korono |
| - nasali | + nasali | + nasali | + nasali |

Zaidi yab hayo, kidawida kina fonimu za Konsonanti zilizonasalishwa awali ambazo katika Kiswahili,

| ᵐb | ⁿd | ᶮj | ᵑg |
|---|---|---|---|
| + konsonanti | +konsonanti - | +konsonanti | + konsonanti |
| - mfululizo | -mfululizo | -mfululizo | - mfululizo |
| + anteria | + anteria | - anteria | - anteria |
| -korono | + korono | + korono | - korono |
| + nasali | + nasali | + nasali | nasali |

Ingawa fonimu aina hii haziko katika Kiswahili sanifu, zinapatikana katika lahaja zingine za Kiswahili kama vile Chi – chifundi, Kivumba, Kimvita, Chijomvu, Kiamu, Kitikuu na Kisiyu, kwa mintarafu ya Mohamed Bakeri (1982). Hii ni sifa mojawapo ya lugha za Kibantu kama vile Kitharaka, Kikikuyu, Kimeru, Kiambu, Kimbeere na Kikamba tunapata fonimu hizi kama alivyouorodhesha Kithaka wa Mberia (1981), Kumbatana na kauli hiyo, basi tunaweza kusema kwamba Kiswahili sanifu ambayo pia ni lahaja ya Kibantu, hapo awali kilikuwa na fonimu za nasali-konsonanti halafu hatimaye fonimu hizo zikapotea labda kwa sababu ya athari za lugha za kigeni.

Vilainisha ni vya aina mbili katika Kiswahili na Kidawida. Tuna kitabaza na Kimadende kama wanavyoviita Tulu (1990)

| l | r |
|---|---|
| + konsonanti | + konsonanti |
| + mfululizo | + mfululizo |
| + anteria | + anteria |
| + korono | + korono |
| + latero | - latero |

Mwisho tuna fonimu za nusu – irabu ambazo katika Kidawida ni mbili sawa na Kiswahili,

| w | j |
|---|---|
| - konsonanti | - konsonanti |
| - silabi | - silabi |
| + nyuma | - nyuma |

## 4.3 HITIMISHO

Kwa kuhitimisha tutasema kwamba lugha hizi mbili zina mshabaha mkubwa kuliko tofauti iliyoko baina yao. Tutatumia takwimu kuthibitisha kauli hiyo kama ifuatavyo:-

| FONIMU | MSHABAHA | TOFAUTI | JUMLA |
|---|---|---|---|
| Mtuo | 7 | 1 | 8 |
| Vikwamizwa | 7 | 4 | 11 |
| Kizuiwa – kwamizwa | 1 | - | 1 |
| Nasali | 4 | - | 4 |
| Nasali - konsonanti | - | 4 | 4 |
| Vilainisho | 2 | - | 2 |
| Nusu – irabu | 2 | - | 2 |
| irabu | 5 | 2 | 7 |
| | 28 | 11 | 29 |

Matokeo haya yanatuambia kuwa asilimia kubwa ya fonimu hizo zinafanana kuliko kutofautiana:-

Kufanana:

$$\frac{28}{39} \times 100 = \frac{2800}{39} = 73.58 = 74\ \%$$

Tofauti

$$\frac{11}{39} \times 100 = \frac{1100}{39} = 25.64 = 26\ \%$$

Matokeo haya yanathibitisha nadhari tete ya kwanza inayosema kuwa fonimu nyingi zinazopatikana katika lugha zote mbili zinafanana na tofauti iliyopo baina yao ni finyu.

## 4. 4 ULINGANISHI WA FONIMU ZA KISWAHILI NA KIDAWIDA KUTOKA KWA BANTU - MZAZI

### UTANGULIZI

Tunaazimia kuchunguza umbali uliopo baina ya fonimu za Kiswahili na Kidawida kutoka kwa Bantu – mzazi. Katika sehemu ya pili ya sura hii.

Kama inavyoaminiwa na wengi, lugha zote za Kibantu zilizaliwa na lugha mama moja, yaani Bantu-mzazi. Kulingana na historia lugha hii baadaye ilitawanyika na hatimaye 'kuzaa' lugha ya Bantu –mzazi ilikuwa ikitumika katika eneo la kaskazini – magharibi mwa Nigeria mnamo miaka elfu mbili iliyopita. Mtawanyiko kutoka eneo hilo ulianzia na watu wakaelekea sehemu tofautitofauti kama vile sehemu za Congo , katika maeneo ya maziwa ya Afrika Mashariki , na hata sehemu za kusini mwa bara la Afrika,wakiwa wanatafuta ardhi zaidi , chakula na maji kwa ajili yao na mifugo yao.

Watu walivyoendelea kutawanyika , lugha ya Bantu –mzazi nayo ikawa inabadilika kadiri walivyoachana kijiografia na kimapisi. Hivi leo , familia ya lugha za kibantu ndio kubwa zaidi barani Afrika ikilinganishwa na familia zingine za lugha ya, Si ajabu basi Mlcom Guthire (1948:7) alisema familia ya kibantu ni kubwa sana hapa barani, kwa kuzingatia kigezo cha kiisimu sio kiethnolojia.

Kwa kulinganisha mifumo ya fonimu za Kiswahili na Kidawida kwa upande mmoja na za Bantu- mzazi kwa upande wa pili tutaweza kujua ni lugha ipi kati ya hizo mbili iliyosongea mbali na Bantu –mzazi kuliko nyingine, na kwa kiasi gani.

## 4. 5 FONIMU ZA BANTU – MZAZI DHIDI YA FONIMU ZA KIDAWIDA NA KISWAHILI

Carl Meinhof (1932) ametoa orodha ya jumla ya fonimu za Bantu-mzazi.

Akianza na fonimu za irabu, meinhof anasema kwamba Bantu –mzazi ilikuwa na irabu msingi tatu ambazo ni /a/, /i/ na /v/, irabu hizi, Meinhof anasisitiza kuwaa zingali katika lugha nyingi za Kibantu hivi leo.

Mbali na irabu msingi, pia meinhof ameorodhesha zile anazosema ni irabu zilizotokana na kuungana kwa irabu msingi; nazo ni /e̱/ na /o̱/.

Kisha tuna irabu finye katika Bantu – mzazi ambazo ni /î/ na /û/. Kwa hivyo jumla ya irabu za Bantu-mzazi ni Saba,

a (Mpangilio hii ni wa
e̱ o̱ Carl Meinhof mwenyewe)

i î û u

Tunaona mshabaha na tofauti mbalimbali kati ya irabu za Kidawida na Bantu-mzazi. Kwa mfano irabu tano zinapatikana katika Bantu-mzazi na Kidawida ambazo ni /a/, /ɛ/* /i/, /ɔ/* na /u/. Tofauti kati yao ni kwa Kidawida kina irabu /e/ na /o/ ambazo hazipo katika Bantu-mzazi. Tena Bantu-mzazi ina irabu /ı/ na /v/ ambazo haziko katika Kidawida.

| **Bantu – mzazi** | | | | **Kidawida** | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | a | | î | u |
| | e̱ | | o̱ | e | o |
| | | | | ɛ | ɔ |
| i | î | û | u | a | |

*/ɛ/ na */ɔ/ ni sawa na /e̱/ na /o̱/ za Bantu-mzazi

Data hiyo inaonyesha kuwa lugha ya Kidawida haikuwahi kuwa na irabu finye (î) na /û/ zilizokuwa katika Bantu-mzazi. Pamoja na hapo irabu zaidi zimeonyezeka katika Kidawida, yaani /e/ na /o/ ambazo hazikuwepo katiika Bantu-mzazi. Huku baadhi ya irabu zinapotea, zingine zinaongezeka katika Kidawida.

Tofauti kati ya Bantu-mzazi na Kidawida si kubwa sana kwa sababu Kidawida si kubwa sana kwa sababu Kidawida kingali kinahifadhi irabu za Bantu-mzazi isipokuwa zile finye. Bantu –mzazi na Kidawida zina jumla ya irabu saba kila moja.

Tukiangalua Kiswahili, tunapata kwamba kinafanana na Bantu-mzazi kwa irabu tano /a/, /ɛ/, /i/, /ɔ/, na /v/. Tofauti kati ya Kiswahili na Bantu-mzazi ni pale ambapo Kiswahili hakina zile irabu finye /î/ na /û/.

| **Bantu –mzazi** | | | | **Kiswahili** | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | a | | i | u |
| | e̱ | | o̱ | ɛ | ɔ |
| i | î | û | u | a | |

Tunaona kwamba vilevile Kiswahili hakikuwahi kuwa na irfabu finye za Bantu-mzazi. Aidha Kiswahili hakikuongeza irabu zaidi, ndiposa kinabaki kuwa na irabu tano pokee.

Tukilinganisha Kiswahili na Kidawida, tunaona kuwa Kiswahili inakaribiana zaidi na Bantu-mzazi kuliko Kidawida. Tunasema hivi kwa sababu mbali na kutokuwa na zile irabu finye, iraba zote za Kiswahili zinawiana na zile za Bantu-mzazi.

Bantu – mzazi vilevile ilikuwa na fonimu za konsonanti chambilecho Carl Meinhof (1932). Kwanza Meinhof anasema kuna vipasuo vya msingi ambavyo ni vitatu vikiwemo /k/, /t/ na /p/.

Pamoja na hayo, Meinhof anasema Bantu-mzazi ina fonimu za vikwamizwa vya kimsingi ambavyo ni /ɣ/, /l/ na /β/.

Aidha Bantu – mzazi ilikuwa na fonimu za kaakaa gumu, yaani /k̲/ na /t̲/ ambazo kwa mujibu wa Meinhof zimetokana na atheri ya irabu /i/ ya kaakaa gumu kwa vipasuo vya kimsingi /k/ na /t/. Fonimu hizi hazina sifa ya ughuna.

Bantu-mzazi pia ilikuwa na fonimu za fonimu za kaakaa gumu, /ɣ̲/ na /l/ ambazo pia zimetokana na athari ya irabu kwa vikwamizwa vya kimsingi /ɣ/ na /l/. Hizi zina sifa ya ughuna.

Pamoja na hayo Bantu-mzazi ilikuwa na fonimu za nasali mbili, /n/ na /m/. Hali kadhalika Bantu-mzazi ilikuwa na fonimu mbili tu za nusu-irabu. Kwa mujibu wa Carl Meinhof (1932) nusu-irabu hizi zinatokana na irabu msingi /i/ na /u/ hivi kwamba /i/ inabadilika na kuwa/j/ ihali /u/ inabadilika na kuwa /w/. Menhof anaeleza kuwa mabadiliko hayo hutokea kwa sababu wakati wa utamkaji wa irabu msingi /i/ na /u/ kunywa huwa kimebanwa kiasi cha kuweza kuleta mabadiliko hayo, tofauti na wakati wa utamkaji wa irabu msingi/a/ ambapo kunywa aghalabu huwa hakibanwi.

Jumla ya fonimu za konsonati za Bantu –mzazi ni kumi na nne chambilecho Carl Meinhof (1932).

| | Vipasuo | Vikwamizwa | Nasali | Nusu-irabu |
|---|---|---|---|---|
| | k | ɣ | (n') | |
| | t | l | n | m |
| Fonimu zilizo | p | β | m | w |
| Kaakaishwa na | k̠ | ɣ̠ | | |
| Athari za irabu | t̠ | l̠ | | |

| AINA ZA KONSONANTI | midomo | midomo + meno | meno | meno + ufizi | ufizi | Kaakaa gumu | Kaakaa laini | Glota | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mtuo | P, ɓ, b | | | | t, d | ɟ | k, g | | 8 |
| Vikwamizwa | β | | | ʃ | s, z | ɣ | h | | 8 |
| Vizuiwa – kwam | | | | | | tʃ | | | 1 |
| Nasali | m | | | | n | ɲ | ŋ | | 4 |
| Nasali –kons | ᵐb | | | | ⁿd | ᶮɟ | ᵑg | | 4 |
| Kitambaza | | | | | l | | | | 1 |
| Kimadende | | | | | ɾ | | | | 1 |
| Nuru - irabu | w | | | | | j | | | 2 |
| | | | | | | | | | 29 |

Tunapolinganisha fonimu za konsonanti za Bantu-mzazi na kidawida tunapata tofauti kubwa sana, kwanza kabisa tuzingatie fonimu zilizo katika lugha zote mbili. Lugha ya kidawida ina nyingi ya fonimu zilizokuwa kwenye Bantu-mzazi. Tukirejelea jedwali la konsonanti za kidawida, tunaona kuwa fonimu zake zinazofanana na za Bantu-

mzazi ni /k/, /t/, /p/, /ɓ/, /l/, /β/, /n/,/m/,/tʃ/,/j/ na /w/. Fonimu ambazo haziko katika Kidawida ni /t/,/ʎ/ , na /l/.

Kulingana na majedwali yetu ya Kidawida na Bantu- mzazi, ni dhaluri kuwa Kidawida kina fonimu nyingi za konsonanti kuliko Bantu-mzazi. Pamoja na kuwa Kidawida kinaehifidhi fonimu za konsonanti za ziada zisizokuwa katika Bantu-mzazi.

Aidha, tunapata ufahamu kutoka kwa majedwali hayo kwamba, fonimu za Kidawida zimepitia mabadiliko ya kifonolojia hasa kudhoofika kwa sauti. Kwa mfano Kidawida kina fonimu za mtuo zenye sifa ya mghuno /ɓ/, /b/, /d/ na /g/ ambazo hazikuweko katika Bantu-mzazi. Inawezekana kuwa fonimu hizi zimetokana na kudhoofika kwa fonimu za mtuo za Bantu-mzazi /p/, /t/ na /k/ kwa sababu ya athari za irabu.

Kidawida pia kimeongeza fonimu zake za vikwamizwa, kimadende, nasali za kaakaa na konsonanti-nasali ambazo hazikuweko katika Bantu-mzazi. Tukitumia takwimu tunapata kuwa kidawida kimesongea mbali kutoka kwa Bantu-mzazi.

<u>Mshabaha</u>

Zinafanana kwa fonimu 11pekee.
*/tʃ / ni sawa na /k/ ya Bantu- mzazi.

11 x 25 = 275 = 34:12 = 34 %
~~32~~ 8
8

<u>Tofauti</u>

Zinatofautiana kwa fonimu 21
21 x 100 = 525 = 6.5.62 ≈ 66%
~~32~~ 8
8

Kidawida inatofautiana na Bantu –mzazi kwa kiasi kikubwa tukiangalia mfumo wao wa fonimu za konsonanti. Hata hivyo tukiangalia zile fonimu za Bantu-mzazi, zote zimehifadhiliwa na kidawida isipokuwa tatu. Tunachoweza kusema ni kwamba, pamoja na kuwa kidawida kimehifadhi fonimu za Bantu-mzazi, vilevile kimeweza kupanua mfumo wake wa fonimu za konsonanti.

Tuangalie kiswahili kwa kukilinganisha na Bantu-mzazi.

KISWAHILI

| AINA ZA KONSONANTI | midomo | Mdomo + meno | meno | Meno + ufizi | ufizi | Kaakaa gumu | Kaakaa laini | glota | jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mtuo | p, b | | | | t,d | j | k,g | | 7 |
| Vikwamizwa | | f, v | θ, ð | | s, z | | x, ɣ | h | 10 |
| Vizuiwa – kwam. | | | | | | tʃ | | | 1 |
| Nasali | m | | | | n | ɲ | ŋ | | 4 |
| Nasali-konsonati | | | | | | | | | - |
| Kitambaza | | | | | l | | | | 1 |
| Kimadende | | | | | r | | | | 1 |
| Nusu- irabu | w | | | | | j | | | 2 |
| | | | | | | | | | 26 |

Kulingana na jadwali hilo, kiswahili pia imehifadhi fonimu nyingi za Bantu-mzazi isipokuwa nne, nazo ni /β/, /t̠/, /ɣ̠/ na /l/. Pamoja na hayo kiswahili pia kimepanwa mfumo wake wa fonimu za konsonanti.

Jedwali hilo linatuarifu kwamba kiswahili hakikuwahi kuwa na fonimu nne za Bantu-mzazi. Aidha sauti za mtuo za Bantu-mzazi zimedhoofika na kuwa na sifa ya mghuno katika kiswahili. Kiswahili vilevile kina fonimu za ziada ambazo hazikuweko katika Bantu-mzazi,zikiwemo vikwamizwa,nasali za kaakaa na kimadande.

Tukitumia takwimu, matokeo ni kuwa Kiswahili kimesongea mbali na Bantu-mzazi.

Mshabaha
Zimefanana kwa fonimu 10 pekee.

$$\frac{10 \times 100}{30} = \frac{100}{3} = 33.3 \approx 33\%$$

Tofauti
Zimetofautiana kwa fonimu 20

$$\frac{20 \times 100}{30} = \frac{200}{3} = 66.6 \approx 67\%$$

Kiswahili kimetofautiana na Bantu-mzazi kwa kiasi kikubwa tunapozingatia idadi ya fonimu zake za konsonanti. Hata hivyo Kiswahili kimehifadhi nyingi ya fonimu za Bantu-mzazi. Pamoja na hayo kiswahili kimepanua mfumo wake wa fonimu za konsonanti.

## 4. 6 HITIMISHO

Tukilinganisha kiswahili na Kidawida, tunapata kwamba Kiswahili ndicho kiko mbali zaidi na Bantu-mzazi kuliko Kidawida. Ni dhahiri kwamba Kiswahili kimepitia mabadiliko mengi kikilinganishwa Kidawida.

Matokeo haya yanakanusha nadharia tete ya pili iliyosema kwmba fonimu za kidawida ndizo zimesongea na kuwa mbali zaidi na fonimu za Bantu-mzazi kuliko fonimu za kiswahili.

## TANBIHI

1. Malcolm Guthrie (1948), The classification of the Bantu languages. London, International African Institute/Oxford University Press. 20.

2. Carl MEINHOF, (1932), Introduction to the phonology of the Bantu Languages. Dietrich Reimer/ Ernst Vohsen/Berlin

3. Malcolm Guthrie (opp cit) 45.

4. Edgar C. Polome (1967), Swahili language Handbook. Center for Applied Linguistics, 1717 Massachusetts Avenue, N.W, Washington, D.C 20036. 37

5. Richard S.Mgullu (1999), Mtalaa wa Isimu Longhorn Publishers (Kenya) Limited, Nairobi. 68

# SURA YA TANO

## 5.0 UTANGULIZI

Katika sura hii tutalinganisha mabadiliko ya kifonolojia yanayotokea katika Kiswahili na Kidawida.

Tulishughulikia mabadiliko ya kifonolojia katika Kidawida kwenye sura ya tatu. Tunayalinganisha mabadiliko hayo na yale yanayotokea katika Kiswahili kwa kurejelea mambo mawili.

Kwanza tunataka kulinganisha motisha ya mabadiliko ya kifonolojia katika Kiswahili na kidawida. Mabadiliko ya kifonolojia yanaweza kuwa sawia katika lugha mbili au zaidi lakini motisha iwe tofauti. Vivyohivyo mabadiliko ya kifonolojia ya lugha au zaidi yanaweza kufanana kabisa pamoja na motisha.

Motisha ni ule msukumo sababu au mazingira ama ya kifonetiki kimofolojia kisintaksia au kisemantiki, ambayo hupelekea kwa sauti fulani kubadilika katika neno. Badiliko la kifonolojia linaweza kuwa ama la kutarajiwa au la, kutegemea motisha. Kwa mfano ile mifanyiko ya kifonoljia asilia ni ya kutarajiwa kwa sababu motisha aghalabu inahusiana na masuala ya kifonetiki. Motisha hizo ni kama vile kanuni za muundo mwafaka wa silabi, kanuni za uwiano na kanuni za kutengana kwa sauti mbali iwezekanavyo. Kanuni hizi zinahusisha masuala ya kifonetiki hasa zile ala za matmshi pamoja na utamkaji wa vpashio. Kwa sababu hiyo lugha nyingi ulimwenguni.

Tukirudi kwa msingi wa nadharia yetu, yaani fonolojia zalishi asilia tutapata baadhi ya kanuni zake zinazohusu mabadiliko kutarajiwa. Mfano ni kanuni za kifonetiki ambazo huhusu kanuni bia za kifonolojia. Kanuni hizi hutkea katika lugha nyingi za ulimwengu ndiposa zinaitwa kanuni bia chabilecho Joan B. Hooper (1976).

Mabadiliko mengine ya kifonolojia si ya kutarajiwa. Kwa mfano tuna kanuni za kimofofonolojia katika msingi wa nadharia ya utafiti huu ambao ingawa unahusisha kanuni za kifonolojia ni mazingira ya kimofolojia au kisintaksia ambayo huamua kutekelezwa kwa mabadiliko hayo kwani mazingira hayo yanahusu lugha maalum .

Pili tunataka kulinganisha peo za mabadiliko ya kifonolojia katika Kiswahili na Kidawida, Mabadiliko ya kifonolojia yanaweza pia kufanana katika lugha mbili au zaidi lakini upeo wa sheria ukatofautiana. Hivi ni kusema kwamba Mabadiliko fulani la kifonoljia linaweza kuathiri sauti za kategoria maalum fulani katika lugha moja na sauti za kategoria maalum fulani katika lugha ya pili. Kwa majibu wa Larry Hyman (1975:139) sauti zilizo katika kategoria maalum huwa za sifa zifuatazo.

a) Vipashio hivyo hupitia sheria sawia za kifonolojia.
b) Vipashio hivyo hufanya kazi pamoja katika mazingira ya sheria za kifonolojia
c) Kipashio kimojawapo hubadilika na kuwa chenzake kupitia sheria ya kifonolojia
d) Kipashio kimojawapo huzaliwa katika mazingira ya kupashio kingine

Tutazingatia zaidi kipengele cha (a) kinachoshikilia kwamba vipashio vilivyo katika kategoria maalum hupitia sheria sawia za kifonolojia. Kwa kuwa zinapitia sheria za kifonolojia zilizo sawia, basi vipashio hivyo viko katika upeo mmoja wa sheria. Kwa mfano katika Kiswahili tuna mabadiliko la kifonolojia la kuimarika kwa sauti. Badiliko hili huhusu vipashio vya likwidi /l/ na /r/ vinavyobakilika na kuwa /d/.

1. $$\left\{ \begin{matrix} l \\ r \end{matrix} \right\} \longrightarrow [d] \ / \ N -$$

kulingana na Larry Hyman (1975) basi vipashio hivi /l/ na /r/ vipo katika kategoria maalum moja. Kwa sababu hiyo vipashio hivyo pia vinakuwa katika upeo mmoja wa sheria ya kuimarika kwa sauti katika Kiswahili. Kwa kurejelea mabadiliko ya kifonolojia ya sura ya tatu tutalinganisha peo za sheria za Kiswahili na Kidawida.

## 5.1 ULINGANISHI WA MOTISHA KATIKA KISWAHILI NA KIDAWIDA

Tutajikita katika mifanyiko ya kifonolojia ifuatayo:-

(a) kudondoshwa kwa irabu
(b) kuundwa kwa nusu - irabu
(c) ukaakaishaji
(d) mkubaliano wa irabu
(e) mkubaliano wa nasali na kitamkwa kinachofuata
(f) kuimarika kwa sauti

## 5.2 KUDONDOSHWA KWA IRABU

Tulivyoshuhudia hapo awali irabu hudondolewa inapotokea katika mazingira mawili tofauti katika Kidawida. Kwanza tuliona kuwa irabi /u/ ya kambishi cha ngeli 1,3 {mu-} ya Kidawida ikidondoshwa pale kiambishi hicho kinapoambishwa mzizi wa nomino ulianza kwa konsonanti kwa mfano,

**Kidawida**

| | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 1. | /mu + ndu/ → | [m + ndu] → [m + ndu] → [mndu] | | mtu |
| 3. | /mu + di/ → | [m + ndi] → [m +ndi] → [mdi] | | mti |

Mifano ifuatavyo inatoa ushahidi kuwa irabu hiyo /u/ inapatikana katika kiwango cha matamshi.

| | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 3. | 1. | /mu + tʃi/ ——— | [mutʃi ] | mtu ambaye si mwenyeji |
| | 3 | /mu + indi/ ——— | [muindi] | mguu |
| | | /mu + mbi ——— | [mumbi] | mwili |
| | | /mu + fu/ ——— | [mufu] | |

Kiswahili

4 1. /mu + kɛ/ ——→ [m + kɛ] → [m + kɛ] → [mkɛ]
3. /mu + ji/ ——→ [m + ji] → [m + ji] → [mji]

Vile vile Kiswahili kina mifano ya maneno yenye irabu /u/ katika cha matamshi.

5. 1. /mu + ungwana/ ——— [Muungwana]
/mu + umba/ ——— [Muumba]
/mu + ujiza/ ——— [Muujiza]
/mu + undɔ/ ——— [muundɔ]

Tukiangalia muundo wa ndani wa data hiyo tunapata kwamba hakuna mazingira yoyote ya kifonetiki yaliyosababisha irabu hiyo kidondoshwa. Miundo ya ndani ya maneno hayo inaonyesha miundo mwafaka ya silabi kama vile KVKKV na KVKV. Ikiwa muundo wa silabi wa maneno hayo ni mwafaka, basi hakuna sababu nyingine inayoweza kuchochea kuondolewa kwa irabu hiyo. Mara nyingi irabu hudondolewa katika mazingira ya mfuatano wa irabu mbili au zaidi lakini mazingira hayo hayako katika mifano yetu hapo juu. Tunachoweza kusema ni kwamba badiliko hilo ni la kihistoria kwani limetokea tu katika mapisi ya wakati. Ufafiti zaidi unalutaji kufanywa ili kuweza kujua sababu za badiliko hilo kutokea. Roger Lass (1984: 196) anasema:

> "Sheria zanye motisha ya kifonetki kwa jumla hutambuliwa kama sheria za Kutarajiwa ilhali zile zilizokuwa na motisha si sheria za kutarajiwa"[3]

Kuambatana na Roger Lass (1984) hatutakosea kusema kwamba ile sheria ya kufutiliwa mbali kwa irabu /u/ si ya kutarajiwa bali ni kubadiliko la kihistroia tu kama invyotokea katika lugha ya Kiswahili na Kidawida.

Irabu pia hudondolewa katika mazingira ya kupakana na irabu nyingine. Badiliko hili hutokea katika Kiswahili na Kidawida kwa mfano.

**Kiswahili**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 6 | 1. | /Wa + anafunzi/ | ⟶ | [wanafunzi] |
| | | /Wa + alimu/ | ⟶ | [walimu] |
| | 5. | /ji + ambɔ/ | ⟶ | [jambo] |
| | | /ji + ɛma/ | ⟶ | [jɛma] |

Hata hivyo badiliko hili halitokei katika nomino zilizoundwa kutokana na vitenzi, kama vile,

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 7 | 2. | /Wa + aʃi/ | —— | [Wa:ʃi] |

**Kidawida**

| | | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|---|
| 8 | 2 | /βa + ana / | ⟶ | [βana] | watoto |
| | | /βa + ai/ | ⟶ | [βai] | wasichana |
| | | / βa + ɔsɛ/ | ⟶ | [βɔsɛ] | wote |
| | | /ji + apɔ/ | ⟶ | [japɔ] | langu |

Vilevile badiliko hili katika Kiawida halitokei katika nomino zilizoundwa kutokana na vitenzi, kama vile,

| | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 9 | 2 | /βa + aʏi/ | [βaiʏI] | "wajenzi" |

Badiliko hili limetokea kwa sababu ya mfuatano wa irabu mbili katika neno. Ili kupata ule muundo mwafaka wa silabi, inabidi mojawapo ya irabu hizo kufutiliwa mbali na hivyo basi kupunguza juhudi za kutamka. Kwa sababu hiyo motisha ya badiliko hilo ni kupata muundo mwafaka wa silabi katika maneno hayo. Hivyo basi badiliko hilo ni la kutarajiwa.

Kufutiliwa mbali kwa irabu pia kunajitokeza katika muktadha tofauti wa mvutano wa irabu. Hapa huwa kuna irabu mbili zilizopakana ambazo huathiriana

na hatimaye tunapata matokea ya irabu moja kudondolewa, Badiliko hili linatokea katika Kiswahili na Kidawida.

10 **Kiswahili**

| | | | 1 | | 2 | | 3 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 6 | /ma + inɔ/ | → | [maɛnɔ] | → | [mɛɛnɔ] | → | [mɛnɔ] |
| | /ma + ikɔ/ | → | [maɛkɔ] | → | [maɛkɔ] | → | [mɛkɔ] |
| 2 | /Wa + ɔtɛ/ | → | [Waɔɔtɛ] | → | [Wɔtɛ] | | |
| | /Wa + iŋgi/ | → | [Waɛŋgi] | → | [Wɛɛŋgi] | → | [Wɛŋgi] |
| 17 | /ku + ɔtɛ/ | → | [kuɔɔtɛ] | → | [kɔtɛ] | | |
| 16 | /pa + iŋgi/ | → | [paɛŋgi] | → | [pɛɛŋgi] | → | [pɛŋgi] |

**Kidawida**

| | | | | | | | | | **Maana** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 11 | 2. | /βa + iŋgi/ | → | [βaɛŋgi] | → | [βɛɛŋgi] | → | [βɛŋgi] | wengi |
| | | /βa + ikɔ/ | → | [βaɛkɔ] | → | [βɛɛkɔ] | → | [βɛkɔ] | wako mahali |
| | 5. | /sa + iji/ | → | [saɛji] | → | [sɛɛji] | → | [sɛji] | jinsi |
| | 2. | /na + isi/ | → | [naɛsi] | → | [nɛɛsi] | → | [nɛsi] | nasi |
| | 14. | /βu + ɔβa/ | → | [βɔɔβa] | → | [βɔβa] | | | woga |
| 16 –18 | | /ku + ɔsɛ/ | → | [kɔɔsɛ] | → | [kɔsɛ] | | | kote |

Motisha ya mabadiliko yanayotokea katika data hiyo ni sheria ya uwiano pamoja na na muundo mwafaka wa silabi.

Katika hatua ya 1 na 2 sheria ya uwiano ndio inayosababisha badiliko hilo kisha sheria ya muundo mwafaka wa silabi katika hatua ya 3 ikasababisha kufutiliwa mbali kwa irabu, kwa hivyo mabadiliko yanayotokea katika data hiyo ni ya kutarajiwa.

## 5.3 KUUNDWA KWA NUSU – IRABU

Wakati mwingine panapokuwa na mkururo wa irabu nusu –irabu huundwa ili kuvunja mkururo huo. Katika Kiswahili na Kidawida badiliko hili hutokea ambapo nusu – irabu [w] na [j] huundwa:-

**Kiswahili**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 12 | 1 | /mu + ana/ | ⟶ | [mwana] |
| | | /mu + ɛma/ | ⟶ | [mwɛma] |
| | | /mu + ɛusi/ | ⟶ | [mwɛusi] |
| | 3 | /mu + ɛzi/ | ⟶ | [mwɛzi] |
| | | /mu + ɛmbɛ/ | ⟶ | [mwɛmbɛ] |
| | 17 | /ku + ɛtu/ | ⟶ | [kwɛtu] |
| | 4 | /mi + aka/ | ⟶ | [mjaka] |
| | 7 | /vi + akula/ | ⟶ | [vjakula] |
| | | /vi + akɔ/ | ⟶ | [vjakɔ] |
| | 9 | /i + akɔ/ | ⟶ | [j akɔ] |

**Kidawida**

13

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | **Maana** |
| | 1 | /mu + aɣi/ | ⟶ | [mwaɣi] | mjenzi |
| | | /mu + ai/ | ⟶ | [mwai] | msichana |
| | 3 | /mu + ɛŋgɛrɛ/ | ⟶ | [mwɛŋgɛrɛ] | mwangaza |
| | 1 | /u + a + kɛʃɔ/ | ⟶ | [wakɛʃɔ] | jina maalum la mtu |
| | 3 | /ɣu + akɛ/ | ⟶ | [ɣwakɛ] | wake |
| | 11 | /lu + aka/ | ⟶ | [lwaka] | sauti |
| | | /lu + aβɔ/ | ⟶ | [lwaβɔ] | wao |
| | | /ku + akɔ/ | ⟶ | [kwakɔ] | kwako |
| | | /ku + akɛ/ | ⟶ | [kwakɛ] | kwake |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | **Maana** |
| 4, 9 | / i + akɔ/ | ⟶ | [jakɔ] | yako |
| | / i + apɔ/ | ⟶ | [japɔ] | yangu |
| | / i + aβɔ/ | ⟶ | [j aβɔ] | yao |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 8 | /vi + adu/ | ⟶ | [vjadu] ⟶ | [vadu] | viatu |
| | /vi + ala/ | ⟶ | [vjala] ⟶ | [vala] | vidole |
| | /vi + akɔ/ | ⟶ | [vjakɔ] ⟶ | [vjakɔ] | vyako |

Kuambatana na data hiyo, nusu – irabu hizo zimeundwa katika mazingira ya mfuatano wa irabu mbili. Hili ni badiliko linalotokea katika mazingira ya kifonolojia kwa ambavyo motisha ni kwa minajili ya kupata muundo mwafaka wa silabi. Baina ya muundo wa silabi wa KVV na *KGV , muundo unopendelewa

zaidi ni ule wa KGV kwa sababu ni rahisi kutamka kuliko ule wa KVV. Kwa sababu hiyo basi tunasema kuwa badiliko hilo ni la kutarajiwa.

## 5.4 UKAAKAISHAJI

Babadiliko hili hutokea pale ambapo kipashio kinachotamkwa kwingineko hubadilika na kutamkwa kwenya kaakaa gumu. Badiliko hili hutokea katika Kiswahili na Kidawida,

**Kiswahili**

14 7

| | | 1 | 2 | 3 |
|---|---|---|---|---|
| /ki+ akula/ | → | [tʃiakula] → | [tʃjakula] → | [tʃakula] |
| /ki + ɛti/ | → | [tʃiɛti] → | [tʃjɛti] → | [tʃɛti] |
| /ki + ɔmbɔ/ | → | [tʃiɔmbɔ] → | [tʃjɔmbɔ] → | [tʃɔmbɔ] |
| /ki + ɔtɛ/ | → | [tʃiɔtɛ] → | [tʃjɔtɛ] → | [tʃɔtɛ] |
| /ki + aŋgu/ | → | [tʃiaŋgu] → | [tʃjaŋgu] → | [tʃaŋgu] |

**Kidawida**

15
7

| | | | | | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| /ki + ala/ | → | [tʃiala] | → | [tʃjala] | → | [tʃala] | → | " kidole" |
| /ki + arɔ/ | → | [tʃiarɔ] | → | [tʃjarɔ] | → | [tʃarɔ] | → | "kazi" |
| /ki + aŋgu/ | → | [tʃiaŋgu] | → | [tʃjaŋgu] | → | [tʃaŋgu] | → | "fimbo" |
| /ki + apɔ/ | → | [tʃiapɔ] | → | [tʃjapɔ] | → | [tʃapɔ] | → | "changu" |
| /ki + ɔsɛ/ | → | [tʃiɔsɛ] | → | [tʃjɔsɛ] | → | [tʃɔsɛ] | → | "chote" |
| /ki + a + sia/ | → | [tʃiasia] | → | [tʃjasia] | → | [tʃasia] | → | "kimeisha" |

Kama tunavyoona katika data hiyo mazingira ya kifonetiki yamechochea badkiliko la kifonolojia la ukaakaishaji KGV inasimamia. Konsonanti nus-irabi , irabu.

Mabadiliko kadha yametokea mabli na ukaakaishaji. Katika hatua ya 1 badiliko la ukaakasishaji limtokea kwa sababu ya kanuni za uwiano. Katika hatua ya pilo nusu irabu inaundwa kwa minajili ya kupata ule muundo mwafaka wa silabi. Hivyo basi hatuna budi kusema kwamba badiliko la ukaakaishaji pamoja na hayo mengine katika data hiyo ni ya kutarajiwa.

## 5.5 MKUBALIANO WA IRABU

Hii ni sheria ya uwiano inayohusu irabu zilizopakana. Katika sheria hii aghalabu irabu ya mzizi wa kitenzi huathiri irabu ya kiambishi kifuatilizi katika vitenzi vya kauli mbalimbali. Haya hutokea katika Kiswahili na Kidawida.

**Kiswahili** **Vitenzi vya Kauli ya Kutendea**

16
/anzi + i + a/ —— [anzia]
/ham + i + a/ —— [hamia]
/imb + i + a/ —— [imbia]
/pig + I + a/ —— [pigia]
/fuŋg + I + a/ —— [fuŋgia]
/tuŋg + I + a/ —— [tuŋgia]

Data hiyo inaonyesha kuwa irabu kaze za mizizi ya vitenzi /a/,/i/ na /u/ zinakubaliana na kiambishi kifuatilizi kase [i] Kiambishi kifuatilizi hiki hakibadiliki katika muundo wa nje. Hii ni kwa sababu irabu zilizo kwenye mizizi ya vitenzi vimeathiri hivi kwamba hakikubadilika. Irabu hizo zimekiathiri kwa kanuni ya uwiano.

17
/Pɛnd + i + a/ ⟶ [Pɛndɛa]
/ɛnd + i + a/ ⟶ [ɛndɛa]
/sɔm + i + a/ ⟶ [sɔmɛa]
/gɔm + i + a/ ⟶ [gɔmɛa]

Data hiyo inaonyesha irabu ya kiambishi kufuatilizi /i/ ikibadilika na kuwa [ɛ] katika muundo wa nje. Badiliko hili linatokea kutokana na athari za irabu hafifu za mizizi ya vitenzi kwenye kiambishi kufuatilizi. Kanuni ya uwiano inaonekana ikifanya kazi ambapo irabu hafifu za mizizi ya vitenzi /ɛ/ na /ɔ/ zinakiathiri kiambishi kufuatilizi hivi kwamba nacho pia kinakuwa hafifu [ɛ].

**Vitenzi vya kauli ya kutendesha**

18 /anz + iʃ + a/ — [anziʃa]
/ham + iʃ + a/ — [hamiʃa]
/imb + iʃ + a/ — [imbiʃa]
/pig + iʃ + a/ — [pigiʃa]
/fuŋg + iʃ + a/ — [fuŋgiʃa]
/tuŋg+ iʃ + a/ — [tuŋgiʃ a]

Katika data hiyo tunaona kuwa kiambishi kifuatilizi /i/ hakibadiliki katika kiwango cha matamshi. kaimbishi kifuatilizi hiki kina irabu kaze [i] ambacho kinakubaliana na irabu kaze za mzizi ya vitenzi hivyo.

19 /Pɛnd + iʃ + a/ ⟶ [Pɛndɛʃa] ⟶ [Pɛndɛza]
/ɛnd + iʃ + a/ ⟶ [ɛndɛʃa]
/sɔm + iʃ + a/ ⟶ [sɔmɛʃa]
/gɔm + iʃ + a/ ⟶ [gɔmɛʃa]

Data hiyo inaonyesha vile irabu /i/ ya kiambishi kufuatilizi kinachobadilika na kuwa [ɛ] katika muundo wa nje. Irabu hii kaze inabadilika na kuwa hafifu [ɛ] kwa sababu ya athari za irabu hafifu zilizo kwenye mizizi ya vitezi hivyo. Hapa tunaona kuwa irabu ya kiambishi kifuatilizi pia inakubaliana na irabu za mzizi ya vitenzi.

**Kauli ya kutendeka**

20 /kat + ik + a/ — [katika]
/sag + ik + a/ — [sagika]
/imb + ik + a/ — [imbika]
/pik + ik + a/ — [pikika]
/fuŋg + ik + a/ — [fuŋgika]
/tuŋg + ik + a/ — [ tuŋgika]

Mifano hiyo vilevile inaonyesha vile irabu ya kiambishi kufuatilizi [i] kinavyokubaliana na irabu za mizizi ya vitenzi kwa sifa ya ukaze. Hii ni aina ya uwiano ambapo irabu za mzizi ya vitenzi zinaiathiri irabu ya

kiambishi kifuatilini. Katika data hivo irabu hiyo haibadiliki katika kiwango cha matamshi.

| | | |
|---|---|---|
| 21 | /Pεnd + ik + a/ → | [Pεndεka] |
| | /kεr + ik+ a/ → | [kεrεka] |
| | /sɔm + ik + a/ → | [sɔmεka] |
| | /tʃɔm + ik + a/ → | [tʃɔmεka] |

Hapa tunaona irabu ya kiambishi kufuatilizi [i] ikibadilika na kuwa [ε]. Tunaona mkubaliano wa irabu kati ya irabu za mizizi ya vitenzi na irabu ya kiambishi kufuatilizi. Irabu hafifu [ɔ] na [ε] za mzizi ya vitenzi huyo vimeathiri irabu ya kiambishi kifuatilizi nayo ikapata sifa ya uhalifu [ε]

**KIDAWIDA** **Vitenzi vya kauli ya kutendea**

| | | | **Maana** |
|---|---|---|---|
| 22 | /ram + i + a/ —— | [ramia] | rukia |
| | /zam + i + a/—— | [zamia] | chukiza |
| | /sεk + i + a/ —— | [sεkia] | chekea |
| | /sεl+ i + a/ —— | [sεlia] | tembelea |
| | /siŋg + i + a/ —— | [siŋgia] | olea utamu |
| | /siɣ + i + a/ —— | [siɣia] | achia |
| | /duk + i + a/ —— | [dukia] | bebea |
| | tʃumb + i + a/ —— | [tʃumbia] | pitia |

Katika data hiyo tunaona mkubaliano wa irabu za mizizi ya vitenzi na kiambishi kifuatilizi. Katika mizizi ya vitenzi tuna irabu /a/, / ε /, /i/ na /u/ zinazokubaliana na irabu ya kiambishi kifuatilizi [i] Tofauti na katika Kiswahili irabu hafifu [ε] ya mzizi wa kitenzi inakubaliana na irabu kaze [i] ya kiambishi kifuatilizi katika Kidawida.

| | | | **Maana** |
|---|---|---|---|
| 23 | /lɔmb + i + a/ | [lɔmbεa] | ambia |
| | /bɔr + i + a/ | [bɔrεa] | imbia |

Data huyo inaonyesha irabu hafifu [ɔ]ya mzizi ya vitenzi inakubaliana na irabu hafifu

[ ɛ ]ya kiambishi kifuatilizi. Irabu ya kiambishi kifuatilizi [i] kinabadilika na kuwa

[ɛ ]kutokana na athari za irabu [ɔ ] ya mzizi ya vitenzi hivyo.

**Vitenzi vya kauli ya kutendesha**

| | | | Maana |
|---|---|---|---|
| 24 | /ram + iʃ + a/ — | [ramiʃa] | rukisha |
| | /zam + iʃ + a/ — | [zamiʃa] | haribu |
| | /siŋg + iʃ + a/ — | [siŋgiʃa] | koleza utamu |
| | /siɣ +iʃ + a/ — | [siɣiʃa] | achisha |
| | /duk + iʃ + a/ — | [dukiʃa/ | bebesha |

Data hiyo inaonyesha mkubaliano wa irabu kaze za mizizi ya vitenzi na irabu kaze ya kiambishi kifuatilizi. Irabu [i] katika kiambishi kifuatilizi kinaelekea kukubaliana na irabu /a/ /i/ na /u/ za mizizi ya vitenzi.

| | | | Maana |
|---|---|---|---|
| 25 | /sɛk + iʃ + a/ ⟶ | [sɛkɛʃa] | chekesha |
| | /sɛl+ iʃ + a/ ⟶ | [sɛlɛʃa] | tembeza |
| | /lɔmb +iʃ + a/ ⟶ | [lɔmbɛʃa] | mbesha |
| | /bɔr + iʃ + a/ ⟶ | [bɔrɛʃa] | imbisha |

Hapo tunaona irabu hafifu ya kiambishi kifuatilizi [ɛ] ikikubaliana na irabu hafifu za mizizi ya vitenzi /ɛ/ na /ɔ /.

Katika mifano hiyo ya Kiswahili na Kidawida tunaona mkubaliano wa irabu ukitokea baina ya irabu za mizizi ya vitenzi na za viambishi vifuatilizi. Badiliko hili linatokea kwa sababu ya kanuni za uwiano ambapo irabu za mizizi ya vitenzi zinaathiri irabu za viambishi vifuatilizi hasa kwa sifa ya ukaze. Badiliko hilo ni la kutarajiwa katika kiswahili na kidawida kwa ambayo motisha yake ni usilimisho au uwiano.

## 5.6 MKUBALIANO WA NASALI NA KITAMKWA KINACHOFUATA

Badiliko hili hutokea hasa pale ambapo kiambishi cha ngeli nomino ya 9/10 {N-} kinapoambishwa kwenye mzizi wa nomino anuwai katika Kiswahili na Kidawida. Kwa mfano.

**Kiswahili**

/N + bɔga/ → [mbɔga]
/N + wili/ → [mbili]
/N + gɔma/ → [ŋgɔma]
/N + gumu/ → [ŋgumu]
/N + jia/ → [ɲjia]
/N + dizi/ → [ndizi]

**Kidawida**

| | | **Maana** |
|---|---|---|
| /N + βoɣɔ/ → | [moboɣɔ] | nyati |
| /N + βɔ βa/ → | [mbɔβa] | shamba |
| /N + ɣɔndi/ → | [ŋgɔndi] | kondoo |
| /N + ɣɔkɔ/ → | [ŋgɔkɔ] | kuku |
| /N + lɛmbɔ/ → | [ndɛmbɔ] | mgomba |
| /N + lazi/ → | [ndazi] | nyingi/nzima |
| /N + ɔni/ → | [ɲɔni] | nyuni |
| /N + jala/ → | [ɲjala] | njaa |

Katika mifano hiyo tunaona sauti ya nasali /N/ ikibadilika na kuwa aina zingine za nasali katika mazingira tofautitofauti ya kifonetiki. Kwa sababu ya mazingira hayo sauti hiyo inaathiriwa mahali pake pa kutamkia na sauti inayoifuata. Hii ina maana kuwa badiliko hilo linatokea kwa sababu ya kanuni za usilimisho ambapo sauti inaathiriwa na nyingine. Hivyo basi badiliko hilo ni la kutarajiwa katika Kiswahili na Kidawida.

## 5.7 KUIMARIKA KWA SAUTI

Katika Kiswahili na Kidawida badiliko la kuimarika kwa sauti linatokea katika baadhi ya vipashio vyao kwa mfano.

**Kiswahili**

| | | |
|---|---|---|
| /N + limi/ | → | [ndimi] |
| /N + lɔa/ | → | [ndɔa] |
| /N + lɔtɔ/ | → | [ndɔtɔ] |
| /N + rɛfu/ | → | [ndɛfu] |
| /N + wili/ | → | [mbili] |

**Kidawida**

| | | | Maana |
|---|---|---|---|
| /N + lɛmbɔ/ | → | [ndɛmbɔ] | mgomba |
| /N + lɛ:/ | → | [ndɛ:] | babake |
| /N + lɔ:/ | → | [ndɔ:] | mchanga |
| /N + lazi/ | → | [ndazi] | nyingi/nzima |
| /N + lɔdɔ/ | → | [ndɔdɔ] | ndoto |
| /N + liʃɛni/ | → | [ndiʃɛni] | malishoni |
| /N+ rifu/ | → | [ndifu] | nono |
| /N + βɔɣa/ | → | [mbɔɣa] | mboga |
| /N + βande/ | → | [mbandɛ] | kuni |
| /N+ βiʃi/ | → | [mβiʃI] | mpya |
| /N + ɣuku/ | → | [ŋguku] | kuku |
| /N + ɣuβɛ/ | → | [ŋguβɛ] | nguruwe |

Data hiyo inaonyesha kuimarika kwa sauti kadha katika Kiswahili na Kidawida. Tunaona sauti za mfululizo zikibadilika na kuwa za mtuo. Badiliko hilo linatokea kwa sababu ya kanuni za usilimisho au uwiano. Sauti hizo za mfululizo zimebadilika na kuwa za mtuo kutokana na athari ya sauti ya mtuo ambayo ni nasali /n/. Kutokana na kaulihiyo ni dhahiri kuwa badiliko hili ni la kutarajiwa vilevile katika lugha hizi mbili.

## 5.8 HITIMISHO

Tumeona kuwa mabadiliko mengi katika Kiswahili na Kidawida ni ya kutarajiwa. Mabadiliko hayo yametokea katika mazingira ya kifonetiki yaliyochochea mabadiliko ya kifonolojia pekee. Motisha katika mabadiliko hayo yanalingana katika Kiswahili na Kidawida. Tunapata kwamba motisha ulikuwa ni za kifonetki

kama vile muundo mwafaka wa silabi, kanuni za usilimisho na kutengana kwa sauti mbali invyowezekana.

Inaonekana mabadiliko ya kifonolojia katika Kidawida ni ya kutarajiwa tu. Katika Kiswahili kuna baadhi ya mabadiliko ambayo si ya kutarajiwa. Kwa mfano kuna badiliko la kudhoofika kwa sauti katika Kiswahili ambayo sauti za mtuo zinabadilika na kuwa za mfululizo kama vile,

**Kiswahili**

30

/mu + ib + i/ → [mwizi]
/mu + fuat + i/ → [mfuasi]
/mu + pɛnd + i/ → [mpenzi]
/mu + andik + i/ → [mfuasi]
/mu + jɛŋg + i/ → [mjɛnzi]

Sheria,

[+ konsonanti, - mfululizo] → [+ mfululizo] / ___ i [konominisha]

Sheria ya badiliko hilo inasema kwa sauti ya mtuo inabadilika na kuwa ya mfululizo ya katika mazingira ya /i/ kuunda nomino kutokana na vitenzi peke yake. Kwa sababu ya mpaka huo tunaona kwamba badiliko hilo sio la kifonetiki bali ni lakimofolojia na kisintaksia. Badiliko hilo ni la kimofolojia kwa sababu linahusu uundaji wa neno kutkana na mzizi wa kitenzi. Pia ni la kisintaksi kwa sababu tunazungmzia kategoria ya maneno nomino. Kutokana na hayo basi chabilecho Joan Hooper (1976), badiliko hilo ni la kimofofonolojia na kwa hivyo si la kutarajiwa[4] Si ajabu hatukeweza kuliona likitokea katika lugha ya Kidawida kwani badiliko la kimofofonolojia huhusu lugha maalum. Licha ya hayo tunona kwamba kuna uwiano mkubwa baina ya kideawida na kiswahili tunapolinganisha kigezo cha motisha. Tunapata kwamba pamoja na kuwa Kiswahili kina badiliko

usilokuwa la kurarajia mabadiliko yake mengi ni ya kutarajiwa sawia na Kidawida.

## 5.9 ULINGANISHI WA UPEO WA SHERIA KATIKA KISWAHILI NA KIDAWIDA

Tukirejelea mabadiliko tuliyoshughulilika katika sehemu ya kwanza ya sura hii tutaangalia peo za sheria za mabadiliko hayo katika Kiswahili na Kidawida.

## 5.10 KUDONDOSHWA KWA IRABU

Kudondoshwa kwa irabu katika Kiswahili na Kidawida kunahusu irau /u/ /a/ na /i/. Irabi hizi yamkini ni zile za viambishi vya ngeli ya 1,2,3, 5, 14 katika Kidawida na 1,3,5,17,18 katika Kiswahili kwa mfano.

Kiswahili

32 /mu + tu/ → [m + tu] → [m̩ + tu] → [m̩tu]
/mu + hindi/ → [m + hindi] → [m̩ + hindi] → [m̩hindi]
/mu + hɔgɔ/ → [m + hɔgɔ] → [m̩ + hɔgɔ] → [m̩hɔgɔ]
/mu + ɔjɔ/ → [m + ɔjɔ] → [m̩ + ɔjɔ] → [mɔjɔ]
/ji +ambɔ/ → [jambɔ]
/ku + ɔtɛ/ → [kɔtɛ]
/mu + ɔtɛ/ → [mɔtɛ

/ha + a + ɛndi/ → [haɛndi]
/ha + u+ piki/ → [ hupiki]

Kidawida

| | | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|---|
| 33 | /mu + ka/ | → [m + ka] | → [m̩ + ka] | → [m̩ka] | mke |
| | /βa + ana/ | → [βana] | | | watoto |
| | /βa + ai/ | → [βai] | | | wasichana |
| | /mu + zi/ | → [m + zi] | → [m̩ + zi] | → [m̩zi] | kijiji |
| | /mu + sigɔ/ | → [m + sigɔ] | → [m̩ + sigɔ] | → [m̩sigɔ] | mzigo |
| | /ji + apɔ/ | → [jiapɔ] | | | langu |

/ɟi + aβɔ/ → [jaβɔ] lao
/βu + ɔβa/ → [βɔβa] woga
/βu + ɔra/ → [βɔri] wazi

Kulingana na data hiyo Kiswahili kinaonekana kuwa na upeo mpana wa sheria kuliko Kidawida. Ingawa irabu zinazodondoshwa ni sawia, katika kiswahili irabu hizi hudondolewa katika mazingira mengi zaidi yaani nomino vitenzi na vivumishi. Kidawida kinadondosha irabu hizi katika nomino na vivumishi peke yake. Hata hivyo upeo wa sheria hii uwiano katika Kidawida na Kiswahili

## 5.11 KUUNDWA KWA NUSU – IRABU

Nusu – Irabu zinaundwa kutokana na irabu /u/ Na /i/. Irabu /u/ ina badilika na kuwa [w] nayo [i] hubadilika na kuwa [j] katika Kiswahili na Kidawida. Badiliko hili hutokea kwenye ngeli nomino ya 1,3,11,13,15,16,17, 18,4,8, 9, za Kidawida badiliko hili hutokea katika mazingira ya ngeli nomino ya 1,3,11 15,17,18 kwa mafano.

**Kiswahili**

34 /mu + ɛnzi/ → [mwenzi]
/mu + alimu/ → [mwalimu]
/mu + aka/ → [mwaka]
/mu + itɔ/ → [mwitɔ]
/u + ajɔ/ → [wajɔ]
/u + ɛma/ → [wɛma]
/ku + ɛnda/ → [kwɛnda]
/ku + ɛmbamba/ → [kwɛmbamba]
/mu + aŋgavu/ → [mwaŋgavu]
/mu + ɛtu/ → [mwɛtu]

/mi + aka/ → [mjaka]
/mi + ɛupɛ/ → [mjɛupɛ]
/vi + uŋgu/ → [vjuŋgu]
/vi + akɔ/ → [vjakɔ]
/i + akɔ/ → [jakɔ]
/i + auŋgu/ → [ja ŋgu]

**Kidawida**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | **Maana** |
| 35 | /mu + aɣi/ | → | [mwa i] | → | mjenzi |
| | /mu + εli/ | → | [mwεli] | → | mtakatifu |
| | /mu + εŋgεrε/ | → | [mwεŋgεrε] | → | mwangaza |
| | /ɣu + akε/ | → | [ɣwakε] | → | wake |
| | /lu + aka/ | → | [lwaka] | → | sauti |
| | /lu + akε/ | → | [lwakε] | → | wake |
| | /tʃu + aka/ | → | [tʃwaka] | → | sauti |
| | /ku + a + βɔna/ | → | [kwaβɔna] | → | umeona |
| | /ku + a + tʃa/ | → | [kwatʃa] | → | umekuja |
| | /ku + akɔ/ | → | [kwakɔ] | → | kwako |
| | /ku + aβɔ/ | → | [kwaβɔ] | → | kwao |
| | /i + apɔ/ | → | [japɔ] | → | yangu |
| | /i + aβɔ/ | → | [jaβɔ] | → | yao |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| /vi + ala/ → | [vjala] → | [vala] → | vidole |
| /vi + ɔrɔ/ → | [vjɔrɔ] → | [vɔrɔ] → | vyoo |
| /vi + apɔ/ → | [vjapɔ] → | [vapɔ] → | vyangu |
| /vi + akɔ/ → | [vjakɔ] → | [vakɔ] → | vyako |

Data yetu inaonyesha kuwa mazingira ya mabadiliko haya katika Kidawida ni mapana kuliko ilivyo katika Kiswahili. Mabadiliko haya yanahusisha nomino, vimilikishi vivumishi na vitenzi katika Kidawida. Katika Kiswahili mabadiliko hili linahusu nomino, vivumishi na vimiliksihi. Pamoja na hayo upeo wa sheria hii unwiano sana baina ya Kiswahili na Kidawida.

## 5.12 UKAAKAISHAJI

Katika Kiswahili na Kidawida, ukaakaishaji hutokea pale ambapo sauti /k/ inabakilika na kuwa [ tʃ ] kwenye ngeli nomino ya 7 kwa mfano.

**Kiswahili**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 36 | /ki + umba/ → | [tʃiumba] → | [tʃjumba] → | [tʃumba] |
| | /ki + ama/ → | [tʃiama] → | [tʃjama] → | [tʃama] |
| | /ki + ɛma/ → | [tʃiɛma] → | [tʃjɛma] → | [tʃɛma] |
| | /ki + ɛusi/ → | [tʃiɛusi] → | [tʃjɛusi] → | [tʃɛusi] |
| | /ki + akɛ/ → | [tʃiakɛ] → | [tʃjakɛ] → | [tʃakɛ] |
| | /ki + aɔ/ → | [tʃiaɔ] → | [tʃjaɔ] → | [tʃaɔ] |

**Kidawida**

| | | | | | Maana |
|---|---|---|---|---|---|
| 37 | /ki + adv/ → | [tʃiadu ] → | [tʃjadu] → | [tʃadu] → | kiatu |
| | /ki + ɔŋgɔ/ → | [tʃiɔŋgɔ] → | [tʃjɔŋgɔ] → | [tʃɔŋgɔ] → | kichwa |
| | /ki + ɛdu/ → | [tʃiɛdu] → | [tʃjɛdu] → | [tʃɛdu] → | chetu |
| | /ki + ɛnu/ → | [tʃiɛnu] → | [tʃjɛnu] → | [tʃɛnu] → | chenu |
| | /ki + ɔsɛ/ → | [tʃiɔsɛ] → | [tʃjɔsɛ] → | [tʃɔsɛ] → | chote |
| | /ki + dua/ → | [tʃidua] → | [tʃjdua] → | [tʃdua] → | kingali kipo |
| | /ki + a + βurwa/ → | [tʃiβurwa] → | [tʃjaβurwa] → | [tʃaβurwa] → | kimeiva |

Kulingana na data hiyo ukaakashaji hutokea kwenye mazingira mapana katika Kidawida kuliko Kiswahili. Tunaona kuwa mbali na nomino, vile vile kuna vimilikishi na vivumishi. Licha ya hayo upeo wa sheia hii. Unalingana katika kiswahili na kidawida, kwa ambayo ni sauti moja tu /k/ inayobadiliki na kuwa [tʃ]

## 5.13 MKUBALIANO WA IRABU

Mkubaliano wa irabu hutokea naina ya irabu ya mizizi ya vitenzi na irabu za viambisi vifuatilizi katika kiswahili na kidawida.

**Kswahili** **Vitenzi vya kauli ya kutenda**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 38 | /amb + i + a/ | — | [ambia] |
| | /amk + i +a/ | — | [amkia] |
| | /tʃinj + i + a/ | | [tʃinjia] |
| | /pit + i + a/ | — | [pitia] |
| | /rud + i + a/ | — | {rudia] |
| | /puŋg + i + a/ | — | [puŋgia] |
| | /sɛm + i + a/ | → | [sɛmɛa] |
| | /mɛg + i + a/ | → | [mɛgɛa] |

/ɛ/ ———————— [ ɛ ]

/ɔ/ ———————— [ ɛ ]

**Kidawida**

/a/ ———————— [ i ]
/ɛ/ ———————— [ i ]
/i/ ———————— [ i ]
/u/ ———————— [ i ]
/ɔ/ ———————— [ ɛ ]

| **Kiswahili** | | **Vitenzi vya kauli ya kutendesha** | | |
|---|---|---|---|---|
| 41 /anz + iʃ + a/ | ———— | [anziʃa] | | |
| /ham + iʃ + a/ | ———— | [hamiʃa] | | |
| /imb + iʃ + a/ | ———— | [imbiʃa] | | |
| /pig + iʃ + a/ | ———— | [pigiʃa] | | |
| /fuŋg + iʃ + a/ | ———— | [fuŋgiʃa] | | |
| /dund + iʃ + a/ | ———— | [dundiʃa] | | |
| /Pɛnd+ iʃ + a/ | ————→ | [Pɛndɛʃa] | ————→ | [Pɛndɛza] |
| /ɛnd+ iʃ + a/ | ————→ | [ɛndɛʃa] | | |
| /sɔm + iʃ + a/ | ————→ | [sɔmɛʃa] | | |
| /gɔm + iʃ + a/ | ————→ | [gɔmɛʃa] | | |

| **Kidawida** | | **Vitenzi vya kauli ya kutenda** | **Maana** |
|---|---|---|---|
| 42 /ram + iʃ + a/ | ———— | [ramiʃa] | rukisha |
| /zam + iʃ + a/ | ———— | [zamiʃa] | haribu |
| /siŋg + iʃ + a/ | ———— | [siŋgiʃa] | koleza utamu |
| /siɤ + iʃ + a/ | ———— | [siɤiʃa] | achisha |
| /duk + iʃ + a/ | ———— | [dukiʃa] | bebesha |
| /sɛk+ iʃ + a/ | ———— | [sɛkɛʃa] | chekesha |
| /sɛl+ iʃ + a/ | ———— | [sɛlɛʃa] | tembeza |
| /lɔmb + iʃ + a/ | ———— | [lɔmbɛʃa] | ombesha |
| /bɔr + iʃ + a/ | ———— | [bɔrɛʃa] | imbisha |

Data hiyo inaonyesha vile irabu kaze za mizizi ya vitenzi inakubaliana na irabu kaze [i] ya kinyambilishi. Tunapoangalia kauli ya kutendesha tunoana kuna uwiano wa upeo wa sheria hii kati ya Kidawida na Kiswahili.

**Kiswahili**

43 **Irabu ya mizizi wa Kitenzi** **Irabu ya Kinyambulishi**

| | | |
|---|---|---|
| /a/ | ———————— | [ iʃ ] |
| /i/ | ———————— | [ iʃ ] |
| /u/ | ———————— | [ iʃ ] |
| /ɛ/ | ———————— | [ ɛʃ ] |
| /ɔ/ | ———————— | [ ɛʃ ] |

**Kidawida**

| | | |
|---|---|---|
| /a/ | ———————— | [ iʃ ] |
| /i/ | ———————— | [ iʃ ] |
| /u/ | ———————— | [ iʃ ] |
| /ɛ/ | ———————— | [ ɛʃ ] |
| /ɔ/ | ———————— | [ ɛʃ ] |

Tunapoangalia vitenzi vy kauli ya kitendeka, Kiswahili ndicho kina vitenzi vya aina hii lakini Kidawida hakina

**Kiswahili** **Vitenzi vya kauli ya kutenda**

| | | |
|---|---|---|
| 44 /kat + ik + a/ | ———————— | [katika] |
| /sag + ik + a/ | ———————— | [sagika] |
| /imb + ik + a/ | ———————— | [imbika] |
| /pik + ik + a/ | ———————— | [pikika] |
| /fuŋg+ ik + a/ | ———————— | [fuŋgika] |
| /tuŋg + ik + a/ | ———————— | [tuŋgika] |
| /Pɛnd + ik + a/ | ————→ | [pɛndɛka] |
| /kɛr + ik +a/ | ————→ | [kɛrɛka] |
| /sɔm +ik + a/ | ————→ | [sɔmɛka] |
| /tʃɔm + ik + a/ | ————→ | [tʃɔmɛka] |

Kwa mujibu wa data hiyo vilevile irabu kaze /a /, / i /, / u / za mzizi ya vitenzi inakubaliana na irabyu kaze [ i ]ya kinyambuhishi. Nazo irabu hafifu / ɛ /, /ɔ / za mizizi ya vitenzi zinakubaliana na irabu hafifu [ɛ] ya kinyambulishi katika Kiswahili peke yake.

**Kiswahili**

| **Irabu ya mizizi ya vitenzi** | | **Irabu ya Kinyambushi** |
|---|---|---|
| /a/ | ———— | [ ik ] |
| /i/ | ———— | [ ik ] |
| /u/ | ———— | [ ik ] |
| /ɛ/ | ———— | [ ɛk ] |
| /ɔ/ | ———— | [ ɛk ] |

Kwa jumla kuna mshabaha mkubwa wa upeo wa sheria hii ya mkubaliano wa irabu kati ya Kiswahili na Kidawida ililinganishwa na tofauti baina yao.

## 5.14 MKUBALIANO WA NASALI NA KITAMKWA KINACHOFUATA

Badiliko hili hutokea katika Kidawida na Kiswahili. Aghalabu huhusu ngeli nomino ya 9/10 za lugha hizi mbili kwa mfano.

**Kiswahili**

46

/N + bɔga/ ——→ [mbɔga]
/N + wili/ ——→ [mbili]
/N + gɔma/ ——→ [ŋgɔma]
/N + gumu/ ——→ [ŋgumu]
/N + tʃi/ ——→ [ɲtʃi]
/N + dizi/ ——→ [ndizi] ?

**Kidawida**

47

| | | | Maana |
|---|---|---|---|
| /N + βoɣɔ/ | ⟶ | [mbɔɣɔ] | nyati |
| /N +βɔβa/ | ⟶ | [mbɔβa] | shamba |
| /N + ɣɔndi/ | ⟶ | [ŋgɔndi] ⟶ [ŋɔndi] | kondoo |
| /N + ɣatʃa/ | ⟶ | [ŋgatʃa] | ndama |
| /N + lazi/ | ⟶ | [ndazi] | nyingi /nzima |
| /N + lɛmɔ/ | ⟶ | [ndɛmbɔ] | mgomba |
| /N + ɔni/ | ⟶ | [ɲɔni] | nyuni |
| /N + jau | ⟶ | [ɲjau] | fahali |

Kulingana na data hiyo, tunaona sauti ya nasali /N/ ambayo ni kiambishi cha ngeli nomino 9/10, ikibadilika katika mazingira tofautitofauti, katika Kidawida na Kiswahili,

48

/N/ ——— [ m – / ŋ – / n – / n – ] / ——— / b/w/β, g/ɣ, j/tʃ, d/l /

Kwa hiyo upeo wa sheria hii unalingana katika lugha hizi mbili.

## 5.15 KUIMARIKA KWA SAUTI

Badiliko hili hutokea katika Kiswahili na Kidawida. Kwa mfano

**Kiswahili**

49

| | | |
|---|---|---|
| /N + limi/ | ⟶ | [ndimi] |
| /N + lɔa/ | ⟶ | [ndɔa] |
| /N + lɔtɔ/ | ⟶ | [ndɔtɔ] |
| /N + rɛfu/ | ⟶ | [ndɛfu] |
| /N + wili/ | ⟶ | [mbili] |

**Kidawida**

| | | | Maana |
|---|---|---|---|
| 50 | /N + lɛ:/ → | [ndɛ:] | babake |
| | /N +lɔ:/ → | [ndɔ:] | mchanga |
| | /N + rifu/ → | [ndifu] | nono |
| | /N + βandɛ/ → | [mbandɛ] | kuni |
| | /N + βiʃi/ → | [mbiʃi] | mpya |
| | /N + ɣukɔ/ → | [ŋguku] | kuku |
| | /N + ɣuβɛ/ → | [ŋguβɛ] | nguruwe |

Kwa majibu wa data hiyo badiliko la kuimarika kwa sauti katika Kiswahili linahusu sauti /i/ /r/ na /w/ amabzo hubadilika na kuwa /d/ na /b/

51 / l/r, w / → [d, b] / N -

Katika kidawida badiliko hili lina upeo mpana zaidi kwani lina upeo mpana zaidi kwani linahusu sauti / l / / r / / β / na / ɣ / zinazobadilika na kuwa [d ] [b] na [g]

52 / l/r, β, ɣ / → [d, b, g] / N -

Mbali na kuwa lugha hizi zinafanana katika kuimarisha sauti za likwidi /i/ na /r/, vilevile zinatofautiana katika peo za sheria kwani Kiswahili pia kinaimarisha nusu-irabu /w/ ilhali Kidawida kinaimarisha sauti za / β / na / ɣ/ kwa ujumla kidawida kina upeo mpana zaidi, wa sheria hii kuliko Kiswahili.

## 5.16 HITIMISHO

Tutasema kwamba upeo wa sheria za Kiswahili na Kidawida zinalingana kwa kiasi kikubwa. Sauti nyingi zinazobadilika katika Kiswahili pia zinabadilika katika Kidawida kwenye mifanyiko mbalimbali. Kwa mfano badkiliko la ukaakkashaji katika kiswahili na kidawida linahusu sauti [k] inayo badkilika na kuwa [ tʃ ]. Vilevile badkiliko ls kudondolewa kwa irabu katika kiswahili na kidawida linahusu irabu /u/ /a/ na /i/ katika miktdha mbalimbali. Aidha badiliko la mkubaliano wa nasali na kitamkwa kinachofuata katika Kiswahili na Kidawida linahusu sauti ya nasli /N/ inayobadilika na kuwa na sura mbalimbali. Pamoja na hayo badiliko la kuimarika kwa sauti katika lugha hizi mbili inahusu sauti /l/ na /r/ zinazobadilika kuwa [d]. Hata hivyo hapa tunaona kuna tofauti kidogo kwani Kiswahili kinaimarisha /w/ huku Kidawida kikiimarisha / β / na / ɣ / mbali na zile likwidi. Tena Kidawida kina idadi kubwa zaidi ya sauti zinazoimarika kuliko Kiswahili.

Matokeo haya yanakanusha nadharia tete ya tatu. Nadharia tete hiyo ilisema kwamba kuna tofauti za upeo na motisha ya mabadiliko baina ya lugha hizi mbili. Kwanza tuliona kuwa mengi ya mabadiliko katika Kiswahili na Kidawida ni ya kutarajiwa kuambatana na motisha pili tumeona vile peo za sheria mbalimbali za kifonolojia katika Kidawida na Kiswahili zinalingana. Hivyo basi kwa kiasi kikubwa motisha na upeo wa sheria katika Kiswahili na Kidawida zinalingana kuliko kutofautiana.

## TANBIHI

1. J. B Hooper (1976), An Introduction to Natural Generative Phonology. New Academic Press.

2. Larry Hyman (1975), Phonology: Theory and Analysis New York: Holt, Reinhart And Wilson.

3. Roger Lass, (1984), Phonology: An Introduction to Basic Concepts Cambridge University Press. Cambridge, London, New York, New Rochelle, Melbourne, Sydney. 196

4. J.B. Hooper (opp. Cit).

* KGV - konsonanti, nusu – irabu, irabu.
* KVV – konsonanti, irabu, irabu

# SURA YA SITA

## 6.0 UTANGULIZI

Katika sura hii tuna lengo la kuorodhesha matokeo ya utafiti huu. Vile vile tutatoa maoni au mapendekezo yanayohusiana na lugha za Kiswahili na Kidawida.

## 6.1 MUHTASARI WA MATOKEO

Katika utafiti huu tumeona kuwa kidawida kina fonimu 36 zikiwemo konsonanti 29 ina irabu 7. Kati ya hizo fonimu za konsonanti ni 8 pekee ambazo ni isoghuna.

Aidha tumeona kuwa kidawida kina ngeli nomino 18 zikiwemo :-

1. { mu-} 2. {βa-} 3. {mu-} 4.{mi-} 5.{ku-} na {ku-}

6. {ma-} 7.{ki-} 8 {vi-} 9.{N-} 10.{N-} 11. {lu-}

12. {ka-} 13.{tʃu-} 14. {βu-} 15.{ku-} 16. aha 17.aja

18.ahɔ.

Pamoja na hayo tumeona mifanyiko 6 ya kifonolojia inayotokea katika kidawida. Hizi ni pamoja na kudondoshwa kwa irabu, uundaji wa nusu –irabu, uaakaishaji, mkubaliano wa irabu, kuathiriwa kwa nasali na kitamkwa kinchofuata na kuimarika kwa nasali kwa sauti. Kati mifanyiko hiyo, ni miwili pekee ambayo inhusu rabu ilhali minne inhusu konsonanti. Kwa hivyo inabainika kuwa mifnyiko mingi katika kidawida inruhusu sauti za konsonanti.

Vilevile tumeona mifumo ya fonimu za Kiswahili na Kidawida zinavyoshabiliana na kutofautiana kwa fonimu 5 za irabu na 28 za konsonanti, huku zikitofautiana kwa irabu 2 na konsonanti 11. Matokeo hayo yameonyesha kuwa lugha hizi mbili zinakaribiana kuliko zinavyotofautiana kama inavyoonekana katika ukurasa ufuatao.

## Irabu

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| X | X | | X | X | | X |
| a | | ɛ | e | i | o | ɔ |
| Y | Y | Y | Y | Y | Y | Y |

## Konsonanti

| | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | x | | | | | x | x | x | x |
| p | b | ɓ | t | d | j | k | g | β | f | v | θ | | ʃ | s | z | ɣ | h | tʃ | m | n | n | ŋ | $^{m}b$ | $^{n}d$ | $^{n}ɟ$ | $^{ŋ}g$ | l | r | w | J |
| Y | Y | Y | Y | Y | Y | Y | Y | Y | Y | Y | Y | Y | Y | Y | Y | Y | Y | Y | Y | Y | Y | Y | Y | Y | Y | Y | Y | Y | Y | Y |

Kiswahili - X
Kidawida - Y

Pia tumeona vile lugha hizo zilivyosonga mbali kutoka kwa Bantu –mzazi. Tumepata kwamba Kiswahili kimekosa fonimu 6 za Bantu – mzazi, nacho Kidawida kimekosa fonimu 5 za Bantu-mzazi. Kwa kutumia kigezo hicho Kiswahili ndicho kiko mbali zaidi na Bantu – mzazi kuliko Kidawida kama inavyoonekana katika ukurasa unaofuata.

## IRABU

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | X | X | X | X | X | X | X |
| B-m | a | *e̠ | i | î | û | u̠ | *o̠ |
| | Y | Y | Y | | | Y | Y |

**X - Kiswahili**
Y – Kidawida
B –m Bantu – mzazi
* e̠ na o̠ ni sawa na ɛ, ɔ
* k̠, t̠, ɣ̠, l̠, ni sauti zilizokaakaishwa.
* k̠, ni sawa na tʃ



**Konsonanti**

| | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | X | X | X | X | | X | X | | | | X | X | X | X |
| B-m | k | t | p | * k̠ | *t̠ | ɣ | l | β | ɣ | *l̠ | n | m | w | j |
| | Y | Y | Y | Y | | Y | Y | Y | | | Y | Y | Y | Y |

Zaidi ya hayo tumeona mshabaha uliopo wa motisha katika mifanyiko ya Kiswahili na Kidawida. Tumeona kwamba motisha ya mabadiliko hayo ni kanuni za muundo mwafaka wa silabi, usilimisho na kutengana kwa sauti kadiri inavyowezekana. Kwa hivyo mabadiliko ya kifonolojia katika Kiswahili na Kidawida na ya kutarajiwa.

Mwisho tumeona kuna kiasi kikubwa cha mshabaha wa upeo wa sheria katika Kiswahili Kidawida. Tofauti inapatikana kwenye mifanyiko michache ambayo ni mkubaliano wa irabu na kuimarika kwa sauti vilevile tumeona kuwa badiliko la kudhoofika kwa sauti linatokea katika Kiswahili lakini halitokei katika Kidawida. Kwa jumla lugha hizi mbili zinalingana sana kwa motisha na upeo wa sheria.

UPEO WA SHERIA

| Kiswahili | Mifanyiko ya Kifonolojia | Kidawida |
|---|---|---|
| u, i, a | Kidondoshwa kwa irabu | u, i, a |
| u, i | Uundaji wa nusu – irabu | u, i |
| k | Ukaakaishaji | k |
| a, i, u ; ɛ, ɔ | Mkubaliano wa irabu | a, i, u ; ɛ, ɔ |
| n | Kuathiriwa kwa nasali | n |
| l, r, w | Kuimarika kw sauti | l, r, β, ɣ |
| p, b, t, d, k, g, | Kudhoofika kwa sauti | - |

## 1. 2 MAPENDEKEZO

Utafiti huu umekumbwa na matatizo kadha. Tatizo la kwanza linahusu undondoshi wa irabu /u/ katika ngeli 1 ya Kidawida. Utafiti wetu umegundua kwamba badiliko hili ambalo ni la kihistoria limetokea katika Kidawida,lakini

Zaidi ya hayo tumeona mshabaha uliopo wa motisha katika mifanyiko ya Kiswahili na Kidawida. Tumeona kwamba motisha ya mabadiliko hayo ni kanuni za muundo mwafaka wa silabi, usilimisho na kutengana kwa sauti kadiri inavyowezekana. Kwa hivyo mabadiliko ya kifonolojia katika Kiswahili na Kidawida na ya kutarajiwa.

Mwisho tumeona kuna kiasi kikubwa cha mshabaha wa upeo wa sheria katika Kiswahili Kidawida. Tofauti inapatikana kwenye mifanyiko michache ambayo ni mkubaliano wa irabu na kuimarika kwa sauti vilevile tumeona kuwa badiliko la kudhoofika kwa sauti linatokea katika Kiswahili lakini halitokei katika Kidawida. Kwa jumla lugha hizi mbili zinalingana sana kwa motisha na upeo wa sheria.

UPEO WA SHERIA

| Kiswahili | Mifanyiko ya Kifonolojia | Kidawida |
|---|---|---|
| u, i, a | Kidondoshwa kwa irabu | u, i, a |
| u, i | Uundaji wa nusu – irabu | u, i |
| k | Ukaakaishaji | k |
| a, i, u ; ɛ, ɔ | Mkubaliano wa irabu | a, i, u ; ɛ, ɔ |
| n | Kuathiriwa kwa nasali | n |
| l, r, w | Kuimarika kw sauti | l, r, β, ɣ |
| p, b, t, d, k, g, | Kudhoofika kwa sauti | - |

## 1. 2 MAPENDEKEZO

Utafiti huu umekumbwa na matatizo kadha. Tatizo la kwanza linahusu undondoshi wa irabu /u/ katika ngeli 1 ya Kidawida. Utafiti wetu umegundua kwamba badiliko hili ambalo ni la kihistoria limetokea katika Kidawida,lakini

halikutokea kwenye lahaja nyingine za lugha ya Kidawida. Hata hivyo kwa sababu ya muda mfupi tuliokuwa nao, hatukuweza kufanya uchunguzi zaidi kuhusiana na suala hilo. Tunapendekeza utafiti zaidi ufanywe ili kulitatua tatizo hilo.

Aidha tunapendekeza utafiti zaidi ufanywe kuhusina na utamkaji wa baadhi ya maneneo kama Kidawida, kulingana na utafiti wetu, maneno kama vile [mburi], [mbuβa ] hutamkwa na [ u ]. Kuna hoja kuwa huenda maneno haya yanatamkwa na [ o ] badala ya [u],yaani [ mburi ] na [moβa ]. Hili ni suala ambalo hatukuweza kulishughulikia kwa sababu ya muda. Tunapendekeza kwamba jambo hili lishughulikiwe kwa undani zaidi.

## 6.3 HITIMISHO

Tumeona kuwa mifanyiko mingi ya kifonolojia katika Kiswahili ni ya kutarajiwa, pamoja na michache isiyokuwa ya kutarajiwa. Mifanyiko tuliyoiona ni pamoja na udondoshi wa irabu, uundaji wa nusu – irabu, ukaakaishaji, mkubaliano wa irabu, kuathiriwa kuwa sauti, na kudhoofika kwa sauti miongoni mwa mifanyiko kwa sauti. Miongoni mwa mifanyiko hiyo ni badiliko la kudhoofika kwa sauti peke yake ambalo si la kutarajiwa katika Kiswahili.

Kwa upande wa Kidawida tumeona kuwa mabadiliko yote ya kifonolojia ni ya kutarajiwa. Kwa hivyo lugha za Kibantu zinaonekana kuwa na mifanyiko mingi ya kifonolojia yenye kutarajiwa kuliko ile isiyokuwa ya kutarajiwa. Tumeweza kuyaona haya kupitia kwa nadharia ya fonolojia zalishi asili ya Joan B. Hooper (1976). Nadharia hii imetusaidia kuona mabadiliko yanayotokea katika Kiswahili na Kidawida. Kuambatana na matokeo tuliyoyapata tumeweza kuibuka ma kauli kwamba lugha za kibantu aghalabu huwa na mifanyiko ya kutarajiwa zaidi ya ile mifanyiko isiyokuwa na za kimofofonolojia ambazo zimemulika aina za mabadiliko ya kifonolojia yatokeayo katika Kiswahili na Kidawida.

<u>MAREJELEO</u>


1. Abercrombie, David (1967), <u>Elements of General Phonetics</u> Edingburgh University Press 22 George Square, Edinburgh.

2. Chomsky, Noam (1965) <u>Aspects of the theory of Syntax</u> Cambridge M. I. T. Press

3. Noam (1965), <u>The Classification of the Bantu Languages</u> London, International African Institute, Oxford University Press

4. Harms Robert (1968), <u>Introduction to phonological Theory</u> prentice – Hall- inc Eaglewood, London and New York

5. Horrocks, Geoffrey (1987) <u>Generative Grammar,</u> Longman London and New York

6. Hooper, J. B. (1976) <u>An Introduction to Natural Generative Grammar</u> New York Academic Press

7. Hyman, L. M. (1975) <u>Phonology: Theory and Analysis</u> Holt, Rinnehart and Winston, Inc.

8. Karega, E.K. (1977) "Sound Change and Classification of the dialects of Southern Mt. Kenya PhD Thesis, University of Nairobi

9. Kithaka wa Mberia (1981) " The Consonants of Kitharaka" M. A. Thesis University of Nairobi.

10. Maganga C. (1990), "The Morphophology of Standard Kiswahili, Kimakunduchi, Kitumbatu and Kipemba

11. Maringah, E. I (1987) "A Comparative Analysis of Verbal Extension in Kimbeere and Kiswahili" M. A Thesis. University of Nairobi.

12. Mukuria, D. M. (1987) "Mpangilio wa ngeli: ulinganishi wa ngeli za kiswwahili sanifu na kikikuyu cha kiambu M.A. Thesis., University of Nairobi

13. Maundu, P. M (1980) "Sound change and the reconstruction of Kikamba consonantal sounds in NGP framework.

M.A Thesis University of Nairobi

14. Meinhof, Carl (1932) Introduction to the phonology of the Bantu languages. Deitrich Reimer Ernst Vohsoen/Berlin

15. Mgullu R.S. (1999) Mtalaa wa Isimu Longhorn Publishers Kenya Limited

16. Mkangi George, C (1975) "The Wataita: From Community to Individualization - An Introductory observation

17. Mohammed, Bakari (1982) " The Morphology of the Kenyan Swahili dialects" PhD Thesis University of Nairobi

18. Mwakio James (1975) "Lines of inquiries into the origin and culture of the wataita in a completiono f seminar papers.

19. Njunguna, Margaret (1992) "Mofofonolojia ya Kiswahili sanifu na kikikuyu sanifu: mathalani Kikikuyu cha kabete: Ulinganishi M. A Thesis University of Nairobi.

20. Polome, Edgar,C (1967) Swahili language Handbook Centre for Applied Linguistic 1717 Massachusetts Avenue, N. W. Washington, D.C 20036.

21. Righa, G. (1978), "A Preliminary analysis of some registers in Taita

21. Schane, Sanford A. (1973) "Natural Rules in Phonology "Katika R.P Stockwill na Ronald K.S Macaulay (wahariri), Lingustic change and Generative Theory Bloomington, Indiana University Press

22. TUKI (1990) Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam